ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini – Tarehe 25 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Naibu wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kwa kuamka salama. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani ya hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2013/2014. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naomba kuwasilisha hati mezani ya hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaanza na majadiliano; tunaanza na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na baadaye atafuata Mhe. Ali Salum Haji na ajitayarishe Mhe. Asha Bakari Makame. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Mwenyekiti, naona leo ni Ramadhani ya 16 na sijui kama tunashuka tunapanda, lakini tunashuka na ndio rahisi zaidi naona wewe bado unapanda.

Utangulizi:

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu, kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kukutana hapa katika Baraza letu tukufu, tukiwa katika hali ya uzima na afya kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu na taifa kwa ujumla. Aidha napenda kukushukuru kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza hili kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kuweza kuiteua Kamati hii ya Mifugo, Utalii Uwezeshaji na Habari na kuipatia wajumbe mahiri na makini ambao wanafanya kazi kwa kujituma. Aidha kamati katika utendaji wake wa kazi katika wizara zote imepokelewa vizuri na kutokana na hilo kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuziahidi wizara hizo kuwa kamati imeridhishwa na mapokezi yao na itaelendeleza mashirikiano hayo kwa muda wote wa uhai wa kamati.

Aidha nisiwe mkosefu wa shukurani kwa kutowashukuru wajumbe wa kamati hii kwanza kwa kunipa imani yao ya kunichaguwa kuwa Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii yenye majukumu muhimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia sina budi kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii Uwezeshaji na Habari, pamoja na Makatibu wa Kamati hii kwa kuonesha ushirikiano mzuri katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa ya kusimamia utekelezaji wa wizara zinazosimamiwa na kamati hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu niwataje Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Moh'd Ali	-	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Bakari Makame	-	Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5. Mhe. Kazija Khamis Kona	-	Mjumbe
6. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mjumbe
7. Mhe. Asaa Othman Hamad	-	Mjumbe
8. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali	-	Mjumbe
9. Ndg. Maryam Hussein Rajab	-	Katibu
10.Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo napenda sasa nitoe Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, tunapenda kuipongeza serikali kwa uamuzi wake wa kuweka wizara inayoshughulikia masuala ya uvuvi, ambayo ndio njia kuu ya ajira kwa wananchi wetu. Tegemeo letu ni kuwa serikali iliona umuhimu mkubwa wa kuwepo wizara hiyo, pamoja na nia njema ya serikali, kamati inasikitika kuona kuwa wizara hii imekuwa kama idara kutokana na kuwekewa kasma ndogo ambayo inashangaza sana, kiasi kwamba umuhimu ule wa mwanzo wa kuunda wizara hii haupo tena.

Mhe. Mwenyekiti, tokea makadirio ya 2012/2013 lengo kuu la serikali ni kuingia Uvuvi wa Bahari Kuu na serikali ilitenga shilingi milioni 500 kwa lengo la kununulia boti pamoja na kutoa mafunzo kwa wavuvi watakaotumia boti hizo. Mhe. Mwenyekiti, hadi kamati yako inapitia Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka 2013/2014 boti hizo hazijanunuliwa kwavile gharama za ununuzi wa boti hizo umekuwa mkubwa zaidi.

Hivyo, kamati kwa kuona umuhimu wa upatikanaji wa boti hizo kamati yako iliomba muda wa ziada za kupitia mswada wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa lengo la kukutana na Uongozi wa Wizara ya Nchi (OR) Fedha,Uchumi na Mipango ya Maendeleoa na kupatiwa maelekezo kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeruhusiwa kununua boti moja kama ni *pilot*. Hata hivyo, kama kutaonekana kuna tija Wizara ya Fedha itatoa pesa katika Mfuko wa MDRI kwa lengo la kununua boti nyengine ili iweze kuzidisha ufanisi katika kazi hizo za patroo na nyenginezo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi ijenge tabia ya kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pindi inapotembelea wajasiriamali wake, kwani kumejitokeza tatizo la wajasiriamali wingi hususani wale wanaojishughulisha na kazi za Ufugaji wa Samaki, kutofahamu kuwa kuna wataalamu wa kizalendo, ambao wanapatikana hapa Zanzibar .

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza sana wizara kwa kufanikiwa kuibua miradi mbali mbali ya maendeleo, kama vile mradi wa Uvuvi wa Bahari Kuu wenye lengo la kukuza uchumi wa nchi kwa kuanzisha njia nyengine ya ukusanyaji wa mapato kwa serikali na pia kuvumbua ajira kwa wananchi walio wengi hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imesikitishwa kwa kiwango kidogo cha fedha kilichowekwa, hasa ukizingatia kuwa mradi huo utajumuisha ununuzi wa boti za kisasa pamoja na kutoa mafunzo kwa wananchi. Kwa hivyo, kiwango hicho kidogo walichotengewa hakitowawezesha kutimiza malengo yao waliyojipangia na itasababisha hicho kifungu cha fedha walizotengewa kutumika vibaya na hazitoleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaharakisha kuletwa kwa Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu, ili iweze kupata baraka za waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa lengo la kuiharakiza ianze kazi ili nchi yetu ianze kunufaika na mradi huo. Mhe. Mwenyekiti, naomba ifahamike kuwa sisi tunaishi katika visiwa ambavyo vimejaaliwa kuwa na bahari yenye kina kirefu na pia yenye eneo kubwa la mraba, hivyo katika mradi huu wazanzibari tutaneemeka sana na tutaweza kupunguza umasikini ambao umetawala katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imesikitishwa na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kwa kitendo wanachofanyiwa wavuvi wetu wanaotumia uvuvi wa kienyeji kudaiwa kukata leseni mara mbili. Mhe. Mwenyekiti, wavuvi wetu hua wanakata leseni ya mwaka mzima Unguja na wanapotoka nje ya Unguja na kuelekea Tanzania Bara kwenda dago pia hua wanakata leseni tena. Kwa kweli hili ni tatizo hasa ukizingatia wavuvi wenyewe kipato wanachokipata ni kidogo hakitoshelezi hata kukuza mitaji yao na bahari yenyewe ndio hiyo hiyo moja.

Kutokana na hali hiyo, serikali ianzishe utaratibu mwengine ili kuwalinda wavuvi wetu kutokatishwa leseni mara mbili, hasa ukizingatia uvuvi wanaotumia sio wa Bahari Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kuzidisha bidii kwa kuzidisha umakini katika makusanyo yake, ili iweze kukusanya zaidi ya kiwango hicho walichojipangia kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imefurahishwa na Idara ya Mazao ya Bahari kwa kufanikiwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya baharini na pia kwa kukamilisha ujenzi wa bwawa moja la mfano au bwawa darasa (*Demonstration Pond*) katika eneo la Jozani Mkoa wa Kusini Unguja na kukabidhiwa wajasiriamali kwa Ufugani wa Samaki.

Hata hivyo kamati inaishauri Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuengezea fedha katika kifungu numbari 0012 Idara ya Mazao Baharini Pemba, ambayo imetengwa jumla ya shilingi

75,500,000/=, ili idara iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kama ilivojipangia katika malengo yake ya mwaka 2013/2014. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kiwango hicho ni kidogo hasa ukizingatia majukumu ya idara hiyo ni makubwa, hii inadhihirisha kuwa serikali yetu bado haijajua umuhimu wa mazao ya bahari katika kukuza pato la taifa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Idara ya Uzalishaji Mifugo kwa kuyapatia huduma muhimu mashamba na vituo vya utafiti wa mifugo hasa Kitumba, Chamanangwe na Pangani ikiwemo huduma za kinga na tiba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nchi yetu haina sababu ya kuagiza mifugo kutoka nchi za nje, ikiwa serikali yetu itaamua kwa makusudi kutoa kipaumbele katika sekta hii muhimu, ikiwa ni pamoja na kuwazidishia kiwango cha fedha, ili kazi zifanyike kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo ina jukumu kubwa katika taifa letu, hasa ukizingatia kila kukicha kunaibuka aina mpya ya maradhi huko duniani na kusababisha mifugo mingi kufariki na maradhi kusambaa duniani kote ikiwa pamoja na kuwasababishia matatizo watumiaji wa mifugo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imefurahishwa na idara hii kwa kufanikiwa kukagua wanyama 372,953 kati ya wanyama hao ngombe ni 5,124, mbuzi 118, kuku (vifaranga vya mayai na nyama) 367,925 na wanyama wengine 70. Mhe. Mwenyekiti, imeridhishwa na kiwango cha fedha walichoekewa ila tunasisitiza fedha hizo zilizoidhinishwa ziwe zinatolewa kwa wakati na kwa asilimia zote 100%

Mhe. Mwenyekiti, kamaiti imefurahishwa na wizara hii kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika maziwa na kuzalisha siagi na mtindi. Hatua hii ni muhimu kwani itawawezesha wafugaji kuongeza thamani kwenye maziwa mara baada ya kuyasarifu na hatimaye kupata faida kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kupatiwa taaluma wavuvi pamoja na kuimarishwa kwa miundo mbinu ya uvuvi hatua kwa hatua, basi kamati yetu inaiomba wizara isibweteke na ifanye kazi kwa juhudi na iendelee zaidi kwa michango yake kwa wananchi. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Sekta ya Uvivu ilichangia kwa asilimia 6.7 kwenye pato la taifa. Kiwango hichi kinatarajiwa kuongezeka katika mwaka wa fedha 2013/2014 kwa kuendelezwa juhudi za serikali na wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri vipaombele katika wizara viwe vichache, ili kuleta ufanisi, ikiwa wizara itaweka vipaumbele zaidi ya kimoja maana yake tutashindwa kufikia lengo hasa ukizingatia serikali yetu ni changa na hata hicho kidogo kinachotolewa huwa hakipatikani kwa wakati. Kwa hivyo, kuna haja ya kubadilika tabia na sio kufanya kazi kwa mazoea.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi hususan kwa upande wa Afisi ya Pemba kuwa na ubunifu wa miradi mbali mbali itakayoingiza mapato kwa maslahi ya wizara na taifa kwa ujumla, badala ya kutegemea ada ya inayopatikana na huduma za utibabu wa mifugo, uzalishaji mifugo, leseni za uvuvi na ushuru wa usafirishaji wa mazao ya baharini pekee, ambao kwa mwaka huu wa fedha inatarajiwa kukusanya shilingi 45,000,000/=. Kiwango hichi ni kidogo mno hasa tukizingatia mahitaji makubwa ya wizara hii changa ambayo inahitaji kujiimarisha kwa kuanzia na rasilimali watu na vyombo vya usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi ni moja kati ya sekta muhimu sana katika kuikwamua nchi yetu kiuchumi kutokana na kuwemo kwa rasilimali muhimu katika sekta hiyo hususan mazao ya baharini kama vile samaki. Vile vile kamati ilipata nafasi ya kuonana na viongozi na watendaji wa Idara ya Uvuvi na kubadilishana uzoefu juu ya njia bora za uvuvi wenye tija kwa lengo la kutunza mazingira ya bahari.

Aidha uvuvi husaidia sana katika kuimarika kwa Sekta ya Utalii. Hivyo ni vyema serikali ikatilia mkazo zaidi katika uhifadhi wa bahari hususan suala la kufanya doria. Sambamba na hilo ufanyaji wa doria katika fukwe utasaidia kuzuia uvamizi wa bahari yetu unaofanywa na meli za nje kuja kuvua kinyume na sheria. Kwa mnasaba huu kamati inaomba serikali kuingiza fedha za kutosha katika fungu la mafuta kwa ajili ya doria ya baharini.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kuwa idadi ya wavuvi sasa imeongezeka kwa kiasi kikubwa na ambao uwezo wao ni wa kuvua uvuvi wa ndani tu na eneo wanalovua kwa sasa limekuwa dogo. Kwa hivyo, kuna haja kubwa kwa serikali kuona umuhimu wa kuanzisha chuo maalum cha hapa Zanzibar, ili vijana wawe na taaluma ya kutosha kwa uvuvi wa kisasa na ule wa bahari kuu, ambao utahitaji elimu ya kuendelsha meli za uvuvi, matumizi ya mbinu na vifaa vya kisasa vya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwepo haja ya kuanzisha Chuo cha Uvuvi, kuna haja pia ya kuwawezesha wavuvi waliopo kwa kuwapatia nyenzo zikiwemo mashine za kisasa, ili angalau waweze kwenda mbali zaidi ya wanapokwenda sasa kwa ajili ya shughuli zao za uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri wizara kuwaelimisha wakulima wetu wa mwani njia nzuri ya kulima na kuanika, kwani njia ya ukilima unaotumika hivi sasa kwa wakulima wetu wa mwani ni ule ukulima wa mwani kwa kutumia vijiti, ambao athari yake kubwa ni kuharibu mazingira kwa huharibu mazalia ya samaki, hupunguza kina cha bahari kwa kusababisha kufanyika kwa mafungu (mkusanyiko wa mchanga). Kutokana na hali hiyo na tukizingatia kuwa tija ya mwani imeongezeka kwa kasi, ni vizuri kwa serikali kuandaa mazingira bora zaidi yatakayowasukuma wananchi kuimarika kiuchumi bila ya kuleta athari za aina yeyote kama vile ufugaji wa samaki na chaza.

Mhe. Mwenyekiti, uhifadhi wa viumbe wa bahari ni suala muhimu linalotiliwa mkazo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwa mantiki hiyo basi kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuzitatua changamoto za sekta, hii kama vile uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi za doria unaopelekea kuanza tena kwa uvuvi haramu pamoja na bajeti ndogo isiyoweza kuleta mafanikio yanayotarajiwa katika MKUZA na Dira 2020.

Mhe. Mwenyekiti, napenda sasa kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu, pia napenda kukushukuru kwa mara nyengine tena wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii,Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kutamka kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkoani ninaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Aidha nawaomba Wajumbe wote wachangie na kuunga mkono Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii, kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu na malengo waliyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maoni hayo na kwa niaba ya kamati, niwaombe sasa Wajumbe wenzetu wa Baraza lako tukufu, wakubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2012/2013 kama wizara ilivojipangia.

Aidha nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuiunga mkono bajeti hii kwa upande wa kazi za kawaida na kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ahsante. Sasa tunaendelea na wachangiaji na tunaanza na Mhe. Ali Salum Haji na baada ya hapo tunampisha Mhe. Asha Bakari Makame na pia ajitayarishe Mhe. Subeit Khamis Faki. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subuhanahu Wataalla* kwa kutujaalia afya njema tukaweza kusimama asubuhi ya leo katika kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Vile vile nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika siku hii ya leo katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nimshukuru Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa namna wanavyosimamia wizara yao pamoja na Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ambayo inaongozwa na Mhe. Mlinde Mbarouk Juma pamoja na Abdalla Moh'd Ali ambaye ni Makamo Mwenyekiti na ameweza kutuwasilishia maoni kamati yao.

Naomba nianze mchango wangu katika sekta ya mifugo. Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 5(c) naomba ninukuu kidogo.

> " 5 (c) Wizara ina malengo ya kuongeza ajira kwa vijana kupitia shughuli za uzalishaji mifugo".

Mhe. Mwenyekiti, moja ya shughuli za uzalishaji wa mifugo basi ni ufugaji wa kuku. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi aje anisaidie, kwamba ile dhamira ya kuongeza ajira wakati leo hii tumeruhusu kuingia kuku wa *PEDUU* na wengine mimi na kuwa napata mashaka kwamba hii dhamira kweli itapatikana. *(Makofi).*

Kutokana na hali hii, vijana pamoja na wazee wetu wanalalamika sana hivi sasa, kwamba wanatumia gharama kubwa za ufugaji na matokeo yake soko lao inakuwa halitambulikani, sasa baada ya kupata faida na ajira na matokeo yake imekuwa wanapata hasara. Kwa kweli wanaoleta kuku hawa wamekuwa wamo katika njia ya ushindani.

Sasa mfanyabiashara uchumi wake unakua mkubwa tofauti na ndugu au vijana wetu ambao uwezo wao wa kufuga unakuwa ni mdogo. Lakini kwa upande mmoja inasaidia wananchi katika suala zima la kupata kitoweo na kwa upande wa pili inakuwa ni tatizo kwa wafugaji wetu. Hata hivyo, tuna wasi wasi kwamba huwenda wafugaji wetu wakafika pahala wakakata tamaa

kabisa katika suala la ufugaji wa ukuku. Mhe. Mwenyekiti, naombo Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kuwa hii dhamira ya kuwasaidia na hususan wafugaji wa kuku wizara imejipanga vipi na ushindani wa kibiashara na kuku wa PEDUU.

Nikiendelea na mchango wangu namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja hapa anisaidie, hivi sasa kumekuwa na manung'uniko makubwa katika suala zima la nyumba za mifugo, nyumba zilizoko Mazizini na nyumba zilizoko katika eneo la Chumbuni. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nyumba hizi lengo na dhamira ni kukaa watendaji na maafisa wa sekta husika lakini tuna wasi wasi kwamba kuna watu ambao wamezihodhi nyumba hizi na kwa muda mrefu wamekuwa wanapigiwa kelele kutoka kwenye nyumba hizi na bado hawajatoka na kuleta ugumu kwa wale watendaji kuweza kuzitumia, kwa ajili ya kufanya kazi zao kwa wepesi na ufanisi na yale malengo ya serikali kuziweka nyumba zile katika hali halisi. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja Mhe. Waziri naomba anisaidie kwamba suala hili la wale watu ambao wameamua kukaa katika nyumba hizi kwa muda mrefu na kukataa kutoka na kuzuia wale watendaji wanaohusika ambao wanapaswa kutumia nyumba zile limefikia wapi na lini watu wale watatoka katika nyumba zile. Nikiendelea na suala hilo la mifugo na ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja hapa anisaidie kwamba tangu mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, nimekuwa nikilipigia kelele sana katika dhana ya mashamba ya mifugo kuvamiwa na mengine kuhodhiwa na baadhi hata kuchukuliwa na watu katika namna mbali mbali. Sasa mwaka jana nilipiga kelele na mwaka huu bado naingia mashaka.

Kwa hivyo, hapa Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri ajitayarishe vya kutosha na wala sina dhamira ya kuzuia bajeti hii kwa sababu Mhe. Waziri ninamfahamu kwamba ni mtendaji na Mhe. Naibu Waziri wake ni mwenzangu wa karibu, lakini katika hili ajitayarishe vya kutosha na kuja kunipa majibu sahihi ambayo yatanifanya kuweza kuipitisha bajeti hii na kuiunga mkono kwa asilimia mia moja, vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti hapa sitaridhia.

Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti, nataka anisaidie kwamba shamba la Kisakasaka limefikia hatua gani katika kupata hati miliki. Vile vile nataka anisaidie na nilizungumzia suala zima kuhusu shamba la Kitumba la ufugaji kuvamiwa. Hivi ni hatua gani za wizara zimechukuliwa kuweza kuondosha watu ambao wamevamia shamba lile.

Sambamba na hili pia nilizungumzia kwa kina kabisa suala zima la shamba la ufugaji la Tunguu. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nilielezea kwamba kuna eneo ambapo mtu mmoja amechukua zaidi ya hekta 1,000 na mwaka huu tayari kuna baadhi ya maeneo tayari kuna watu wameshaanza kulihodhi hilo shamba.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi anieleze ni nani ambao wamehodhi eneo lile na kwa misingi gani na wizara imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba wale ambao wamehodhi basi ni kuwachukulia hatua na kuwaondosha kwenye yale maeneo.

Mhe. Mwenyekiti, shamba linajengwa na wapo watu wa aina mbali mbali wanajenga na shamba linamalizika na malengo ya serikali hayafanikiwi, lakini tukija hapa tunasema kwamba serikali inajitahidi na ina mipango mizuri, hivi ni mipango gani Mhe. Mwenyekiti, wakati maeneo tuliyoyaweka yanachukuliwa? Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri anieleze ni hekta ngapi zimechukuliwa Tunguu na pia anitajie nani na nani waliochuku na wizara imechukua kuwaondosha katika eneo lile, vyenginevyo sitakubaliana na wizara hii katika kupitisha bajeti yao. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, najaribu kwenda haraka kwa sababu muda ni mdogo na wala sitaki kupoteza muda wako. Vile vile naomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja anisaidie. Kwa kweli serikali yetu inakuwa na mipango mizuri sana lakini mipango mingi inakuwa inakatika njiani na ile dhamira ya serikali inakuwa haifikiwi na tunakuwa tunapata tabu sababu gani na nini kinachosababisha suala hilo.

Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe. Lengo la mradi ule ilikuwa ukipewa ng'ombe akizaa, basi yule mtoto apewe mwenzako lakini ule mradi haujulikani hatma yake imeendea wapi. Waliopewa ng'ombe sijui kama ile dhamiri waliyokusudiwa kama wameitekeleza. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hebu anisaidie ile dhamira ya kopa ng'ombe lipa ng'ombe imefikia hatua gani na maendeleo yake ya huu mradi na mafanikio na yale malengo ambayo yamekusudiwa Mhe. Mwenyekiti, yapo katika hali gani.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nataka nizungumzie katika suala zima la *MACEMP* ndugu zetu wafadhili mara nyingi tunasema wanakuwa na dhamira nzuri. Wanajaribu kutusaidia katika miradi mbali mbali lakini miradi mingi ambayo tumekuwa tukisaidiwa imeonekana inakuwa na mashaka katika umalizikiaji wake. Hii inatupa wasi wasi kwamba itafika pahala wale ambao wanatusaidia basi wataacha mkono kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa *MACEMP* ulikuwa na mambo mengi. Moja ya jambo ambalo wamelifanya ni ujenzi wa soko la Tumbe. Soko lile nimefika Mhe. Mwakilishi, hapa atakuwa ni shahidi, tulikuwa wote katika kuliangalia soko lile, katika ziara zangu za kawaida tu, wakati nilipokwenda katika maeneo mengine nikakutana naye nikamuomba Mhe. Mwakilishi tuende angalau nikalione lile soko. Lakini Mhe. Mwenyekiti, soko linasikitisha, kwanza hatujui ni sababu gani inayosababisha mpaka leo kwa muda mrefu soko lile halijafunguliwa.

La pili ubora wa soko lile haupo, soko halijafunguliwa lakini soko limeshaanza kubomoka. Baada ya kuwa tufungue tunaanza kufanya matengenezo kabla ya kuingia na kuanza kazi. Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba Kamati ya *PAC* ifanye kazi, ikaliangalie soko lile ubora wake na ijiridhishe *value for money* kama pale imeweza kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni masikitiko nasema kwamba tusipokuwa waangalifu basi ile tegemezi ya ndugu zetu wahisani kutusaidia inaweza ikakatika njiani na hatimaye ile dhamira na yale malengo ya kuwasaidia wananchi wetu yakawa hayafanikiwi.

Mhe. Mwenyekiti, soko linasikitisha sana, bado katika soko lile kuna malalamiko ya watu ambao wanamdai mkandarasi *engineer* ambaye amefanya kazi katika eneo lile. Hapa nina kopi ya watu wanaodai, kuna watu karibuni tisa wanadai shilingi milioni kumi na mbili laki tano tisini na moja elfu. Mhe. Waziri atakapokuja hapa basi anisaidie kama wizara imejitahidi vipi kuwasaidia wananchi wa Tumbe katika kulipwa madeni yao ambayo imekuwa wakisumbuliwa kwa muda mrefu kutokulipwa. Kama tunavyoelewa wananchi wetu wanafanya kazi kwa malengo ya kujisaidia katika maisha yao. Basi Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze jitihada zilizotumika katika kuwaondoshea kadhia ya madeni wananchi hawa wa Tumbe. Lakini pia aje anihakikishie ni lini soko la Tumbe litafunguliwa. Pia anielezee ni jinsi gani ameliangalia katika ubora wa soko hili.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kabisa kwa kutoa pongezi. Watu wanasema kwamba muungwana anapotendewa wema basi ni lazima atoe shukurani. Mara nyingi Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukipiga kelele juu ya masuala ya utendaji na uaminifu katika taasisi mbali mbali. Tunakuwa tunatoa manung'uniko kwa namna baadhi ya watendaji kutokuwa waaminifu na wanapofika pahala kuharibu miradi hata kuharibu mali za serikali za nchi hii. Kwa upande wa Wizara hii ya Mifugo pamoja na kutaka kwamba nisaidiwe na kupata majibu halisi ndipo nipitishe bajeti hii, lakini katika kitengo cha bahari Kuu Mhe. Mwenyekiti, napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mkurugenzi wa Bahari Kuu ndugu yetu, kijana wetu Zahor Al-Kharous kwa

namna anavyosimamia na namna alivyokuwa muadilifu katika utendaji wake wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nililalamikia hapa juu ya ubadhirifu wa Idara hii wa shilingi 1.7 bilion lakini nampongeza sana kijana huyu Mkurugenzi wetu namna alivyoweza kufuatilia na kusimamia na kugundua ubadhirifu ule na kuhakikisha kwamba sheria inafuata mkondo wake na wale wote waliohusika kuwafikisha katika vyombo vya sheria pamoja na kushirikiana na serikali. Mwenyezi Mungu Inshallah amjaalie ampe nguvu na moyo wa imani na ampe nguvu katika kusimamia majukumu yake ya kila siku na iwe somo kwa wengine katika kusimamia maidara yao na maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nasema nashukuru kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kwahani nasema nitaunga mkono hoja ya wizara hii mpaka nitakapoelezewa kwa kina suala zima la eneo la mifugo la Tunguu lilichukuliwa na watu waliokuwa hawaitakii mema nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote kwanza nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma ambaye ametuwezesha kwa mara nyengine kuwepo katika Baraza lako hili tukufu kwa mintarafu ya kuchambua mambo mbali mbali ambayo yataleta tija kwa wananchi wetu. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii niwapongeze sana Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara hii kwa kushirikiana kwa pamoja ili kuleta ufanisi mzuri zaidi katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo mimi naiita wizara mpya, ni wizara ambayo kwa kweli ni mpya na inatarajia kufanya kazi zake kwa uaminifu na uadilifu. Lakini pia niiombe serikali kwa sababu hii Wizara mimi naiita wizara mpya, huko nyuma ilikuwa imechanganyishwa na Wizara ya Kilimo. Kwa hivyo niombe sana serikali katika wizara moja ambayo nayo tuna matumaini makubwa ya kuleta maendeleo katika nchi yetu ni Wizara hii ambayo wizara ina mambo mengi. Wizara hii ina mifugo na mambo ambayo ya kuweza kuwashajihisha wananchi kujikwamua katika hali ya umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, wakati tulipokuwa kwenye Kamati nilikuwa kidogo mkali kwa wizara hii na leo niseme tu kwamba hii wizara tulikuwa tunapata misaada kutoka mashirika mbali mbali. Nianze na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi. Kama mwenzangu ambaye amemaliza sasa hivi Mhe. Ali Salum ameelezea tulikuwa na misaada mingi tunapata kutoka *MACEMP,* lakini sasa hivi kwa kweli nimesikitishwa kwamba idara hii imetiliwa pesa kidogo sana, milioni mia moja. Maana sasa najiuliza pesa hizi zifanye nini? Milioni mia moja hizi zitafute mafuta ya doria, milioni mia moja hizi ziwape wananchi

kuwasaidia kutokana na yale maelekezo ambayo tulikuwa tunasaidiwa na *MACEMP*.

MACEMP ilikuwa inasaidia sana lakini kwa kweli kama hatukufanya serikali tukahakikisha idara hii tunaipa nguvu zote basi itakuwa sisi si waungwana hata kidogo. Itakuwa tumepoteza mambo mengi sana ambayo wananchi wetu walipatiwa na *MACEMP* ili kuhakikisha kwamba wanajikwamua katika hali ya umaskini. Niiombe sana serikali na hili tukubaliane na Wizara ya Fedha, tulikutana na wenyewe Wizara ya Fedha, kwa hivyo niwaombe kwamba lile suala tulilokubaliana niwaombe sana kwamba watenge pesa ambazo zitaweza kusaidia kwa sababu doria tu ni milioni 28 kwa mara moja. Sasa katika milioni 100 jamani mfanye doria au itoe nini hii milioni 100. Mimi najiuliza. Kwa hivyo naomba sana kama kweli tumeunda Wizara hii peke yake basi tuhakikishe hii Wizara tunaisaidia. La si hivyo tuburuzane basi mambo yeshe, kila ikifika mwaka sisi tuseme tunataka hili, halipatikani basi twende tu lakini kwa kweli hii ni Wizara muhimu Mhe. Mwenyekiti.

Mimi nasema haya nasema kwa nia safi, hii ni wizara katika wizara muhimu na hii ni moja ya wizara muhimu sana hii ambayo ndiyo inayoleta tija katika taifa letu hili. Ukiona kuku, hayo makuku yanayoambiwa yanaagizwa huko paja moja kuliko la ng'ombe sijui yanaladha gani. Mimi nitoe wito bwana wizara na niiombe serikali makuku hayo hatuyataki. Tumetoa mipango ya serikali yetu kwamba wananchi wetu wafuge kuku, wafuge ng'ombe, mbuzi ili wajinasue, leo wananchi wetu sasa hivi wananung'unika sisi ndio tunaonung'unikiwa Mhe. Mwenyekiti, lazima tuseme ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wananung'unika kwamba wanapewa mikopo kwa kufuga kuku lakini kuku watu hawawaoni wanakwenda kuchukua kwa maboksi mikuku hiyo nyama hata haijulikani, midude inayoletwa hapa hatuijui mwanzo wala mwisho. Mimi nasema ni midude tu ile sijui inalishwa nini. Natoa wito kwa wananchi wetu msivunjike moyo ndio tunasema hivi, serikali ione, sisi ndio tunashajihisha watu kwamba watu hawa watafute mifugo wajiendeleze. Leo mtu ana mikuku, mimi nitaisema sana hii mikuku. Tuwape moyo wananchi wetu na wananchi wetu wamekopa pesa nyingi kwa ajili ya kujiendeleza, lakini leo imetuingilia midude hiyo hatuijui mwanzo wala mwisho.

Naiomba sana serikali kile kinachowezekana katika nchi yetu basi kiachiwe kiwezekane, kile kilichokuwa hakiwezekani ndio tunakiagizishia huko, tuna madude tele tunaagizishia yanakuja hapa jamani. Lakini hata kuku jamani tuagizishie nje tena mikuku ya Brazil, paja moja kama mguu wa mbuzi, midudu hiyo si kuku, hilo moja.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nije katika maeneo ya wizara hii. Kama tunavyoelewa kwamba hii Wizara ilikuwa imechanganyishwa na Wizara ya Kilimo. Katika Wizara ambayo ilikuwa na maeneo ni Wizara ya Kilimo, lakini sasa hivi kwa sababu zimegawanywa Wizara ya Uvuvi na Kilimo mbali lakini na wizara hii ina maeneo mengi. Niiombe serikali maana kuna watu humu wanatumia jina la Rais. Rais msimtumilie kama Rais kasema sio tena mtu aseme Rais kasema na saa nyengine Rais hajasema. Tusichukue mambo yetu binafsi tukamtia Rais Mhe. Mwenyekiti, ili watu waogope. Sisi tunachokitaka ni ukweli tusimsingizie Rais tukamkumbizia Rais, aah! maana yake hapa Rais kasema pasichukuliwe, pafanywe hivi, apewe huyu apewe huyu. Hatutaki hayo msimsingizie Rais jamani.

Maana sisi midomo yetu ndio kama hivi tunasema Rais unasingiziwa baadhi ya sehemu kwamba wewe umedhibiti na umesema apewe fulani na fulani na fulani. Si kweli mimi namkatalia Rais si kweli kwa sababu Rais ni kiongozi wa nchi ambaye anataka wananchi wake wote wawe katika hali ya usawa na maeneo na kila kitu. Tusimuingize Rais kumgombanisha na wananchi wake, naomba sana kwa sababu ni muadilifu. Katika Rais muadilifu mmoja ni huyu, haki ya Mungu nasema kwa udhati kabisa. Rais wetu ni muadilifu kweli kweli, tusimtie dosari kwa mambo yetu binafsi tukamtia dosari yeye. Naomba sana *to take care* na baadhi ya mazungumzo yetu, ikija kamati ukasema kasema Rais hapa pasitolewe pana hivi, pana hivi. Maana sisi midomo yetu ndio kama hivi tunasema tu. Kwa hivyo tusimsingizie Rais kwa mambo yetu binafsi, tusimsingizie Rais wetu ni muadilifu wa hali ya juu. Kwa hivyo haya tuachane nayo tuzungumze yetu sisi kama umetoa wewe Waziri sema nimetoa mimi nimekosea basi nawarudishia wenyewe wananchi. Hilo jengine maana nimesema leo kidogo nizungumze na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala jengine kuhusu mabwawa ya samaki. Naomba sana wizara ifanye tena tathmini kubwa kuhusu haya mabwawa ya samaki. Mengine yamefanikiwa lakini hii yote ni wananchi kutaka walipoambiwa kwamba ufugaji wa samaki upo hivi, wanataka kujitafutia fedha na kujinasua katika hali ya umaskini, walivamia wananchi wetu katika sehemu mbali mbali bila ya kufuata masharti na kupata taaluma ya mambo hayo. Sasa naiomba wizara hii ifanye tathmini upya, ipitie mabwawa yote, yale ambayo yamefanikiwa kufuata taratibu za kufuga samaki basi wapewe taaluma nyengine zaidi na wale ambao hawakufuata taratibu wapewe taratibu nzuri na wapewe taaluma ambayo itaweza kuwasaidia katika shughuli zao hizi za mabwawa ya samaki.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwa mwenyekiti niliitaka wizara hii ilinileteе nyumba zote ambazo zilikuwa zinamilikiwa na wizara hii. Nikaletewa, tukatoa miongozo. Sasa leo nataka Mhe. Waziri aje anambie

miongozo ile imefikia wapi. Si hivyo mimi leo hapa tutacheza msewe humu. Kwa nini nikasema haya. Tuna matatizo katika mawizara yetu lazima tuseme ukweli. Nyumba za kila wizara kwa sababu tunatoa fedha nyingi kwa maafisa wetu kuwapa pesa za kukodi nyumba wakati kila wizara huko nyuma ilikuwa na nyumba zake na mpaka hii leo imani yangu kwamba kila Wizara ina nyumba zake. Lakini tumeziachia nyengine zimeshachukuliwa watu wameshajibinafsishia bila ya utaratibu wowote, wengine wamezifanya ndio zao, nyengine zimeachwa zimebomoka na kuharibika.

Sasa nataka Mhe. Waziri anambie ni nyumba ngapi ambazo amezipata na nyumba ngapi ambazo hakuzipata na ni sababu zipi. Sasa hivi tunahangaika hapa kujenga maofisi na tulikuwa tuna maofisi, lakini tatizo letu tukishakurithi kitu matengenezo hatuna. Tunaacha mpaka jumba linataka kutuangukia mle ndani. Ndiyo yale aliyoyasema Mhe. Ismail Jussa juzi au jana kwamba usipoziba ufa, utajenga ukuta.

Mimi naomba serikali ifanye tathmini kila wizara nyumba walizonazo, zinazotengenezeka zitengenezwe, zilizokuwa hazitengenezeki basi tutafute mbinu namna ya kuzifanya ili tujenge upya. Lakini tunafanya baadhi ya mambo kwa makusudi ili kwa matakwa ya mtu binafsi, hili ndio tatizo letu. Mtu akishakupita jicho pahala akishapaona hapa pazuri basi atafanya kila njia ahakikishe pahala pale panafanywa mavarange ili pawe pake.

Jamani tusende namna kama hii, *wallahi* tutakufa kila kitu tutakiacha hapa hapa, tutakufa sisi, majumba ya maghorofa tunayojenga, magari, kumi, ishirini, na nini, *wallahi* tutayawacha hapa hapa, tukifanya mambo tufanye '*aste asteeeh'*. Naomba baada ya kusema hayo namuomba Mhe. Waziri aje anieleze kuhusu habari za nyumba. Najua yupo na Naibu pale wananong'ona wanasema kwamba mama Asha hawezi, kwa sababu hii ni Wizara yake. Lakini safari hii kama sikufanya ukali kwa kweli mambo hayendi. Hii yote ni kutaka kukusaidieni nyinyi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze tena sana wizara hii na sio kusudio langu, lakini haya yote ni kwa ajili ya kujenga ili wizara hii iende sambamba na yale mambo ambayo tumekubaliana katika Kamati pamoja na kuisaidia serikali yetu. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana asubuhi hii ya leo kunipa fursa na mimi kuchangia hotuba ya bajeti ya rafiki yangu Mhe. Abdillahi Jihadi Hassan. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni muhimu sana hasa katika nchi yetu kwa sababu nchi yetu ya Zanzibar ni kisiwa.

Wizara hii ina mambo muhimu yaliyokuwemo katika nchi yetu, kwa sababu ina uvuvi, ina na mifugo. Uvuvi hasa kwa Zanzibar ni muhimu kweli kweli na mifugo wananchi wetu walio wengi ni wafugaji. Kwa hivyo wizara hii ni wizara muhimu sana kwa nchi yetu lakini nasikitika kidogo kwamba serikali bado haijaona kwamba hii wizara kama ina umuhimu na bado hawajaiwezesha hii wizara ikatoa ajira kwa wananchi wa Zanzibar. Hii wizara inaweza ikatoa ajira nyingi kwa wananchi wa Zanzibar, kama inafanyiwa kazi kikamilifu. Mimi nasikitika sana kama bado serikali haijafumbua macho hasa kuona kama hii wizara ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti iliyopita nilizungumza sana hapa kuhusu suala la mifugo, nilisema kwamba serikali saa nyengine inapoteza fedha nyingi lakini fedha zile zinazopotea kwa ajili ya utekelezaji wa serikali kuwa bado haijajipanga vizuri, inatekeleza lakini haijajipanga vizuri. Nilizungumza hapa kwamba kama mfugaji unakwenda kumpa mbuzi mmoja tena dume kwetu sisi tunawaita mabeberu, unampa afute atazalisha nini? Unampa beberu bila ya kumpa mbuzi jike atazalisha nini. Nilisema sana mimi hapa mkaniona kama nafanya masihara, sasa kuna watu wengi walipewa mabeberu, beberu mmoja, wengine walipewa mbuzi wake mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nauliza serikali kama inakusudia kweli kuwaboresha wafugaji unakwenda kumpa mtu mbuzi mmoja au kuku mmoja atazalisha nini? Sasa namuomba Waziri kwanza akija anieleze katika fedha zile zilizotolewa kwa kutolewa mbuzi mmoja moja wakapewa wafugaji na kuku zilitumika shilingi ngapi na halafu atwambie kwamba je, ni vikundi vingapi vimezalisha katika yule mbuzi mmoja mmoja na faida gani tuliyoipata katika zile fedha zilizotolewa. Namuomba Mhe. Waziri akija anisaidie hilo.

Suala jengine kwenye mifugo nataka nizungumze kwenye kitengo hichi cha huduma ya uratibu wa mifugo. Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichopita katika bajeti zilitengwa fedha kwa ajili ya hawa wataalamu kupata mafunzo ili waongeze utaalamu wao. Bahati nzuri serikali imesifu kwamba katika kitengo hichi kimetoa fedha nyingi, kwa hivyo kazi yao imekuwa ni nzuri. Sasa naomba Mhe. Waziri anieleze kwamba zile fedha zilizotengwa na wakati hayo mafunzo hayakutumika maana wamekwenda wale wataalamu na kupata hayo mafunzo. Sasa anieleze ni sababu zipi zilizobidi kwamba fedha zimeshatolewa na wataalamu hawa hawakupelekwa kwenda kusoma au kwenda kupata hayo mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, anieleze kama basi hawakwenda je, amejipanga vipi kwa kipindi hiki wataalamu wale kuwaongeza utaalamu wao ili kufanya kazi vizuri zaidi. Suala jengine nataka nilizungumze kwenye mifugo kwamba wamejitahidi serikali kujenga vituo vya wataalamu wa mifugo lakini katika

vituo vile vilivyojengwa vimejengwa vituo tu lakini hawakuwekewa kitu chochote kwenye vituo vile, hakuna fanicha za aina yoyote, wala hakuna vitendea kazi vya aina yoyote ile. Sasa wanatumia utaalamu wao lakini sasa ikibidi wana dawa au wana zana zao zinawekwa kwenye saruji. Kwa nini iwe hivyo?

Mfano mimi wa kituo changu kilichokuwepo Micheweni, kipo kituo kimejengwa ni kizuri lakini vifaa vyote vinawekwa chini, hawana vitendea kazi vya aina yoyote, hakuna makabati, hakuna chohote kile, akiwa ana zana zake zinawekwa chini, zinapotea potea. Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja pia anieleze ni lini vituo vile wataviboresha kwa kuviwekea zana ili vionekane. Halafu hakuna hata mabango ya kuonesha kama hapa kuna kituo fulani. Ni lini atafanya kazi hiyo ya kuwaboreshea vile vituo na halafu viwekwe mabango hasa watu wakipita wajue kwamba hapa kuna kituo fulani, kuliko hivi vilivyo, mtu akipita hajui kama kuna chochote, kama hapa kuna kitu fulani. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hili alishughulikie.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nitoke kwenye mifugo nende kwenye uvuvi. Nimesema kwamba serikali bado haijawa tayari, sekta hii ya Idara ya Uvuvi na Mifugo kuiboresha. Mimi kila siku huwa nasema tunakuwa wataalamu wazuri wa kupanga kwenye makaratasi lakini utekelezaji wetu unakuwa ni mzito. Mheshimiwa kila mara tunazungumza suala la uvuvi wa bahari kuu kama tuna samaki baharini wanaoweza kutoa ajira kwa wananchi uvuvi unaweza ukatoa ajira kwa wananchi wetu walio wengi leo tukija hapa tunasikitika watu hawana kazi. Vijana wapo wengi hawana kazi na wakati bahari ipo visiwa vya wenzetu wanaendeshwa na bahari tu. Lakini leo bahari ipo mazao yapo baharini tunayatizama tu hivi hatuna vya kuyafanyia kazi. Tulizungumza hapa kama jamani eeh! serikali ijitahidi kutafuta wahisani halafu sadaka huanza nyumbani kila siku mimi nasema sadaka huanza nyumbani, serikali ifanye maarifa ipate japo boti ambayo itakuwa ni mfano halafu wawekezaji wengine wafuate lakini sisi tunasema tu utekelezaji haupo.

Leo serikali inatenga Wizara hii, uvuvi kwa kutumia uvuvi wa bahari kuu inatengewa shilingi milioni mia moja, zifanye nini milioni mia moja, hizi milioni mia moja zinaweza zikatumika kweli. Leo ndugu zetu wote tumewaweka kitako tuliwaambia kama uvuvi wote wanaovua ni uvuvi haramu watu wamekubali wametulia hawatumii uvuvi haramu. Lakini watu ukiwakosesha hiki wape mbadala. Sasa mbadala gani tumewapa wetu leo tunawazuia watu kuvua uvuvi huu tunawaambia ni haramu lakini uvuvi halali hatuwapi, tuwapeni zana za kufanyia kazi. Bahari ipo, samaki wapo, zana za kufanyia kazi hazipo. Sasa Mhe. Waziri twambie hasa ni lini mtakusudia kuvua uvuvi wa bahari kuu, kwa sababu wanakuja watu na meli samaki wakiibiwa tu sisi tupo tunatizama tu jamani, sisi tutafika mpaka lini, kila kitu

tunasubiri tu, jamani chelewa chelewa utapata mtoto si wako, kila siku tutachelewa mpaka lini kila kitu tunachelewa tu, kila kitu bado tu hivi lini tunakuja kutekeleza hasa?

Mhe. Mwenyekiti, kwa kusema ukweli wavuvi wetu hatuwatendei haki, serikali bado haijataka kuvuliwa uvuvi wa bahari kuu. Watu tumewazuia, kama uvuvi haramu watulie wamekubali lakini kama wamekubali ni lini hasa tutavua huo uvuvi wa bahari kuu wananchi wa Zanzibar wapate ajira kazi zipo, kazi zipo lakini sisi wenyewe tu hatujawa tayari. Mlitueleza kipindi kilichopita kama watu tumekwenda kuomba watajenga maboti hapa watafanya nini, wataleta meli lakini tunasema kwenye karatasi tu lakini utekelezaji wake haupo kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninalotaka nilizungumze ni suala la hawa wakulima wa mwani. Kwa kweli wananchi waliitikia kilimo cha mwani nguvu kwa zao zote lakini sasa hivi wamevunjika moyo laisal kiasi. Maana mwani umerundikana kwenye majumba mpaka watu hawana tena zile sehemu za kukaa, sehemu zote zishachukuliwa na mwani. Mwani haunununuliwi, watu wanayo mashamba wanao majumbani labda tufanye maarifa sasa watu wautafune huu mwani. Tulizungumza kama serikali ijitahidi kutafuta soko pamoja na kuwa Waziri wa Biashara alitwambia kama mwani umejaa duniani watu wengi wanalima mwani lakini bado tunasema serikali iwatafutie wananchi soko kwa sababu mwani mwingi na uko na hawana pa kuupeleka.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ufugaji wa samaki. Suala hili ni suala muhimu sana lakini na bado serikali haijawawezesha wafugaji wa samaki kwa sababu wamefuga samaki kwa ajili ya kuwa wapate wale samaki baadae wawe ni biashara iwasaidie, sio kwa ajili ya kitoweo na nilisema kipindi kilichopita kama wafugaji wetu wa samaki wote ni wakulima wa kitoweo tu kwa sababu mimi sijapata kuona hata siku kama leo gari hii ina samaki, ni watu wanaofuga samaki sehemu fulani, kwa hivyo ni sawa sawa na kuwa wanavua kwenye ndoo moja wanauza ni kitoweo tu si biashara. Kwa hivyo bado ninaiomba serikali iwape elimu wafugaji wa samaki na iwape nyenzo za kufanyia kazi ili iweze kuzalisha zaidi na hii inaweza ikasaidia kutoa ajira kwa wananchi wetu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, naomba suala hili waziri aone na aitake serikali kuwasaidia wawezeshwe zaidi hawa wafugaji wa samaki.

Suala jengine tulilizungumza kipindi kilichopita pia hawa wazalishaji wa chumvi, bado Zanzibar tunaweza tukazalisha chumvi nyingi zaidi na ikiwa kuna soko watu wakitafutiwa soko basi ikatoa fedha zaidi za kigeni Zanzibar kwa ajili ya chumvi inayozalishwa Zanzibar. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri na hili kwanza awe na utaratibu wa kuwatembelea hawa wakulima wa

chumvi na aone maendeleo yao, na la pili ajue kwamba hii chumvi inapata hii madini joto kwa sababu isije kuwa ni chumvi inazalishwa halafu ikawa inawadhuru wananchi wetu wa Zanzibar. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba sana na hili uliangalie sana.

Jengine ninalotaka nilizungumze ni soko liliopo Malindi. Mhe. Mwenyekiti, lile soko kama tunavyozungumza wananchi wengi wa Zanzibar wapo pale wanafanya kazi pale na wanapata ajira alhamdulillahi lakini kwa kweli soko haliridhishi ni chafu, ni chafu kupita maelezo, yaani kama utakwenda kwa kweli ukawaona pale samaki wanapouzwa jinsi palivyo pachafu mara unaweza usimtake kumla. Ninakuomba sana Mhe. Waziri tumia jitihada zako zote lakini pale pahali paboreshwe, uchafu uliopo, matope, uchafu kinyaa hapafai kabisa. Kwa hivyo pale pahala panatoa ajira nyingi kwa wananchi wetu ninakuomba serikali itumie jitihada yake yote lakini ipaboreshe, pawekwe japo sehemu za juu juu, saruji kidogo pale wanapopita wananchi au kama si saruji japo kifusi kiwekwe pale lakini alimradi yale matope na ule uchafu uliopo upungue kidogo. Mhe. Mwenyekiti, ni pachafu mno nakuomba sana paboreshwe pale pahali.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba Mhe. Waziri anipe majibu yangu niliyomuuliza, akishanipa majibu yangu mazuri mimi ni rafiki yangu sina tatizo la kumzuilia bajeti yake nitamuunga mkono lakini kwanza sijibu moja kwa moja kama ninamuunga mkono, mpaka kwanza nipate majibu ya maswali yangu niliyomuuliza. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Subeit Khamis, Waheshimiwa ninakuombeni wakati mchangiaji anachangia naomba sana kuwe na utulivu kwa sababu sauti zenu zikiwa nyingi inaingiliana na mawasiliano na tunajua kwamba tuko *live*. Kwa hivyo ninakuombeni sana mpunguze mazungumzo wakati mjumbe anachangia.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya inaniruhusu. Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Naibu Waziri wake na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa kweli watu hawa niliowataja wanakwenda vizuri sana. Wanakwenda vizuri pamoja na wavuvi na ni jambo zuri ili kupata mafanikio kuwa wanakwenda sambamba na hao wavuvi.

Ninashukuru Mwenyezi Mungu ndani ya mwaka huu hakuna bughudha lolote lilitokea kwa wavuvi hata siku moja, nasema ni hatua kubwa ya kufikia maendeleo na haya ni kutokana na mashirikiano makubwa wanayofanya

Waziri wetu, Naibu Waziri pamoja na mtendaji mkuu Mkurugenzi wa Uvuvi Mussa Aboud Jumbe wanafanya vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 5 ambao ni sekta ya uvuvi. Naomba uniruhusu ninukuu:-

> 'Mhe. Mwenyekiti, sekta ya uvuvi imezidi kuimarika kutokana na kuongezeka kwa wavuvi wa baharini pia wananchi wengi wameanza kufuga samaki na mazao mengine ya baharini'.

Hapa nimesikia kama uvuvi umeimarika kutokana na kuongezeka wavuvi wengi baharini lakini tujiulize kuongezeka kwa wavuvi baharini mafanikio au vipi. Mhe. Waziri ninakuomba sana utapokuja hapa utueleze kuongezeka kwa wavuvi baharini ni faida au ni hasara, utapokakuja unieleze vizuri ili tujue lipi lililo sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia katika ukurasa huu wa 5 amezungumzia kuongezeka kwa sindikizo la uvuvi katika maeneo ya hifadhi kutokana kuongezeka kwa idadi ya wavuvi, ndio maana nikaulizia kule kuongezeka kwa wavuvi kuna faida au kuna hasara? Lakini hapa katika mambo ya hifadhi nimeona wenyewe walioko katika hifadhi ni wenyewe waliokubaliana walioweka hifadhi hawa, kuna siku zao wanakubaliana kwenda kuvua katika maeneo ya hifadhi kwa utaratibu waliojiwekea. Mimi sioni mtu mwengine yeyote kwenda kuvua katika eneo la hifadhi na kama yupo Mhe. Waziri akija hapa atuambie lakini wasisingizie watu wengine waliokuwa hawendi. Lakini namna wanavyokaa katika eneo la hifadhi wana siku yao ya kwenda kuvuna katika yale maeneo ya hifadhi kwa utaratibu wao waliojiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nizungumzie tu kidogo kwamba bado sheria nambari 7 ya mwaka 2010 ina matatizo kwa wavuvi haitekelezeki, bado ni changamoto kubwa ya kwamba haitekelezeki na sheria ili iwe nzuri iwe inatekelezeka. Lakini sheria hii imekwenda sana kuwabana wavuvi na sio kuwapa fursa kufanya kazi zao. Mhe. Waziri wa Uvuvi na Mifugo atakuwa shahidi tarehe 3/7/2012 katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi kongwe Jumuiya ya Wavuvi wa Kojani walifanya mkutano ulioshirikisha mikoa mitatu ya Unguja kwa kilio chao hichi na walimualika Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa bahati mbaya Mhe. Balozi Seif Ali Iddi hakufika na akamuakilisha Waziri wa Uvuvi na tunashukuru alifika na ndiye aliyetwambia kama Mheshimiwa hatowahi kufika na ninamwakilisha mimi.

Lakini ilisomwa risala juu ya kilio cha wavuvi katika mkutano huo, hebu tumuulize waziri alifikia wapi, hakuna jibu lolote. Na alitueleza kama nimechukua ninarikodi na nitampelekea Mhe. Makamu wa Pili wa Rais

hatukuona chochote kilichotendeka. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri atapokakuja hapa anieleze au hapa leo patazuka kivumbi.

Mhe. Mwenyekiti, sheria ni nzito kutekelezeka kwake leo umemuweka mtu katika Ofisi unamnyang'anya kalamu, unamnyang'anya *computer,* hivyo unakusudia huyo afanye kazi au unakusudia vipi. Sasa leo mvuvi unamwambia asitumie kioo ambacho kioo kinamsaidia kwa kuona ndani ya bahari lakini unamwambia asifanye hivyo, mvuvi kutumia chupa ya *gas oxygen* kwa kupata hewa unamwambia asifanye unakusudia kumfanya nini? Hebu Mhe. Mwenyekiti, tuambieni tatizo ni nini? Nakumbuka mwaka jana katika kitabu cha Makamu wa Pili wa Rais ilizungumzia kuwaboresha wavuvi wadogo wadogo kwa sababu kuelekea uvuvi wa bahari kuu, lakini uvuvi wa bahari kuu ni mipango ya muda mrefu hata kufikia huko uvuvi wa bahari na ninaamini samaki tunao wengi sana katika bahari yetu na bado hatujapata zana za kwenda kuvulia.

Lakini sasa uvuvi huu tulionao lazima tuuboreshe tusiweke vikwazo vya kuweza kuwazuia wavuvi, Zanzibar hii mimi nasema hilo haliwezekani kwa sababu ni nchi ya visiwa na ina wavuvi wengi. Ukiangalia mvuvi mmoja tu anawasaidia watu kumi mgongoni kwake. Angalia mvuvi anaporudi baharini wachuuzi, akina mama ntilie na wengi wengineo wanafuata wote ni ajira kutoka kwa wavuvu. Hii ni sekta inayoajiri watu wengi sekta binafsi ya uvuvi hiyo tutaiboresha tutaweza kuwasaidia wananchi wetu, lakini leo tunatunga sheria ya kuwabana wasipite popote. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, sheria hii sio msahafu tunarekebisha sheria nyingi ndani ya Baraza la Wawakilishi hili, kufanya marekebisho ili kwenda sambasamba tukafanya kwa utulivu na amani kuna tatizo gani hebu Mheshimiwa tueleze, ni tatizo lipi la msingi linalotukwaza. Ni vyema kukawa na wavuvi, Mwenyezi Mungu Wakojani katupa kipaji cha uvuvi na hata hilo jarife unalosema kama ndio haki ya kuvulia ukitaka haramu linakuwa, alimradi ni mipango mizuri tu na tunaoneshwa katika *screen* hilo jarife liko katika matumbawe tushawahi kuona picha hizo.

Sasa hapa ni kushirikiana kwa kufanya mipango mizuri. Hivi kama mimi Mhe. Hassan, Mhe. Haji Omar Kheri wa Tumbatu utamueleza nini, hawa ni wamoja ni wavuvi na kama ni elimu tupate kwanza sisi tukaelimishe wenzetu huko tuwe walimu wakubwa wa kuelimisha wavuvi wetu. Tukiwatenga wavuvi hatutopata mafanikio hata siku moja, unapofanya jambo mshirikishe yule mwenye kitu, lakini ukifanya kwenda kukaa ofisini mkafanya nyinyi, mumefanya semina muwashirikishe watu waliokuwa si wavuvi haisaidii, hebu tuwaiteni wadau na wote ni wavuvi tutapata mafanikio makubwa sana, hii sheria iliyotungwa wao hawaijui. Sheria hii imetungwa kwa lugha ya Kiingereza hakuna hata mvuvi mmoja anayeifahamu huko ofisini tu ndiko

inakojulikana, kwa nini isifanyiwe marekebisho. Leo wavuvi wanajua kuvua na kwenda baharini na kurudi tu hawajui chengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea Idara ya Mipango na Sera katika ukurasa wa 9 huu. Mimi nizungumzie tu katika kifungu (d) kinasema kuzifanyia mapitio sheria ya mifugo na sera ya uvuvi na mazao ya baharini. Sasa tujiulize sheria ya mifugo ni nani anayelalamika, hakuna mtu anayelalamika, hakuna mtu anayelalamika inayolalamikiwa ni hii sheria ya uvuvi lakini mifugo hakuna malalamiko yoyote. Hebu twendeni kwenye sheria ya uvuvi tuangalie tutafanya nini, tutawasaidia wananchi wetu. Halafu anaendelea katika (e), anasema kuendeleza mashirikiano na taasisi za serikali na zisizo za kiserikali za ndani, kanda na kimataifa hii ni nzuri. Hii ni nzuri lazima tuwapongeze kama hii ni nzuri ukiwashirikisha watu kama hao tunafikia muafaka lakini tukijaribu kuwatenga hawa hakuna kinachopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea katika Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ukurasa wa 25 imezungumzwa hapa, imesema kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ilipanga kutekeleza yafuatayo:

Moja, kuimarisha usimamizi wa raslimali za baharini na hii niseme tu kuimarisha usimamizi wa raslimali za baharini ni nzuri kwa nini mali zetu tusizisimamie vizuri, tukizisimamia hizi tutapata malengo mazuri ufanisi na utendaji mzuri wa kazi. Mimi ninawapongeza sana hawa.

Lakini vile vile inasema (b) kuimarisha shughuli za uvuvi wa kienyeji na bahari kuu hapa sasa. Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyozungumzwa nilivyoinukuu hapa kuimarisha shughuli za uvuvi wa kienyeji na bahari kuu, sasa mimi masikitiko yangu makubwa huu kuita uvuvi wa kienyeji, kwa nini tusiite uvuvi wa asili au uvuvi wa jadi. Hii ni kuwatafutia sababu kuwaangamiza wavuvi. Hapa daktari unapomwita daktari wa kienyeji basi utaona huyu hana kazi na ukitaka kumuua mbwa ukimwita mbwa kichaa umeshampatia sababu. Naomba kuwe na mabadiliko makubwa hapa, waitwe wavuvi asili au wa jadi sisi ni Wazanzibari ni watu wa visiwa, uvuvi ni asili yetu, hakuna sababu ya msingi watu kuita uvuvi wa kinyeji hii ni kutafuta sababu ya kuwaangamiza wavuvi na sio kuwajenga.

Halafu anazungumzia kuimarisha shughuli za utafiti na uwekaji wa matumbawe ya kienyeji na hii ni nzuri sana. Vile unavyowaona Wakojani wanawakamata samaki sana haya matumbawe wanayatengeneza wenyewe, ni magogo wanakwenda kuweka baharini pamoja na kutumia magari mabovu wanaweka kama matumbawe, wakenda pale samaki wanakuwa ni makaazi yao hii ni nzuri inasaidia sana kuwapata samaki.

Lakini vile vile (d) kuimarisha mazingira ya uendeshaji kazi na hii nawapongeza sana ni jambo zuri sana tena kwa kushirikianana wadau hawa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika Idara ya Mazao Baharini ukurasa 28, imezungumziwa kuendeleza katika mazao ya biashara ya baharini. Kama inavyozungumzwa hapa naomba ninukuu;-

> "Idara ya Mazao ya Baharini ina majukumu ya kuendeleza wafugaji wa samaki na mazao ya baharini, wakulima wa mwani pamoja na wadau wengine wanaojishughulisha na mazao ya baharini kwa ajili ya kuinua hali zao kiuchumi na kuinua pato la taifa".

Mhe. Mwenyekiti, katika mazao ya baharini sasa hivi watu wamejikita na upandaji wa mwani, ukienda katika maeneo yetu ya bahari sehemu nyingi imechukua eneo kubwa ni wapandaji wa mwani lakini jambo la kusikitisha mwani hauna thamani, kazi nzito, ngumu lakini kipato chake kidogo sana kinawaumiza. Kwa hivyo kama kuna jambo la kufanyiwa kazi ni hili lazima tupate masoko mazuri na wapandishiwe bei, kilo shilingi mia tatu au mia nne tunawaumiza.

Mhe. Mwenyekiti, tujifunze kutokana na tunakokwenda lakini vile vile kazungumza Mhe. Subeit hapa katika wafugaji wa samaki, Wizara imefanya kazi kubwa sana nadhani inafikia mara mbili kuwapeleka wananchi China kwenda kujifunza namna ya ufugaji wa samaki, lakini mimi kama mvuvi ninayejua uvuvi basi sijaona mafanikio katika ufugaji wa samaki wa kuweza kumkomboa mwananchi kuondoka katika umaskini bado kabisa. Mheshimiwa afuatilie sana asingeambiwa kama mna samaki elfu mbili humu kwenye ziwa hili akakubali, lazima aangalie sana tushirikishwe, unapotushirikisha utapata mengi, tutapata mengi kutoka kwako utapata mengi kutoka kwetu, tutafanya kazi kwa pamoja na mafanikio yapo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumzia uvuvi tunasema tunataka kuboresha uvuvi angalia Idara ya Uvuvi imewekewa shilingi milioni mia moja ifanye nini, iangalie hiyo doria yao tu ni kiasi gani kwa mwezi hata hiyo shilingi milioni mia moja kwa doria tu haitoshi. Mhe. Waziri wa Fedha upo na unatoka mwangalie huyu na umuongezee ili tupate ufanisi lakini shilingi milioni mia moja haitoshi haikidhi Idara hii itakufa. Idara imeelekea kufa moja kwa moja haiwezi kuwasaidia wavuvi hata siku moja. Mhe. Mwenyekiti, leo nasema kwa uchungu kabisa pamoja na mradi wa *MACEMP* uliopita, Wizara na Idara ilifanya kazi kubwa sana ya kuwasaidia watu kwa kuwapa boti lakini nataka tuangalie boti ziko wapi mpaka leo hii, hebu tuangalie ziko wapi boti zile, tusiwape watu kienyeji kienyeji tu. Majimbo ya Waheshimiwa Wawakilishi wanapokwenda kukabidhi kitu na wao

washirikishwe wajue na wafuatilie wasimamie, boti zote zile zimesimama zimeshauzwa kwa faida ya watu wachache. Zilitoka kwa kila vijiji, zilitoka boti zile na watwambie ziko wapi. Mimi pale Kojani ilitoka boti sijui hata ilipo walikabidhiwa watu wachache kwa kikundi fulani tu sio wavuvi na hivi sasa haipo, ufuatilie Mheshimiwa ukija hapa utwambie iko wapi kama kweli unafanya kazi zako vizuri. Nataka leo unieleze hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mengi tunayo lakini kuna wenzangu kila mtu ana mawazo tofauti lakini naamini nataka nimalizie kwa kusema hii ni barua unayoiona. Mhe. Said Ali Mbarouk Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo alipokuwa Waziri wa Uvuvi aliwahi kutembelea kisiwa cha Kojani mwaka 2012 na katika ziara hiyo na mimi alinishirikisha na Mhe. Farida alikuwemo na watu wa Idara waliwemo. Mheshimiwa katika mzunguko wake pale pale tukafanya majumuisho mafupi akatoa upendeleo ya wananchi wa Kojani wapatikane wananchi wawili wende wakasome Chuo cha Uvuvi Mbegani. Jambo la kusikitisha tulikuwa na waandishi wa habari tulikuwa na wafanya kazi katika Idara hii leo anatwambia katika barua hii katika majibu yao hawajapata kuona lakini hapa imetiwa nakala kwa huyu Mhe. Said Ali Mbarouk na mimi Hassan Hamad Omar nikiwa mtu wa jimbo nimetiwa nakla lakini nakala hiyo mimi sijaipata mpaka hii nimepata wananchi kwa malalamiko yao.

Sasa nizungumze Mheshimiwa watu katika migogoro yao ya kazi ofisini isichukuliwe wananchi wale kukosa kwenda kusoma naomba utakapokuja hapa unieleze kwa kina wananchi hawa utawasaidia vipi ile ahadi aliyoitoa Mheshimiwa kuweza kufanikisha mambo hayo tuijue iko wapi. Isije kuwa sababu ndani ya ofisi yao wakaleta matatizo kuwasimamisha hawa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha kabisa, kwa nini hawa wavuvi wa Kojani hawasaidiwi. Wakojani ni wavuvi na popote utakapokwenda wanatajikana hata ukiangalia kwenye *internet* utawaona. Mhe. Waziri uangalie misaada mingi inapotea tunayo jumuiya ya wavuvi na tukafanya hata mazungumzo na wavuvi wa Chwaka, Marumbi na wengine jumuiya hii inasaidia, jumuiya hii ina vitengo vingi, hata katika mambo ya uokozi wamo, kwa nini hatuwasaidii. Kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika basi muwe sambasamba muwasaidie wavuvi, tusipange nguvu zetu kwa kuwakamata wavuvi na kuwachomea nyavu zao moto bado hapo hujafanya kitu au uwe tayari kwenda kuwafunga jela wote kuhakikisha kwamba uvuvi Zanzibar hakuna, lakini kwa sababu hivi ni visiwa uvuvi hauwezi ukaondoka hata siku moja.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kumshukuru tena Waziri na Naibu Waziri na watendaji wake wote tunashirikiana vizuri kwa muda huu tunakwenda vizuri kabisa, hasa nimsifu sana Mkurugenzi anatupa mashirikiano makubwa

sana na ndivyo inavyotakiwa na tunamuomba Mkurugenzi tuzidi kushirikiana atapata mengi, atapata ufanisi wa kazi yake. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie hapa lakini sitounga mkono na wala sina haja kumpiga buti rafiki yangu atakaponipa maelezo mazuri lakini kama si hivyo bado ngoma nzito. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Muumba wangu Allah Subhanna Wataalla kwa kuniamsha mimi na wenzangu tuliomo humu pamoja na wewe Mhe. Mwenyekiti, tukiwa hai, wazima wa afya na tukaweza kuendelea na shughuli zetu hapa huku tukiwa tunaendelea na mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi pamoja na jina jipya ulilonipa leo nakushukuru, lakini naomba vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake hapa, nimpongeze yeye niwapongeze na watendaji wake ambao wamemsaidia kuandaa hotuba hii imepangika vizuri kama kawaida ya hotuba za Wizara hii huwa hazina kazi kubwa kuzifuatilia kutokana na mtiririko wake unavyowekwa na viambatisho vyake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu naomba nianze kwanza na hoja ambayo mara nyingi nimekuwa nikisema katika Baraza hili na leo inadhihirika kutokana na michango ya wajumbe ambao nimeisikia tangu asubuhi. Mara nyingi nimesema kwamba naamini kwamba wakati umefika wa Mhe. Rais, kuangalia tena muundo wa Serikali yake. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, zimeundwa wizara nyingi kwa kutegemea kwamba zitaongeza tija na ufanisi kwa kuyagawa majukumu kila mmoja kumpa yake, lakini tunakuta mwaka wa tatu tena sasa, tija katika zile wizara zilizogaiwa haionekani, lakini gharama za uendeshaji zimeongezeka zikiwa ni mzigo kwa walipa kodi wa Zanzibar. Sasa leo wanapotokea Waheshimiwa Wawakilishi wakalalamika kuhusu bajeti ndogo kwa mfano katika Idara ya Maendeleo ya Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, tusimalizie hapo hebu tuende zaidi kidogo. Mimi mtazamo wangu ni kwamba hii imetokana na muundo wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, ukitizama katika kiambatisho nambari 14 kipo ukurasa wa 57, inazungumzia makadirio ya matumizi kwa mwaka 2012/13 fedha za kazi za kawaida kuanzia Julai, 2012 hadi April, 2013. Mhe. Mwenyekiti, ukitizama utaona kwamba katika fedha za matumizi ya kawaida, fedha zilizopatikana Julai mpaka April, 2013 mishahara peke yake ni shs.1,888,546,684/= chini huko jumla kuu. Matumizi mengineyo sasa ni shs.601,485,751/= katika hali hiyo Mhe. Mwenyekiti, tutegemee nini. Fedha za matumizi mengineyo kwa maana ya *other charges* ni kama theluthi moja tu kama asilimia 33 ya fedha iliyotumika katika mishahara. Hii inakuja kwa sababu ukishaunda wizara mpya utakuwa na Wakurugenzi, Waziri, Naibu Waziri na watumishi wao

wanaowafanyia kazi, inaongeza gharama za utawala na uendeshaji, matokeo yake ndio haya. Fedha hii ingelikuwa bado Wizara moja kama ilivyokuwa zamani pengine ingeweza kuokolewa ikenda katika kuhudumia hizo shughuli za uvuvi ambazo zinazungumzwa leo na Wawakilishi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo bado mimi namshauri Rais wangu, nimemshauri mara nyingi kwamba wakati umefika atazame tizame tena muundo wa Serikali yake, huu ni mzigo mkubwa kwa walipa kodi maskini wanyonge wananchi wa nchi kubeba gharama hizi na matokeo yake huduma haziwafikii, pesa zinamalizikia kulipana mishahara na marupurupu na huduma za wakubwa tu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hilo tulitazame sana.

Mhe. Mwenyekiti, hata tukizama hilo Idara zenyewe zilivyogawika unakuta Wizara hii ukiona Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Idara ya Utumishi na Uendeshaji ina Idara nyengine nne ambazo pengine huko zamani zilivyokuwa katika Wizara moja zilikuwa pengine ni Idara mbili tu hizi ya mifugo ikashughulikia shughuli zote za mifugo na uvuvi. Lakini leo kuna Idara ya Maendeleo ya Uvuvi mbali, na Idara ya Mazao ya Baharini, sasa mazao ya baharini nini kama si samaki, ukinambia mwani hivyo kweli mwani imekuwa ni shughuli kubwa Zanzibar kiasi cha kuundiwa Idara yake, maana sijawahi kuona Idara ya Mikarafuu, mimi katika Wizara ya Kilimo. Sasa nauliza kwamba shughuli hizi zingeweza kabisa kufanywa ukapunguza gharama za utawala zikafanywa chini ya Idara moja na ukaokoa fedha za walipa kodi. Hilo moja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ninalotaka kulizungumzia kabla sijaingia katika maeneo yaliyokuwemo ndani ya mradi huu. Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Rais, katika Baraza hili hebu aitupie jicho la karibu Wizara hii. Zanzibar ni ndogo sana, tunayasikia yaliyoko Wizarani, wakubwa wenyewe kwa wenyewe wanagombana hawasikilizani huo ufanisi na tija itapatikana wapi, hakuna hata kuheshimu *authority*. Mkurugenzi anaweza kukiuka maagizo na maelekezo ya wakubwa wake akafanya anavyotaka, akiwemo Katibu Mkuu, Naibu Waziri, akiwemo Waziri, wasitufiche watuambie hawa, sasa ufanisi na tija itapatikana wapi. Hii tabia ya kutoka watu wakajifanya wao kama vile ni wafalme katika Idara zao wanamiliki na yako katika Wizara nyingi haya ndio yanayokwamisha utendaji, kwa sababu mtu anajifanya hawezi kuhojiwa, yeye anaweza kuamua lolote tu, sasa kila kitu katika utawala Mhe. Mwenyekiti, wewe mtu mzuri katika mambo ya utawala basi ule mtiririko na mpangilio wa dhamana una faida gani ikiwa mtu anafanya jambo analotaka yeye mwenyewe tu, una faida gani. Kwa hiyo namuomba Mhe. Rais, hilo la pili alitazame.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa naomba niingie katika sehemu za Idara hii na mchango wangu hautokuwa na mambo mengi. La kwanza ninataka niungane na Mhe. Asha Bakari Makame, tulizungumza sana mwaka juzi, tumelizungumza sana mwaka jana bado na mimi naungana naye kwa ufupi tu kumuomba Waziri akija aje atusaidie. Tulilalamika sana kwamba Serikali inaporuhusu biashara ya kuleta kuku kutoka nje ya nchi si wanauwa ile biashara inayofanywa na wenyeji ya wananchi wetu ambao wamejitolea kufanya kazi ya ufugaji wa kuku, wateja wameonekana baada ya miaka miwili, wengi waliokuwa wakifuga biashara imewashinda, kwa sababu kuku wanaoletwa kutoka Brazil au kama alivyoita Bi. Asha, Makuku madudu, gharama zao ni nafuu, hatujaweka kodi ya kuwafanya hawa wakawa ghali kuliko wale wanaozalishwa ndani. Matokeo yake tumeuwa biashara yetu ya ndani na tumeua ajira kwa watu wetu. Nilisema humu mwaka juzi kwa nguvu zote na wengine wakalichangia yamekuwa yale yale. Hivyo naomba Mhe. Waziri, akija anisaidie katika hili. Hivyo ndivyo makusudio ya Serikali kuwaangamiza ajira za raia wake ili kuvutia kuku wanaotoka nje ya nchi kuingia ndani ya nchi hapa kuliko kuku wa kienyeji au tuliowazoea ambao wanaoweza kufugwa, lakini hata hawa wengine waliokuwa wanafugwa hapa ndani, naomba hilo pia akija Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika sekta ya uvuvi. Kwanza kuwapongeza kwa azma nzuri ya Serikali ya kuwa na hifadhi ya mazingira ya kupiga marufuku aina fulani za uvuvi ili wanavyosema kunusuru mali asili zetu na mazingira. Lakini Mhe. Mwenyekiti, najiuliza kwamba ikiwa lengo ni hilo basi Serikali makini ingelikuwa pia imejipanga kuona vipi hawa watu ambao watakosa ajira kutokana na sheria mpya na kanuni za Serikali, vipi kuwasaidia kupata ajira mbadala ili kupata riziki zao na wao wakaishi kama watu wengine, hilo halionekani kama limefanyika na pamoja na ahadi nyingi za Serikali bado wananchi wa maeneo ya ukanda wa pwani wanalalamika sana kwamba wamekoseshwa ajira na hawakupewa ajira mbadala. Sasa naomba hili pia Serikali ikija ije inijibu kupitia Mhe. Waziri wamejipanga vipi katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nije katika madughuli. Naomba nije katika madughuli kwenye fedha, Marehemu Mzee Idrissa Abdulwakil akisema fedhwa. Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na mradi huu wa *MACEMP* umesaidia sana lakini tatizo kubwa la mradi huu tumelihoji mwaka juzi, mwaka jana, mwaka huu mpaka sasa hivi naona kimya labda kwa sababu naambiwa mradi umefungwa, lakini kufungwa kwa mradi si hoja ya kunyamaza kutokuhoji. Kwa nini kuna usiri mkubwa katika mradi huu. Sasa mradi mwaka jana tuliombwa fedha na zimo kwenye maelezo katika kitabu hiki za kufunga mradi huu ambazo nyengine zinatoka katika Serikali kwa sababu wahisani walikuwa tayari wamejiondoa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naombaWaziri akija aje anisaidie, hebu atuambie baada ya kufunga mradi

umefanyika tathmini na uhakiki wa mali zilizokuwepo chini ya mradi wa *MACEMP* na kama umefanyika hebu aje atuambiwe hapa wamekuta wana *assets* au mali za thamani ya kiasi gani na ni vifaa gani na anavimiliki nani, fedha nyingi sana imetoka nje na nyengine imechangiwa na walipa kodi wa Zanzibar katika mradi huu lakini leo inaonekana hakujulikani baada ya mradi kufungwa ni kama vile milki ya ule mfalme niliyemtaja. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hebu naomba Waziri akija aje anisaidie. La pili nataka anisaidie vile vile kwenye *account* za mradi huu, je zimepitiwa na kumeonekanwa nini.

Mhe. Mwenyekiti, katika jumla ya matokeo ya mradi wa *MACEMP* ni kuwa na hifadhi za maeneo haya *marine conservation*, ziko nyingi mimi katika Jimbo langu la Mji Mkongwe iko moja inayofika mpaka kwenye visiwa vidogo vidogo kule, lakini Chwaka iko, Tumbatu na maeneo mengine nina hakika hata Pemba pia zipo, baadhi yake zinatajwa katika ukurasa wa 49 wa hotuba ya bajeti katika kiambatisho nambari 8 mradi wa usimamizi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani *MACEMP* ukisoma kule kwenye ukurasa wa 49 zinatajwa kuna CHABAMCA, TUMCA, na KIMCA. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hizi zinaingiza mapato kwa sababu kumewekwa ada ya wageni wanaotembelea hizi na taarifa nilizopata kutoka katika maeneo yaliyokuwa kutoka katika jimbo langu na maeneo mengine naambiwa ni hivyo hivyo kwamba panatozwa dola 5 kwa mgeni anayetembelea pale, fedha hizi zinaingia wapi na katika *account* ipi. Nimeangalia Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hichi cha bajeti sikuona katika mapato ya Wizara na humu tunasema kwa sababu wapiga kura wetu wana haki yao humu, kwa mujibu wa kanuni zake asilimia nadhani kama sikosei 30 zinapaswa zibakie katika maeneo. Sasa hatuzioni huku hazionekani lakini naona hata katika mapato ya serikali humu hazionekani Mhe. Mwenyekiti, naomba Waziri akija katika hili aje anijibu.

Mhe. Mwenyekiti, si hilo tu naomba vile vile niingie hilo hilo katika eneo la mapato katika sekta inayohusu muungano. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeshtuka kidogo, uvuvi si suala la muungano lakini tulisukwa sukwa hapa tukazongwa zongwa tukaambiwa katika usimamizi wa bahari kuu basi uvuvi wa bahari kuu usimamiwe kwa pamoja na ikaweka *formula* ya mgawanyo wa mapato. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi napata matatizo sasa, kwa sababu nikitizama makadirio Mhe. Mwenyekiti, naomba tuangalie kiambatisho cha 11 ukurasa wa 13 cha hotuba ya Waziri, chini pale leseni za uvuvi wa bahari kuu, makaridio kwa mwaka 2012/13 yalikuwa ni shs.2,077,000,000/= lakini mapato halisi hadi April, 2013 ni shs.146,560,000/=. Kutokana na hali hiyo Mhe. Mwenyekiti, makadirio ya mwaka huu yametoka kutoka zilizokadiriwa shs.2,077,000,000/= mpaka yameekwa shs.400,000,000/=. Sasa wewe jiulize hii tija ya kuchanganya na ndugu zetu wa damu iko wapi, imekuwa kabla hatujakusanya kwa pamoja Zanzibar ikikusanya zaidi kuliko leo

tunavyokusanya chini ya usimamizi wa pamoja, sasa faida yetu ni ipi. Hapa mimi naomba nisaidiwe maelezo, kama haya ndio matokeo ya mfumo wa Serikali kuelekea moja naona bado tutaendelea kuzikataa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha zaidi kwa wananchi wanyonge wa Zanzibar wanavyokandamizwa na mfumo huu wa muungano. Huku mapato yanapungua tunapata kama nilivyosema zimekisiwa shs.2,000,000,000/=, tumepata shs.146,560,000/= lakini katika kugharimia mradi ambao tunaambiwa sasa hivi unaendeshwa kimuungano tukitizama buku hili Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 461 buku la makadirio ya mapato na matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo. Kwenye fedha za maendeleo, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja kuna mradi wa uimarishaji uvuvi wa bahari kuu kumetengwa shs.100,000,000/=. Sasa baada ya kupata faida sisi tunamchumia bwana, mapato ndio yanapungua tunapata shs.100,000,000/= tunatumia shs.100,000,000/= si biashara ya mgema hii, sawa na biashara ya mlevi kuliwa na mgema, unatoa mia unapata mia, si pata potea hiyo lakini hutoi mia Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kuna gharama za uendeshaji baadae, sasa tunapata faida gani. Mimi naomba Serikali ije itueleze hili kwa nini Baraza la Wawakilishi lisipitishe azimio kurejesha usimamizi wa uvuvi wa bahari kuu katika mamlaka ya Zanzibar, kwa sababu hili wala si suala la muungano limepitishwa katika sheria ya usimamizi tu, kwa nini tusirejeshe ikiwa hatupati faida yoyote Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosikitika zaidi kwamba tushatafunwa kwenye uvuvi wa bahari kuu tena na Ramadhani hii tunaendelea kutafunwa lakini hatujakoma. Katika kitabu cha Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 49 chini ya mradi wa *MACEMP*, naomba wasome Waheshimiwa Wajumbe katika ukurasa wa 49 nukta ya mwisho. Sasa Wizara ya Mifugo Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo Tanzania Bara na nafurahi kama wameiga Wizara ya Mifugo Tanzania Bara maana hawakuita Wizara ya Mifugo ya Muungano maana si masuala ya muungano, imewasilisha Benki ya Dunia azma ya kuanzishwa kwa mradi wa uvuvi wa ukanda wa magharibi mwa bahari ya hindi (*South West Indian Ocean Fisheries Programm SWIOFish*) vikao mbali mbali vya kujadili muelekeo wa mradi kazi zake na mipango ya utekelezaji zimeshafanyika. Mhe. Mwenyekiti, huku tumeshapigwa tunajipeleka tukapigwe tena, maana yake sisi na ndugu zetu wa damu katika kutukandamiza na kuwanyonya wananchi wa Zanzibar tumekaa kama mbwa na chatu, mbwa analia lakini anajipeleka tu kwa chatu. Tumeshapigwa kwenye bahari kuu hatujatosheka tunaweka na mradi mwengine wakatumalize sasa, nataka maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho katika hili hili la uvuvi la mradi wa bahari kuu. Nimesema hapa kwamba mapato yameshuka, kama kuna dhulma ya ndugu

zetu waliotupenda sana wa damu upande wa pili wa bahari pia utakuja kuniambia Waziri, lakini upande wa pili nnazo taarifa kwamba pia kuna ufisadi mkubwa katika mamlaka inayosimamia uvuvi wa bahari kuu. Mhe. Mwenyekiti, siku hizi taarifa unajua kuzipata si kazi kubwa. Ninazo nyaraka hizi hapa Mhe. Mwenyekiti, nimezipata kutoka katika *website ya Indian Ocean Tuna Commission* (*IOTC*), hii ni tume inaitwa katika bahari ya hindi kusimamia uvunaji wa samaki wa Tuna tunamwita jodari.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bahati mbaya katika shughuli nyingi nilizozifanya lakini uvuvi haumo, mwalimu wangu Mansour Yussuf Himid kanifundisha mengi lakini uvuvi hakunifundisha bahati mbaya. Mhe. Mwenyekiti, katika *Indian Ocean Tuna Commission* taarifa nilizozitazama zimenishitua. Sasa naomba kwa sasa hivi nataka nimuone Mhe. Waziri na Wizara yake ukweli wao katika hili, sisemi zaidi ya hili nakwenda katika vifungu, haya ninaweka lakini nataka aje anisaidie kwamba kuna taarifa katika mamlaka yao hii ambayo inaendeshwa kwa pamoja lakini makao makuu yapo hapa Zanzibar, inaandikishwa meli kwa leseni za kughushi, meli za uvuvi wa bahari kuu kwa leseni za kughushi na haraka haraka nikiangalia humu katika yaliyokuwa yameripotiwa katika *Indian Ocean Tuna Commission,* kuna meli mbili zimetajwa, kuna meli inaitwa *Hwa Kun* ya Taiwan na kuna meli *Hsiang Fa* ya Seyshelles inatumia bendera moja ya Seyshelles na moja Taiwan, lakini ziligundulikana kwa kuja ripoti hii zinavua katika ukanda wetu wa bahari na nimefurahi hata sikutarajia kwamba mpaka ramani zinaonesha visiwa vya Unguja na Pemba vilipo na nishani hii inaonesha meli hizi safari zake. Sasa mimi nashukuru mamlaka inahitaji kufanya kazi kubwa inayofuatilia ukisoma hii mamlaka yepi, lakini baada ya mamlaka kuhoji naambiwa mamlaka yenyewe ni hizo mamlaka za kimataifa, kwamba hawa mmewapa nyinyi leseni na ku-*operate* katika bahari yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa ziko mbili lakini si mbili, kuna meli nyingi sana kwa sasa hivi na-*hold* kwanza nitakuja kwenye vifungu, nataka nione ukweli wa uongozi wa Wizara hii waje watuambie hapa wamechukua hatua gani kwa suala hili na kuna mtendaji anayetajwa hebu aje atuambie nani aliyehusika kutayarisha leseni feki za kughushi kuzipa meli hizi, kama wao hawamtaji mimi namjua nitakuja kumtaja, lakini katika Mahakamani tunasema *the honest is on their side* sasa hivi, kwanza nawapa wao upande wao waje wanitajie huyu aliyetoa leseni feki nani na halafu aje atuambie kwa leseni hizi feki tumepata hasara kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wanadhalilika sana, wanakwenda hospitali hakuna dawa, tunapeleka watoto skuli wanaambiwa wakachangie, maji unaambiwa changia, kwa sababu unaambiwa Serikali yetu ni changa na sijui itakua lini, lakini kwa wizi wa namna hii kila siku itaendelea kuwa changa au

itakuwa imedumaa. Kwa hivyo nataka maelezo ya kina juu ya hili na yale mengine nilowaambia na hapo Mhe. Mwenyekiti, kuwaambia mbali ya kuomba Wizara ije itupe maelezo, lakini baada ya maelezo haya niiombe Kamati yetu ya *PAC* ikafanye uchunguzi wa kina katika maeneo haya yote ambayo nimeyataja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo haya kwa niaba ya wananchi wanyonge si wa Mji Mkongwe tu bali wa Zanzibar nzima waliokoseshwa haki zao kwa watu kujitajirisha kupitia migongo yao, siungi mkono bajeti hii na nitazuia shilingi mpaka nipate maelezo ya kina.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake pia nikiwapongeza watendaji wake wote kwa hotuba yao hii ambayo wameiwasilisha hapa jana katika Baraza letu hili tukufu.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuniamsha salama na nikafika hapa leo na ukanipa ruhusa ya kuweza kuchangia katika hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa 3 unaosema mafanikio ya sekta ya mifugo. Nilikuwa kidogo Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13 kwenye sekta ya mifugo imeweza kupata mafanikio kadhaa miongoni mwa mafanikio haya ni kama haya yafuatayo:-

1.Kuimarika kwa utoaji wa huduma za uzalishaji na utabibu wa mifugo.

2 Mwenyekiti, mitambo mipya kumi na moja iliyojengwa Unguja nane na Pemba mitatu na kujumlisha kuwa mitambo 24.

Hapa Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri, kwa kupata mafanikio haya.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikija katika ukurasa wa 4 kwenye changamoto ya sekta ya mifugo ambayo inasema kuna upungufu wa wataalamu wa sekta ya mifugo. Hapa nimuulize Mhe. Mwenyekiti, kwa nini tuwe na upungufu wa wataalamu wakati ya kuwa watoto wetu tunao ambao wamemaliza skuli wanazurura ovyo wako vibarazani wanahitaji kuajiriwa, kwa nini erikali haifanyi jitihada hii ya kuwaajiri watoto wetu kwenda kusoma ili kupata wataalamu ambao wataweza kuiongoza nchi yetu hii.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba Mhe. Waziri amesema kumejengwa mitambo 11 na jumla yake ni mitambo 24. Je, Mhe. Waziri nimuulize mitambo hii ya nini wakati hatuna wataalamu. Hebu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anambie mitambo hii iliyojengwa 24 ikae pale kama ni kioo tu, wakati haina wataalamu? Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna uhaba wa malisho hasa wakati wa Kiangazi na uchache wa maeneo ya malisho. Hapa niungane naye kweli Mhe. Waziri kwa sababu wakati wa kiangazi hata sisi wafugaji wa majumbani huwa majani ni tatizo. Sasa nimwambie Mhe. Waziri kwa nini hawatengi eneo maalum ambalo litakaloweza kuwaajiri wafanyakazi ili kwenda kupanda majani pale na ikawa ni majani ya malisho ya ng'ombe wakati waajiriwa hao watakuwepo pale kupanda majani na kutilia maji ili kupata malisho ya ng'ombe wetu.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nije katika Idara ya Mazao Baharini ukurasa wa 28. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa huu unasema kwamba,

> "Idara ya Mazao Baharini ina jukumu la kuwaendeleza wafugaji wa samaki na mazao ya baharini, wakulima wa mwani pamoja na wadau wengine wanaojishughulisha na mazao ya baharini kwa ajili ya kuinua hali zao kiuchumi na kuinua pato lao la kitaifa".

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kifungu (a) kinasema,

> (a) "Kuimarisha ukulima wa mwani na ufugaji wa mazao ya baharini".

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hivi sasa kuimarisha wakulima wa mwani wakulima hao tayari wamekwishaimarika, kwa sababu hivi sasa niseme kwamba katika wilaya na shehia yangu kuna mwani mwingi sana ambao umekosa wanunuaji na hivi sasa wananchi wanadhalilika sana, kwa sababu wanategemea kwamba wapate wanunuzi ili wapate sikukuu za watoto wao lakini hadi hii leo mwani uliorundikana ni mwingi sana majumbani na wenyewe wanashindwa hata kukaa ndani kwa harufu. Kwa hivyo, nimwambie Mhe. Waziri aliangalie suala hili la kuwapatia wanunuzi wa mwani na pia aangalie suala la kuwapatia soko na suala la kuwaongezea bei wakulima hawa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri alione hilo.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa huo huo wa 29 ambao unasema,

"Jumla ya watu 29 wakiwemo wajasiriamali 23 na wafanyakazi sita (6) waliyohudhuria mafunzo juu ya njia bora za ufugani wa mazao ya baharini".

Mhe. Mwenyekiti, hapa nimpongeze pia Mhe. Waziri kwa kuwapa elimu wajasiriamali wetu ambao hivi sasa wanajiendeleza katika ufugaji. Lakini niseme pamoja na kuwapa mafunzo hayo wizara imefanya utafiti gani ya kuwa wajasiriamali hawa wanayatumia mafunzo katika vikundi vyao au wanayatumia mafunzol hayo katika mioyo yao tu. Mhe. Waziri anieleze mafunzo hayo aliyowapeleka wafanyakazi na wajasiriamali hawa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikija katika ukurasa wa 6(a) kuongezeka kwa idadi ya samaki wanaovuliwa kutoka kilogramu 28,758,997 zenye thamani ya shilingi 85,667,819,035. Mhe. Mwenyekiti, niseme idadi hii iliyoongezeka ni kutokana na wavuvi na wafugaji, lakini Mhe. Waziri yeye anataja kwamba thamani ya pesa walizozipata na kilogramu ambazo wamezipata lakini haangalii kwamba kuna mabwawa ambayo yamepata hasara kubwa sana wakati wa mvua zilizopita na tayari nimeshamuendea nikamueleza, viko vikundi vyangu ambavyo hivi sasa vimeathiriwa na maji ambapo samaki 300 walipotea kutokana na kukokotwa na maji. Mhe. Waziri hadi hii leo bado hajanipa jibu lolote kama wale watu atakwenda kuwatembelea au kuwafariji. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze hapa, isiwe kwamba kutangaza thamani ya fedha zinazopatikana tu kutoka kwa wavuvi hawa lakini pia atangaze kwamba alikwenda kuwaona wavuvi hawa walioharibikiwa na mazao yao hayo ya ufugaji wa samaki.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nimwambie Mhe. Waziri kwamba vipo vikundi ambavyo hivi sasa vinahitaji kupewa taaluma. Kiko kikundi kimoja cha Kangani kinaitwa, 'Mungu ndiye Hakimu' na kiko chengine cha Kukuu ambacho hiki pia Mhe. Waziri nimeshamjia kumwambia kwamba bado hawana taaluma ya ufugaji na kipindi chengine ambacho walikokotwa na maji samaki wao. Je, Mhe. Waziri ni lini atavitembelea vikundi hivi ili kuvipa motisha na pia kuwapa misaada ya kuweza kujikimu katika vikundi vyao hivi.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, viko vikundi ambavyo viko katika Wilaya ya Mkoani ambavyo viko Wambaa. Vikundi hivi ni vya ufugaji, navyo pia Mhe. Mwenyekiti, vikundi hivi vinafuga samaki wazuri tu lakini pia Mhe. Waziri sijasikia hata siku moja kusema kwamba katembelea kikundi cha Wambaa, Chwaka Kiwani ambapo watu hawa wamejiajiri wenyewe kufanya kazi ili kuleta maendeleo ya nchi yao pia na kuisaidia serikali. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atapokuja hapa anipe jibu.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba niishie hapo naunga mkono pale Mheshimiwa atakaponijibu. Ahsante.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti ya wizara hii. Kwanza kabisa nachukua fursa hii kuwashukuru Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao kwa kazi kubwa na nzito ambayo wameifanya.

Lakini baada ya hapo napenda pia kuanza kwa kurejea nyuma katika bajeti ya mwaka ulipita ambapo mwaka uliopita nilisimama hapa na kuomba baadhi ya mambo ambayo niliomba katika wizara hii niweze kupata ufafanuzi au mwelekeo wa mambo hayo.

Jambo la kwanza ambalo ningeanza nalo ningependa kupata taarifa kwanza inayohusiana na eneo la Kizingo ndani ya Jimbo la Kikwajuni hapa Zanzibar. Eneo lile mwaka jana nilichangia naomba kunukuu,

> "Baada ya maelezo hayo sasa niseme mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naomba kuuliza swali moja atakapokuja Mhe. Waziri, lile soko la samaki katika eneo la Kizingo je, litakamilishwa lini kujengwa au serikali ina mpango gani juu ya soko lile".

Mhe. Waziri alipokuja hapa alitwambia na tunaomba atuelekeze jinsi gani ataweza kutupa maelezo juu ya utekelezaji wa kuliimarisha na kuliendeleza eneo la Kizingo kwa kujengwa soko la samaki katika maeneo yale. Naomba kupata maelezo yatakayoweza kunitosheleza ili niweze kufahamu harakati hizi za soko la samaki katika maeneo ya Kizingo limeishia wapi.

La pili Mhe. Mwenyekiti, mwaka juzi niliposimama katika bajeti ya Wizara ya Mifugo nilichangia hapa, lakini pia nilibahatika kuchangia katika maswali na majibu juu ya kuangalia uwezekano wa kujenga Chuo cha Uvuvi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni visiwa na visiwa vyetu vya Zanzibar vimezungukwa na bahari kila upande, lakini wakaazi wa nchi ya Zanzibar ni watu maskini sana na wengi wao wana taaluma ya masuala ya uvuvi. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba pamoja na raslimali hii ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia nayo kwenye visiwa vya Zanzibar, hadi leo hii hatujajipanga juu ya kuweza kuwa na Chuo cha Uvuvi ambacho kingeliweza kuwasaidia wananchi wetu wa Zanzibar na kuweza kuondokana na…

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe minong'ono imezidi, Waheshimiwa Wajumbe naomba mkae kimya ili Mheshimiwa aweze kuchangia na kusikilikana vizuri.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ningelimuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelekeze ni mikakati gani ambayo imepangwa na wizara yake kuhakikisha kwamba Chuo cha Uvuvi Zanzibar kinajengwa kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar. Lakini kama hiyo haitoshi endapo kwamba watakuwa wana mipango ya muda mrefu ambayo itakuwa haina uwezo kwa sasa kujenga chuo hicho, ningeliomba katika maeneo ambayo ni ya elimu ya amali basi wafikie muafaka na watu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili waweze kuwapa maeneo angalau japo mabanda fulan wapewe waanzishe madarasa haya katika masuala ya uvuvi kwa upande wa Zanzibar.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika kitabu chetu hiki tulichonacho sasa katika ukurasa wa tano ambapo hapa kunazungumzia suala la changamoto mbali mbali mpaka ukurasa wa saba zinazohusiana na masuala ya uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, ningeliwaomba watendaji pamoja na wasimamizi wa Wizara ya Uvuvi hebu waangalie mtazamo na malengo ambayo walikuwa wamejipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, halafu aweze kulinganisha vile vile na mipango yao na matumizi ambayo wamejipangia katika mwaka 213/2014. Kuna mambo mengi ambayo yalikuwa yameahidiwa katika kipindi kile lakini katika kitabu chetu hiki hatukukuta mwelekeo wala kuendeleza wa mambo yale. Sasa sijui katika utaratibu wa kutayarisha haya maelekezo ya bajeti sijui wanakuwa wana-*base* vipi. Tunachotaka kukifahamu hapa ni utekelezaji wa yale malengo ambayo walikuwa wamejipangia mwaka 2012/2013 ili tuone utekelezaji wake mwaka 2013/2014 yamekuwa vipi ili tuweze kupata mbinu ya kuweza kuidhinisha fedha nyengine kwa sababu ya maelekezo ya mwaka unaofuata.

Jengine ambalo nataka kuchangia nimejaribu kuangalia katika hiki kijitabu wenzangu walitembea sana waliopita hususan Mhe. Ismail Jussa katika maeneo ya bahari kuu. Mimi nilikuwa nataka nije zaidi katika maeneo ya mifugo. Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki nimejaribu kukiangalia sikuona muendelezo wa mifugo yetu mengine ukiacha mbali mambo ya kuku. Katika kitabu chetu cha mwaka jana tulipata kuelezewa vile vile jinsi ya vinyama kama paka, mbwa na wengineo ambao walikuwa wanaendelezewa harakati za kupigwa sindano ili kupunguza vizazi vya wanyama hawa. Kwa namna moja au nyengine vinyama hivi vina baadhi ya faida kwa binadamu lakini vina hasara pia katika maeneo ya binadamu, lakini kulikuwa kuna utaratibu huu wa kuangamiza niseme labda au kuwapunguzia uzazi vinyama hivi. Sasa katika

kitabu chetu cha mara hii hatukuona utaratibu gani unaendelezwa. Kwa ile taarifa ambayo nilikuwa nimeanza nayo mwaka jana.

Lakini pia tukiondoka hapo nakuja katika kitabu chetu hiki kuna malengo ambayo yalikuwa yamepangwa katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2012/2013 juu ya uzazi wa mbuzi kwa kutumia sindano. Mbuzi wale mwaka jana walikuwa wamefanyiwa matayarisho mazuri katika ukurasa wa 20 wa kitabu chetu cha mwaka jana, lakini hatukupata muendelezo wa kuweza kufahamu je, ni maendeleo gani yanapatikana kwa mbuzi wale ambao wanazalishwa kwa kutumia utaratibu wa kutumia sindano.

Jengine ambalo nataka kupata ufafanuzi na ufahamu katika kijitabu chetu hiki cha mwaka jana katika maeneo ya malengo yao, walizungumzia vile vile katika ukurasa wa 38 kwamba katika mwaka wa fedha 2012/2013 idara itasimamia utekelezaji wa miradi miwili, mradi wa uhifadhi wa mazingira ya bahari (*MACEMP*) na mradi wa bahari kuu. Tungelipenda kupata maelekezo miradi hii imefikia katika utaratibu gani hadi hivi sasa ambapo bado tunahisi kuna matatizo ambayo watu wetu ili yaweze kutatuka yanahitaji maelekezo pamoja na usimamizi mzuri wa fedha na mambo mengineyo ambayo yanatokana na miradi hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa nije katika suala zima la uchinjaji wa ng'ombe katika maeneo yale ambayo yamewekwa kwa ajili ya kuchinja wanyama hao. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hali nzuri inayoendelea katika machinjio ya wanyama pale Kisakasaka, lakini tungelipenda vizuri zaidi wizara hii ikajitayarisha kuhakikisha kwamba ng'ombe wote ambao wanachinjwa katika visiwa vya Zanzibar wawe ni ng'ombe ambao wanapita katika taratibu ambazo zinapaswa kisheria, na kama pale Kisakasaka ndio eneo kuu basi na wao wawe wanajua utaratibu mzima wa ng'ombe wanaochinjwa katika maeneo haya na taratibu zile za kiafya pia zinafuatwa. Lakini kama hiyo haitoshi ningeliomba wizara yake kile kitengo ambacho kinakuwa kinaangalia usalama na umakini wa zile nyama ambazo zinauzwa katika masoko yetu wahakikishe kwamba nyama zile zinauzwa zikiwa katika misingi ya hali ya salama ili wananchi wetu wasije wakaathirika. Kuna maelekezo kwamba baadhi ya wananchi wanalalamika kuwa baadhi ya nyama huwa zinalala na nyengine huwa zinaharibika lakini wanaendelea kuuziwa, ningeliomba wizara ilisimamie hili na kuhakikisha kwamba wananchi wanakula nyama iliyo safi na salama.

Baada ya maelezo hayo sasa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono hoja kwa asilimia tisini nabakisha asilimia kumi mpaka nitakapopewa majibu ya kuridhisha na Mhe. Waziri. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kutia nyalio kidogo katika hoja iliyopo mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutujaalia hazina ya afya njema na uwezo wa kutoka katika maeneo yetu hadi hapa. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Allah (*S.W*) na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kukushukuru wewe kunipatia angalau hizi dakika 15 za kueleza chochote hapa. Kwa kweli nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Sasa nadhani nianze tu katika hoja iliyopo mbele yetu na ukurasa wa tano katika ibara ya 22 katika sekta ya uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, asilimia karibu 60 za Wazanzibari wanaoishi katika miji na vijiji vya nchi hii wamewekeza maisha yao katika sekta hii ya uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, ukizungumzia uvuvi katika nchi hii na ukiuwezesha uvuvi katika nchi hii maana yake umefanya mambo matatu katika moja (*three in one).* Unapomuwezesha mvuvi Mhe. Mwenyekiti, basi moja kwa moja umemuajiri mchuuzi wa samaki. Kwa hivyo mchuuzi wa samaki atakuwa amepata ajira pale kwenye uvuvi. Halikadhalika mtu wa tatu kunufaika ukiacha mvuvi mwenyewe basi atakuwa ni mama lishe hawa. Kwa kweli mama lishe watakuwa wameneemeka sana kama utaiinua sekta ya uvuvi katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, ni aibu sana kuona kwamba makundi makubwa ya wale omba omba sasa hivi humu mitaani ni akinamama. Sasa kama utaweza kuufanya uvuvi ukautilia bajeti nzuri na ukaimarika basi utapunguza kwa kiasi kikubwa sana hili tatizo la omba omba katika nchi hii. Katika hilo Mhe. Mwenyekiti, samahani kwa kukwita Spika lakini Mungu akipenda Baraza lijalo tutakupa Uspika tupate Spika mwanamke.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili nadhani serikali yetu haikuwa *serious*, serikali yetu ni yenye kusema-sema tu maneno haipendi sana kufanya matendo, na serikali makini mara nyingi hutakiwa ifanye matendo sio kusema. Umakini wa serikali ni ule unaopatikana baada ya kufanya matendo na kuwaacha raia wake waseme maneno kwa kuishukuru. Sasa Mheshimiwa hapa tunazungumzia mambo ya *poverty reduction and income generating* katika MKUZA II, yaani kupunguza umaskini na kuongeza kipato cha wananchi wetu tunazungumzia kwenye nadharia lakini kimatendo ni tatizo. Hivi wakati nazungumza Mheshimiwa katika sekta hii ya uvuvi suala la kupunguza umaskini na kuongeza kipato cha wananchi ni tatizo na ni pahala pekee ambapo tungeweza kuutekeleza MKUZA II kwa kiasi kikubwa sana kama

tungeuwezesha uvuvi. Leo inasikitisha Mheshimiwa achilia mbali kuwawezesha wavuvi bajeti ya nchi hii haiwezeshi hata sisi kuwalinda wale samaki wetu walioko katika bahari kuu wasiibiwe, yaani haiwezeshi ni tatizo Mheshimiwa.

Mimi sidhani kwamba ni tatizo la umaskini lakini mipango ni kuchagua lazima uangalie umuhimu. Mhe. Mwenyekiti, sisi kama kisiwa bahari ni hazina lakini baharini ni hazina zaidi lakini tumeshindwa kuweza kudhibiti bahari yetu isiibiwe kutokana sijui na ubahili au kutokuwa na mipango mizuri. Hivi karibuni zile meli za Dar es Salaam za Waziri gani yule Magufuli, samaki wale nina hakika asilimia kubwa walitokea huku kwetu kwa sababu hatuna udhibiti, bajeti ya nchi hii haiwezeshi kumvua samaki achilia mbali kumlinda, sijui shilingi milioni 200 wanapewa nani namuonea huruma sana yule kijana Mussa Aboud Jumbe, Mkurugenzi wa Idara ya Mazao ya Baharini, kwa kweli anafanya kazi ya ziada lakini hatumuwezeshi kabisa kabisa Mhe. Mwenyekiti.

Mimi nadhani tuwe-*serious* kuweza kuvuna hii hazina tuliyonayo. Zanzibar wanatushangaa tukisema maskini tukienda nje ya nchi, sisi wengine tumebahatika kusafiri katika nchi hizi za ulaya na hata zile za Falme za Kiarabu wanashangaa kwamba Wazanzibari tunakuwa maskini huku tumezungukwa na bahari yenye samaki, tumezungukwa na bahari yenye fukwe nzuri halafu tunajiita maskini halafu nchi yetu ina kijani cha kutosha, umaskini huu unatoka wapi Mhe. Mwenyekiti. Mimi nadhani tujipange vizuri tu na ikiwa serikali ina matatizo ya wataalamu katika mambo haya basi njooni *backbenchers* tuko watu tuliyobobea katika mambo ya *animal husbandry*, njooni mumege mambao huku. Mimi nadhani msiende *by trial and error* mfanye mambo *scientifically* kuweza kuona kwamba kilimo kinaendelea katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine kwamba serikali yetu haiko *serious*, kwanza tukiangalia kule Pemba. Pemba Mhe. Mwenyekiti, kuna vikundi vingi vya akinamama vimewekeza katika masuala ya bahari, achilia mbali kusaidiwa *financially* lakini hata kupata zile *technical advise* hawapati, hawatembelewi. Kwa mfano, kikundi kimoja katika jimbo la Mhe. Hamad Masoud wanakiita Kichakasi Shangi. Hawa mama wanavua samaki vizuri tu, Kichakasi Shangi ni akinamama ukienda wamechachamaa sana pale lakini kwa kweli hawasaidiwi katika kupewa mawazo ya kitaalamu wala hawasaidiwi katika suala zima la kupewa fedha, ingawa Waziri wa Fedha ndio anatoka huyo lakini naomba usikie vile vile. Sasa katika hili Mheshimiwa mimi nadhani hawa akinamama wameshajihamasisha.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wavuvi wa pweza katika kijiji changu cha Umangani Vitongoji wamejikusanya pamoja pale Vitongoji Umangani akinamama wamewekeza katika masuala ya kujivulia pweza. Mhe. Mwenyekiti, pweza ni lishe halikadhalika pweza ni tiba na hawa akinamama wanajitahidi sana na wanawapata, lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu sana akinamama hao katika kazi yao ya kuvua pweza, kule ukienda kuvua unapita katika miamba ina miba, *they can't avoid even* kuwa na yebo yebo, hawawezi hata kuvaa ile yeboyebo wasichomwe na miba serikali yetu ipo inawatazama tu na huku wakishavua wale pweza hata soko ni tatizo Mhe. Mwenyekiti. Mimi nadhani katika hili muone jinsi ya hawa akinamama walivyojitolea muweze kuwapa mawazo ya kitaalamu na muweze kuwasaidia *financially*.

Kwa mfano, mpaka hivi sasa wale akinamama wa pale Vitongoji huwaonea huruma, bado wanatumia zile chokoo kwa kuvulia pweza na misumari ya kienyeji, wakati mimi niko pale Rashidia nilikuwa naona kuna pweza anaingizwa tu katika nyumba yake anatoka mwenyewe kazi yako ni kumkamata na kumchukua, leo wale akinamama wamefanya vibyongo kwa kuvua pweza, ni tatizo tuwasaidieni, kuwaajiri serikalini uwezo hatuna wameshajiajiri wenyewe hatuwasaidii jamani ni tatizo. Kwa hivyo, naomba serikali ione hilo na iweze kuwasaidia hawa maskini wa Mungu angalau kwa kuwapatia uwezo wa kununua yebo yebo ili ile miguu isichomwe na miba kusudi kama sikukuu inayokuja waweze kupaka hina na wao pamoja na wenzao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa twende hapa Unguja na wao vile vile wana matatizo, akinamama wamejitolea wako imara katika kujipunguzia umaskini. Nilitembelea katika kikundi kimoja cha Raslu-Minallahi kilichoko Kizimkazi nafikiri jimbo la Mhe. Haroun Ali Suleiman, hili wamepewa boti na *TASAF* miaka kadhaa iliyopita lakini hao akinamama mwanangu eeh! makini sana, wanakwenda mbali huko visiwani wanachukuliwa na lile boti wanakwenda kuwanasa madagaa boti ni moja tena ndogo halafu wanalazimika wanavua karibu mara tatu wanakuja kupeleka madaga wao wamebakia kisiwani tu huko, huku watoto wao wanataka kunyonya, huku wanataka kuwastarehesha mababa wenye nyumba, hawapati maskini kwa kusubiri kwamba boti hiyo hiyo ilete madagaa mara tatu huku ni mwendo karibu wa masaa mawili kutoka juu Kizimkazi kuleta juu madagaa yale ni tatizo Mheshimiwa. Nadhani tuwasaidie wale na isitoshe wale ni akinamama *incase of emergency* wale ni akinamama hao akinababa maji yaliopo hawawezi kuyashika basi jamani hata *life jacket* mbili tatu kuwasaidia pale ndio pia hawawezi, hawawezi kuwanunulia mashua ya pili mkawapa wale jamaa zangu wa Kizimkazi basi hata hizo *life jacket* mbili, tatu au nne mkawaambia *in case emergency* hizi hapa jamani, wakiambiwa wanasema serikali haikui, serikali

tangu 1964 *up to date*, kama ni mtu tayari anakulisha huyo wataalamu wetu ndio wanaotuendesha katika ndege tuliowazaa mwaka 1964, ni tatizo.

Mimi nadhani lazima wawe makini serikali wanatuaibisha, wawe makini katika kuleta maendeleo ya nchi hii, wawe makini katika masuala mazima haya ya kuongeza kipato na kuwasaidia hawa akinamama katika kuondosha umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, kuna akinamama wana kikundi chao cha kulima lulu na chaza sehemu za Mkoani Makombeni, hawa mama utashangaa sana wameanza kuzalisha lulu za kiwango kabisa wewe ukiona hiyo lulu unataka uitizame tu. Mimi nilikuwa siijui nikatembelea siku zile niko kwenye Kamati ya Wanawake na Watoto nikaenda kutembelea kule, kwa kweli nimeridhika sana na jinsi ya wale akinamama walivyojiimarisha lakini wanafanyakazi katika mazingira magumu, bila ya kupatiwa misaada.

Mhe. Mwenyekiti, huteremka maji mpaka kwenye shingo kwenda kuzamia hizo lulu zao wanateremka mpaka kwenye mapaja hapa huku wakiwa hawana hata visaidizi. *Incase* kama yule mama hana hata *life jacket.* Mimi nadhani muwatembelee na muwaone mnaweza kuwawezesha vipi hawa akinamama naona kwa jinsi ninavyomuona Mhe. Naibu Waziri ni mtu mmoja mwenye usikivu kabisa mwenye taaluma kabisa kabisa anaweza kulisikia hili na akaweza kutembelea huko Kizimkazi na hawa mama zangu wa pale Makombeni.

Mhe. Mwenyekiti, kuna uvuvi wa kamba kocho pale kinapokaa hasa Umangani kuna vijana wamejiajiri pale wanavua kamba kocho. Hawa wana bei sana na kama tungewaendeleza nakuhakikishia kwamba wangekuwa sasa hivi wameshapata kipato na wameshaweka ajira kwa wenzao. Lakini tangu waanze kuvua wanazama chini sana wakifika kule ni tatizo wanatafuta kamba pumzi zinawamalizika kama ana uwezo wa kuvua kamba 20 kwa siku, basi atapata kamba 5 kwa sababu pumzi zinawamalizikia, na wao hawana uwezo wa kununua yale masanduki ya hewa wakavaa mgogoni wazama kule chini. Jamani hata mtungi mmoja ule wa hewa kuwasaidia pale au kuwakopesha na wanapeleka Kenya kamba wale wanapata fedha nyingi. Kama wanawavua wengi wataweza kulipa tu, sasa mnashindwa hilo. Mimi nadhani acheni ubaghili huo jamani kabisa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nawatetea akinamama tu mwezi huu wa Ramadhani, wanaovua mwata hawa ambaye pia ni Mwenyekiti wa UWAWAZA. Kuna akinamama wenzeko kule Kangani wanavua mwata. Mwata ni *delicious* nafikiri wengi hamuujui, lakini mwata kwa kweli is a *delicious and nutritions*, unalika na kwa kweli ni mtamu basi hawa

akinamama huwa wanapata tabu sana na wanatumia vile vile chokoo kuwachokolea mwata na huku wakiangalia wanatembea masafa marefu hawapati kitu. Hebu jamani niendeni huko mkawasaidie akinamama ili waweze kuvua vizuri mwata.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaondoka katika suala hili la uvuvi sijaingia katika suala la mifugo naona mambo haya ya kufuga samaki kuna sehemu inaitwa Kibokoni wamejitokeza vijana wamechimba bwawa zuri tu la kuweza kufuga samaki Vitongoji Kibokoni pale. Hawa vijana tu kwa utundu wao wameweza kulichimba likiongozwa na kijana mmoja anaitwa Chuma cha Pua ndio umaarufu wake jina lake Ali Khamis Fereji. Huyu kijana kafanya bidii kachimbisha lile bwawa na samaki wanakwenda lakini hawana utalaamu, hawajui kuwa-*handle* wale samaki. Tatizo hebu nendeni mkawape maneno ya kitaalamu ili waliendeleza hili bwawa. Nadhani mkiwapa haya maneno ya kitaalamu mnaweza mkafanikiwa sana na wale vijana wakafanikiwa na familia zao zikafanikiwa na wakiwa samaki wengi mpaka sisi tutafanikiwa, kwa sababu watalipa kodi baada ya kujiajiri wenyewe katika sekta ya uvuvi.

Mimi nadhani serikali Mhe. Mwenyekiti, haiko makini katika hili kwa sababu mimi nilitembea nchi moja hapa hapa tu nchi zilizokuwepo Kusini mwa Jangwa la Sahara sitaki niitaje. Lakini nilipofika kule wanafuga samaki katika *interval* ya muda mdogo tu hivi samaki wao unaona tayari wamekuwa kwa sababu kuna dawa wanawatilia mle. Kuna dawa ambazo zinawasababisha wakue kila baada ya wiki mbili senti mita tatu wanakuwa na wanaongezeka sijui *zero point* ngapi *gram*.

Sasa unaweza kuvua samaki baada ya mwezi tu ukapata masamaki makubwa kwa sababu wanawawekea dawa ambayo wanaita *somatocrofin powder,* hili ni neno la Kilatini, maana yake ni unga unaofanya mwili ukue. Sasa wanawatilia mle na wakishawatilia baada ya muda wa wiki mbili tatu hivi unaliona limekuwa kubwa. Lakini humu wewe unakaa na samaki miezi sita hajapata ukubwa. Huku ukitilia maanani kwamba kuna mabadiliko ya tabia ya nchi, joto linapanda sasa hamuwasaidii kwamba joto limepanda tuwasaidie vipi ili samaki wakue ilimradi wanafanya mambo wakati na wataalamu mpo jamani. Tatizo wasaidieni hawa kusudi ili na wao waweze kulisaidia taifa letu pale watakapokuwa na mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, nije moja kwa moja katika masuala ya ufugaji. Hii mifugo hapa ufugaji ni njia moja muhimu sana ya wananchi kujipatia kipato na njia hii Wazanzibari karibu asilimia 40 tumeekeza katika masula haya ya mifugo hasa sisi tulioko mashamba. Mimi *in profession* ni mwalimu lakini karibu miaka 20 sijakaa darasani kufundisha, kazi yangu kubwa ni kufundisha. Kazi yangu kubwa ni kufuga tu kuku, ngombe na mbuzi. Tatizo ninalokumbana

nalo katika ufugaji ni moja kwamba sisi hatuna taaluma ya kufuga na serikali yetu haiko *dynamic* imekaa inatuangalia tu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna njia tatu ambazo mtu anaweza kufuga mifuko yake. Njia ya kwanza wanaita unawaachia ndani mifugo, huwatoi unawapelekea chakula humo humo. Njia ya pili unaichukua mifugo unaweka ndani usiku lakini asubuhi unakwenda kuwalisha ambayo pia lazima uwe na banda na njia ya tatu hii ya kuwaweka nje. Ndio hiyo tunayotumia sisi maskini ya Mungu saa 24 jua mvua mifugo yetu sisi iko nje. Sasa njia hii ina madhara na hata kama huna ushauri wa kitaalam, hawa maaafisa wa mifugo sijui wana nini.

Lakini maafisa mifugo hawatufiki kule kuja kutusadia sisi wafugaji. Mhe. Mwenyekiti, matokeo yake mimi nina kuku wa kienyeji tuseme mathalani kuku wangu 200 wa kienyeji huwa nawaachia wanaranda huko. Matokeo yake vifaranga wanakumbana na wale adui zake Mhe. Fatma Fereji wanachukuliwa na kunguru. Kwa hivyo, baada ya kupunguza umaskini sasa tunaongeza umaskini.

Halafu isitoshe kuna hawa vijana wanaovuta unga wanawakamata kuku wanawaiba halafu inakuwa ni tatizo. Baada ya kupunguza umaskini sasa unawaongezea. Sasa sijui mnaweza mkatusaidia nini nyinyi wataalamu. Sisi wafugaji tunaweka mifugo yetu nje tuliokuwa hatuna uwezo wa kujenga mabanda, tunataka tufuge kuku wengi lakini wanaibiwa na kunguru na wanaibiwa na hawa wavutaji wa unga inakuwa ni tatizo.

Mimi nafuga ng'ombe lakini nakwambia katika Wilaya ya Chake Chake tuna tatizo yeye Mhe. Mohammed Aboud pale juzi juzi nilimuuliza swali akanitia huku na kunitoa huku tu. Nilimuuliza kwamba pale ng'ombe wetu wanaibiwa na kesi zinakwenda mahakamani lakini tatizo lake huyo mwizi wa ng'ombe akishakamatwa baada ya siku mbili unamuona anaranda pale pale mtaani kesi haiendi akitoka tu hakikisha atachukuliwa tena ng'ombe pale.

Sasa hapo jamani umaskini utakuwa umeondoka au umeongezeka. Mtusaidie Serikali kama kesi tukizipeleka, hii ni hoja ya kilimo lakini nataka niipeleke kwa mtendaji Mkuu wa Serikali. Hawa Mahakama inakuwaje hawazihukumu wezi wa ng'ombe wakafungwa. Wanaendelea kutuibia ng'ombe na mbuzi wetu ni tatizo, siku ya pili unamuona keshaiba mbuzi siku ya pili anaranda randa mtaani anakuja kutuibia tena.

Mimi nadhani Balozi Seif Ali Idd lisikie hilo halafu ufuatilie mambo haya na Polisi sisi Wapemba tunaita kusoza, yaani watatusoza watatumaliza. Wewe una king'ombe kimoja tu halafu kinaibiwa Polisi wapo, mahakama zipo, wezi wanaendelea kudunda tu na sisi tunakuwa maskini mpaka lini. Mhe. Balozi

katika hili naona limemu-*over head* huyu Waziri wa Mifugo na huyu ni waziri wako na ng'ombe akikatika mguu malishoni basi anarudi zizini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu katika kushadidia hili kidogo ninukuu maneno ya mtaalamu Bwana Shaaban Bin Robert katika kitabu chake cha 'Kusadikika', pale aliposema, "Ngombe akivunjika mguu malishoni hujikokotea zizini kusaidiwa". Mhe. Balozi Seif Ali Idd wewe ndiye zizi, sisi ng'ombe wetu wanaibiwa vibaya huko vijijini maskini ya Mungu sikukuu kama hii. Mimi ng'ombe wangu namwambia mke wangu wawafunge chini ya dirisha, kamba zinafungwa kwenye kitanda. Lakini hiyo si dawa wanakata zile kamba wanachukua ng'ombe mke wangu anaamka asubuhi ng'ombe keshachukuliwa. Ni tatizo lakini hatuna la kufanya. Katika hili Mhe. Mwenyekiti, naomba tusaidieni sana.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza tena hapo hapo mambo hayo hayo ya mifugo na nyinyi Serikali nikuulizeni kitu kimoja. Mhe. Mwenyekiti, hapa awamu ya kwanza na awamu ya pili walifanya mambo mazuri sana tu katika kutuokoa sisi wafugaji awamu ya kwanza na awamu ya pili. Lakini la kusikitisha nyinyi awamu hii iliyokuja juu juu ya mambo mnayazdharau. Sisi tulijengewa majosho ya ng'ombe kule kwetu yale ya kukoshea, wanaita mahodhi kila baada ya mwezi ng'ombe wetu wanapita. Mwenyekiti wa Afro- Shirazi anatupigia upatu tunakwenda kukosha ng'ombe wetu katika majosho haya, yaani unapigwa upatu kutoka *branch* ya Afro- Shirazi. Sasa tulikuwa tunakwenda na tuna mpango mzuri ng'ombe wetu wanakoshwa wala hatulipi hata shilingi moja, halafu tunachukua ng'ombe wetu hawana kupe unamuona kanawiri baada ya miezi tu anajifungua, mifugo ilikuwa inanawiri.

Sasa kuja nyinyi yale majosho yote mmeyadharau na hayafanyi kazi mengi yameshavunjwa. Sasa mambo haya mpaka lini ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti, sasa wanachofanya upulize dawa kwa lile *pump*, unapuliza dawa kumua kupe lakini vile vile kuna na panzi hapo utamuua, pana sisimizi pia unamua pale. Mimi nadhani muige hii mifano ya Mzee Karume na Bwana Aboud Jumbe kwa kuweza kufufua yale majosho ya ng'ombe kusudi sisi wanyonge tujue ndio kusudio letu kupeleka mifugo pale tuweze kunufaika nao.

Nimalizie kwa kuiuliza Serikali yale maziwa tuliokuwa tukiyapata Chamanagwe yako sasa. Mhe. Mwenyekiti, palikuwa na shamba zuri la mifugo pale Mtakata huku Kusini katika jimbo langu la Wawi. Pale tulikuwa tukizalisha sisi zaidi ya lita elfu nane kwa wiki tu, tunapeleka maziwa mpaka Commoro na Chamanagwe tulikuwa tukizalisha maziwa mengi tukiyapeleka mpaka Mombasa.

Inasikitisha mlivyokuja nyinyi hii Serikali iliyopo mnayaharibu haribu hatujui nini ilimradi nyie hamfanyi na yale yalikuwepo mnayaua mambo haya mpaka lini jamani. Maana ingelikuwa nyie mnafanya basi sisi tungekuwa hatusemi. Lakini Mtakata mshaiuwa hamlet, Chamanangwe mmeshaiua hamleti, mahodhi mmeshayavunja hamleti yenu nyie mambo haya mpaka lini.

Mimi nadhani katika hili itabidi Mhe. Waziri sitaunga mkono hoja hii mpaka pale mambo yafuatayo utajkaponielewesha nikaelewa.

(a) Hatma ya shamba la Mtakata na Chamanagwe ikoje ardhi zile je, bado ni za Serikali au zimeshapewa watu.

(b) Mna mpango gani wa kuweza kuwasaidia wavuvi niliowataja wale wa Kwa-Pwenza katika eneo la Vitongoji Umangani, wavuvi wa kamba kocho wa Vitongoji/Umangani,wavuvi wa mwata Kukuu Gangani, kikundi cha dagaa kilichopo Kizimkazi kile cha Ras Minallahi, Kikundi cha Kishangi Minungwini utawasaidiaje. Hapo mkishanifahamisha basi naweza kuunga mkono hoja taratibu.

Baada ya maelezo hayo ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu huu kwenye hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa wizara hii kwa kutuandalia bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu utakuwa mdogo sana maana yake mengi waliotangulia wenzangu wameweza kuyazungumza na unatuhimiza mara nyingi tusirejee rejee. Kwa hivyo, nitakuwa nanukuu nukuu madogo madogo tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa masikitiko sana lakini kwanza nianze kwa masikitiko sana juu wa wizara hii. Mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti mimi nilibahatika nilichangia kwa maandishi katika hotuba ya Mhe. Waziri huyu. Lakini katika mchango wangu mlikuwa na maswali lakini Mhe. Waziri aliniahidi kwamba atanijibu kupitia kwa maandishi vile vile kama vile mimi nilivyopeleka mchango wangu.

Lakini cha kusikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, nimekumbana na bajeti nyengine yale majibu sijayapata. Huu umekuwa ni utamaduni wa baadhi ya mawaziri kwamba tunapochangia kwa maandishi wanatuahidi kwamba wanatujibu kwa maandishi. Lakini inakuwa kama ni kichaka cha kujifichia tu,

maana wanatuondosha njiani, aah! nitamjibu kwa maandishi. Kama mpaka mwaka mzima umetimia maandishi yale hujajibiwa kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kabisa. Ndio maana nasema kwamba mchango wangu utakuwa mdogo, maana yake ule wa mwaka jana sijapata jawabu sijui nikichangia huu wa leo itakuwaje labda Mhe. Waziri atanambia. Kwa hivyo, namuomba atakapokuja hapa yale majibu yangu ya mwaka jana niyapate na haya nitokuwa nayo kidogo ya leo anichanganishie.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikianza naanza na ukurasa wa 3 wa kitabu hiki cha Mhe. Waziri kwenye sekta ya mifugo. Hapa Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia mimi narejea kile kitabu chake cha mwaka jana alionesha changamoto nyingi sana pale mwaka jana. Nimejaribu kuangalia humu labda nilitegemea kwenye kitabu hichi tutaziona namna alivyofanyia kazi zile ambazo alizoonesha mwaka jana, maana mwaka jana ninacho kitabu chake cha hotuba mna changamoto nyingi.

Sasa hebu Mhe. Waziri utwambie changamoto zile umezifanyiakazi vipi au ndio zinaendelea kuwa ni changamoto tu, mwaka huu zimeibuka tena changamoto na mwakani zitakuwa changamoto, kwa hivyo tunaendelea na changamoto tu. Mimi nafikiri hivyo tutakuwa hatwendwi. Namuomba Mhe. Waziri hebu uje utueleze zile changamoto za mwaka jana na kuna nyengine umezitaja humu kidogo mbili tatu. Lakini nina nyingi zinaonekana zimejirejea tena kuendelea kuwa ni changamoto. Sasa nilikuwa naomba maelezo katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, nasogea mbele kidogo kwenye sekta ya uvuvi. Sekta ya uvuvi nayo inajirejea. Mimi hupenda kuangalia kitabu zaidi huwa narudi kule mwaka jana na naangalia na mwaka huu bado nayo iko vile vile ina changamoto nyingi ambazo mwaka jana alizionesha na mwaka huu zimeibuka tena kuwa bado changamoto. Sasa hebu Mhe. Waziri tuambie hasa una kikwazo gani kwamba changamoto hizi unashindwa kuzifanyiakazi au zimekuwa za kudumu. Maana kama za kudumu basi usiziite changamoto hizi. Mimi nafikiri zibakie kwamba ziko kwenye kitabu tu. Mhe. Mwenyekiti, sisi tunahitaji maendeleo katika nchi yetu hasa katika sekta hizi muhimu ambazo zinazigusa jamii zetu moja kwa moja sekta hii ya mifugo, uvuvi ni sekta ambazo zinazigusa sehemu zetu moja kwa moja.

Kama mimi kule jimboni kwangu wote ninao wafugaji, wavuvi, wakulima lakini hizi sekta zinawagusa watu wetu moja kwa moja. Sasa tunapoendelea kupata changamoto tu Serikali haioneshi namna gani inazifanyia kazi, maana yake zinawavunja moyo wale wavuvi wetu na wafugaji wetu kwamba wasiendelee. Tunahitaji maendeeleo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi nafikiri

ni vyema changamoto hizi ukaja kutwambia namna ambavyo wewe unazifanyia kazi na lini zitakuwa zimeondoka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nizungumzie tena kwenye hii sekta ya uvuvi kwenye suala la mradi hapa. Nilikuwa nataka kuugusia zaidi huu mradi umezungumziwa sana na wenzangu waliotangulia mradi wa *MACEMP* kwenye ukurasa wa 48 kwenye kitabu chake Mhe. Waziri amesema kwenye mradi wa usimamizi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani *MACEMP*. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia hapa mradi huu Mhe. Waziri ametwambia kwamba umeshamaliza tena anasema kuwa una mafanikio kabisa. Mimi nikiangalia kwa haraka haraka sijayaona bado na nina sababu zangu. Tukiangalia lengo kuu la mradi wa *MACEMP* Mhe. Waziri anatueleza hapa ni kuimarisha matumizi endelevu ya bahari kuu na bahari ya maji madogo, kuimarisha ukusanyaji mapato yatokanayo na uvuvi. Kupunguza athari za uharibifu wa mazingira, kuinua hali ya maisha ya wanajamii wanaoishi katika wilaya zilizo katika ukanda wa pwani. Pia mradi umelenga kuimarisha miundo mbinu na utendaji wa taasisi zinazoelekeza mradi.

Sasa haya Mhe. Mwenyekiti, ndio yale ambayo Mhe. Ismail Jussa amezungumza kwamba walifanya tathmini ya huu mradi baada ya kumalizika kuona kwamba haya yamefikiwa. Haya tukiyatizama kwa haraka haraka sisi hatuwezi kuyaona. Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiria hebu Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwa kina hasa juu ya mradi huu. Maana yake inaonekana mradi umekamilika pesa ni nyingi sana gharama za huu mradi ni zaidi ya dola milioni 60, sio shilingi pesa nyingi sana hizi.

Sasa tukiangalia yale malengo yake mimi kwa haraka haraka kwa haya ambayo ameyaeleza Mhe. Waziri mimi siyaoni kwa haraka haraka, maana yake tukiangalia ni endelevu kwa wavuvi wetu kwamba waweze kwenda kuvua kule kwenye bahari kuu. Sifikirii kwamba kuna wavuvi wanaweza kuvua katika maeneo yale ama ni nyenzo hakuna au vitu gani. Lakini huu mradi kama ulikuwa maudhui yake ni kuwasaidia hao basi mimi naona haujafikia malengo yake.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulikuwa na mambo mengi sana hapa ameyaeleza Mhe. Waziri. Tukiangalia kulikuwa na suala zima la ukusanyaji wa mapato katika huu mradi katika zile sehemu ambazo mradi upo hasa kwenye maeneo ya kule wanaita Ghuba ya Menai, halafu kuna ile nyengine *Peca* na nyengine Mimka.

Katika mgawanyo ule wa mapato zile asilimia 30. Kuna asilimia 30 ambazo huu mradi unaonekana ule ukusanyaji wa yale mapato kutoka katika jumuiya hizi zinakuwa zinapewa zile jumuiya zenyewe. Lakini cha kushangaza mimi

sijui kama kuna jumuiya ambayo inapata hizi fedha nimejaribu kuwauliza wenyewe kule, ukiwauliza wanakwambia kuwa wao hawajawahi kuona kuna kitu kama hicho. Sasa hebu Mhe. Waziri uje utusaidie katika hizi jumuiya vipi. Katika kipindi cha miaka miwili hizi jumuiya kila moja imepata kiasi gani, utusaidie hili ili tuone basi kwamba hizi jumuiya kumbe zinapata fedha mmekusanya kiasi gani na hizi jumuiya mmezigawia kiasi gani, hebu tuletee hesabu angalau ya miaka miwili tuweze kuona namna ambavyo zinafaidika zile jamii husika kule.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, huu mradi mzima ukiutizama una mambo mengi sana, una malengo mengi nikianza kuyapitia moja baada ya moja hapa nitachukua muda wako mwingi sana. Lakini mimi niseme kwa ujumla wake siridhiki na mradi huu namna ulivyoendeshwa. Nina wasi wasi mkubwa wa matumizi mabaya ya fedha hizi.

Sasa hoja yangu hii Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiria waziri atakuja kutusaidia kutueleza kidogo. Lakini sifikirii kama ataweza kupata *datas* zote za yale malengo na namna walivyoyatekeleza akaja akatupa kwa uhakika.

Mimi niombe kama wenzangu waliotutangalia kwamba ni lazima tukubaliane basi kwamba tukafanye uchunguzi kupitia kamati yake Mhe. Mwenyekiti, ile ya Uchunguzi wa Hesabu za Serikiali na Mashirika, tukaufanyie uchunguzi mradi huu namna ulivyofanywa. Kwa sababu fedha hizi Mhe. Mwenyekiti, ni za walipa kodi, hizi fedha ni mkopo mara nyingi na mkopo huu usione labda una muda mrefu au uko vipi, ukinipa mimi nilie hai mimi nikifariki lakini watoto wajuu na virembwe vyetu vitaendelea kulipa haya madeni. Sasa ni lazima sisi ambao tumekaa kwa wakati huu tunaozitumia basi tuwe tumezitumia katika ule mfumo ambao unatakiwa. Tuutumie katika yale makusudio.

Tukiacha Mhe. Mwenyekiti, namna hii kwamba mradi ndio umekwisha na fedha zile zimekwenda lakini matokeo ya mradi ule hatuyaoni. Mimi nasema Mhe. Mwenyekiti, tutakuwa hatuyatendei haki wananchi wetu walipa kodi wetu hawa ni vyema basi mradi huu ukachunguzwe na ripoti yake iletwe Barazani kwa ajili ya kupewa taarifa Wajumbe wengine. Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la *MACEMP,* mimi nafikiri nimalizie hapo.

Nije kwenye suala la ukusanyaji wa mapato kwenye kitabu chake hapa Mhe. Waziri ukurasa wa 53 ametuonesha namna ya mapato yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Aprili, 2013 na mapato yanayotarajiwa kukusanywa. Sasa katika kuangalia Mhe. Mwenyekiti, mimi nina hoja na hoja yangu ni juu ya makusanyo ambayo hayaridhishi kabisa. Sasa nilikuwa nataka kujua sababu, kwa sababu kila idara unayoiona ambayo inakusanya hapa basi

haikufikia yale malengo, wakati ukiangalia katika kitabu chake cha mwaka jana, idara nyingi zilivuka malengo, 150, 130 na kuna nyengine zaidi ya 500 ya malengo yaliyokuwa yamepangwa. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja utupe maelezo ya kina, kwa nini hukufikia malengo ya makusanyo, maana tunapata wasi wasi.

Kwa mfano hapa ada ya utibabu wa vinyama makadirio ni shilingi milioni 12 lakini mmekusanya milioni 6 tu, asilimia kama 50 tu. Sasa ningeomba katika ukurasa wako huu Mhe. Waziri uupitie halafu uje uniletee sababu za kushuka kwa makusanyo haya ambayo ulikuwa umejikadiria kwa nini hukuweza kuyafikia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikimalizia hapo nisogee kwenye mafungu kidogo. Sitaki kwenda mbali sana, niende kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi, fungu 0401, fungu 220701 na fungu 220702 kuhusu matengenezo madogo na matengenezo makubwa. Nilikuwa nahitaji maelezo katika idara hii kwa nini mna hayo kwa sasa wakati nyinyi mnatuambia mmehamia katika jengo jipya juzi. Jengo mmehamia mwaka jana, ingawa mmetuambia limefunguliwa rasmi lakini sisi tunaliona kama lililofungwa, maana mpaka leo lina uzio wa mabati, sijui tatizo ni nini kama ndio kweli limeshafunguliwa rasmi au mlikuwa mnafurahisha tu ili tuwahi sherehe za mapinduzi kufungua. Lakini uzio upo wa mabati kama jengo linajengwa lakini nyinyi wenyewe mnasema mmeshalifungua rasmi. Sasa ule uzio wa mabati wa kazi gani. Mwaka jana tulikuuliza hili, ukasema ni kitu cha mpwito tu, mnamalizia mnaondosha. Lakini mwaka umemaliza huu uzio wa mabati upo, maana mimi nimepita juzi tu kwenda kuhakiki tena nimeukuta. Sasa sijui Mhe. Waziri na wewe ofisi yako imo mule mule au ushahama pale ulikokuweko mwanzo umehamia mule, kama umehamia mule unakaa kwenye jengo ambalo bado linatengenezwa. Sasa mimi nilikuwa nataka maelezo katika idara hii ili kuona kwamba fedha zile ambazo mnaziomba sasa kwa ajili ya matengenezo makubwa na matengenezo madogo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, yako na mafungu mawili matatu, naomba nisichukue muda mwingi niweze kuwapisha na wenzangu waweze kuchangia. Mimi hoja zangu ziko pale pale Mhe. Mwenyekiti, sitoiunga mkono bajeti hii kwa sasa, maana nina hoja ya mwaka jana sikupata majibu, nasubiri majibu yangu yaletwe, yakiletwa na hoja nilizonazo leo hapa basi Minal-faidhina naweza nikaja nikamuunga mkono Mhe. Waziri lakini kwa sasa siwezi kuiunga mkono hotuba hii mpaka pale ambapo nitapata majibu yangu tena ya kuridhisha, nikipata majibu ya kuridhisha sina tatizo Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia saa 6:00 hii kutupa uwezo wa afya na nguvu za kiwili wili kuweza kusimama mbele ya Baraza lako hili kuweza kutoa machache katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi iliyo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi sana kwa sababu inaelekea wizara idara zake ni mbili tu, mambo ya mifugo na uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni miongoni mwa wizara mpya alizozitengeneza Mhe. Rais wa awamu hii ya saba lakini hii wizara bado haijapewa uwezo wa kuwa wizara kama wizara nyengine. Kuna baadhi ya wajumbe waliochangia hapa wakasema kwamba wizara hii ni wizara mama, ni wizara ambayo wana jamii wengi waliitegemea kwa mambo ya mifugo na mambo ya uvuvi, kwa sababu Zanzibar yetu ni sehemu ambayo imezungukwa na mambo hayo mawili. Wananchi wetu wengi wanapenda kufuga na wengi ni wavuvi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nitakwenda kwenye ukurasa 16, kifungu cha 3.3 kinachozungumzia Idara ya Uzalishaji Mifugo. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli serikali ilifanya mafunzo mbali mbali kwa wananchi wetu katika kuwataka wananchi wakae vikundi ili kujiandaa na kuweza kuingia katika miradi hii iliyoletwa na wenzetu wakiwemo watu wa *TASAF*, mpaka watu wa *PADEP* katika ufugaji wa mbuzi, ng'ombe, kuku na kadhalika na wananchi wakaitikia kwa wingi kabisa, suala hili la ufugaji kwa kweli watu walifuga katika maeneo mbali mbali kwa Unguja na Pemba.

Kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti, kwa mafanikio baadhi yao wengi mno hayakuwa mazuri. Moja ni ng'ombe wenyewe walioagiziwa. Tunafikiri kwamba kila ng'ombe aliyekuwa hana nungu basi huyo ni ng'ombe wa maziwa hilo sio kweli. Watalaamu wetu walikuwa wakiwachukua hawa watu wa vikundi kwenda nao kule, kwa sababu mwananchi anayetoka kijijini, yeye hafahamu ni yupi ng'ombe wa mazina na ni yupi aliyekuwa sio wa maziwa. Inawezekana baadhi ya ng'ombe wengi waliochukuliwa ni wale ng'ombe wanaoachiwa tu wakawa wanakwenda malishoni na jioni kurudishwa katika mazizi yao. Kwa hivyo, hawakuleta tija wala faida.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika Jimbo langu la Tumbe wadi ya Shumba Vyamboni, nilipata mradi huu wa *PADEP*, karibuni wananchi wa eneo lile walipata ng'ombe 20 wa *PADEP*, lakini ng'ombe hawa baadhi yao walikuwa sio wa maziwa, walikuwa ni ng'ombe wa kawaida waliokuwa wanaachiliwa huko wakawa wanakwenda malishoni na kurudi mazizini jioni. Lakini watu wakalazimishwa sasa wawajengee mabanda, mabanda yatiwe saruji, ng'ombe wale wasilale ovyo ovyo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ng'ombe aliyezowea kwenda kwenye malisho anayejitegemea, lakini leo unamlazimisha mfugaji hapa amjengee banda, ng'ombe huyo ataelekea wapi, huyo ng'ombe ni kufa tu. Katika ng'ombe 20 hao waliobahatika, bahati nzuri walipata ng'ombe 10 ndio wa maziwa, lakini wale 10 waliobakia ni ng'ombe wa kawaida. Ng'ombe wale walikuwa ni wa Wadi ya Shehia nzima ya Shumba Vyamboni. Waliopewa hawa ng'ombe watu 20 hakuna faida iliyopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, ng'ombe 10 walikufa na vifo vyao vilikuwa vinachangia wakati ule wa kuzaa ng'ombe mwengine. Kwa hivyo, alikuwa anazaa anatangulia kufa ndama mwenye kuzaliwa na hatima yake anafuata mama mwenye kuzaa yule ndama. Katika ng'ombe 10, faida ilipatikana kwa ng'ombe mmoja, ng'ombe 9 wote walikufa wakazikwa, ng'ombe mmoja ndio walibahatika wakapata nyama.

Mhe. Mwenyekiti, ufugaji huu gharama zake kubwa na majani yenyewe ya kulisha na yanapatikana katika maeneo ya mbali mno, utibabu ni wa bei ya juu. Leo hata ile nyama ya yule ng'ombe anapopata yale matatizo akafa haipatikani, hii ni hasara juu ya hasara. Wananchi wengi hivi sasa ukiwashauri kuhusu kufuga huu ufugaji wa ng'ombe basi hawako tayari, kwa sababu kipato hakipatikani. Mtu siku zote anafanyakazi ile ambayo atapata faida, lakini hakuna faida. Kwa hivyo, mimi mara nyingi huwa najiuliza wataalamu wetu wanaofanya hii miradi iwe endelevu, kwa nini miradi hii inapokuja na muda unapomalizika na ile miradi pia inakufa, kwa nini haiwi endelevu. Inaelekea kwamba utaalamu uliopo hauendi na wakati. Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Mwenyekiti, tunapopata miradi kama hii, basi wataalamu waende *deep* zaidi kujifunza ili kuhakikisha miradi imekuwa endelevu. Kinyume na hivi mtakuja kusema Wazanzibari hawataki kazi, lakini kumbe Wazanzibari wanataka kazi, lakini kile cha kufanyia kazi kinakatisha tamaa.

Kwa hivyo, hili ni tatizo Mhe Mwenyekiti, mimi ningewaomba sana ndugu zetu wataalamu wa mifugo walione hili na wanapokwenda huko kutafute hawa wanyama basi wahakikishe wamewachagulia wananchi wetu wanyama wenye sifa, sio wakakokote magombe yashachoka huko wakawaletea wananchi wetu hapa, wakapata kazi na hatima yake wakala hasara, itakuwa hii miradi haiwi endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kuwa na miradi ambayo wananchi hawapati tija. Mradi huu hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, umebakia na ng'ombe 10, katika hao ng'ombe 10 watano tu ndio wa maziwa na watano ni hawa wa kawaida. Ndama waliozalishwa katika ng'ombe hawa 20 wamepata ndama mmoja wa maziwa na waliobakia wote ni madume, faida haikupatikana. Kwa

hivyo, wananchi wamekata tamaa hawana watu wa kuwaelekeza, hawa madaktari wa hawa wanyama pia hawapatikani. Kwa hivyo, wamekata tamaa kabisa, hii sio miradi endelevu ni kuwazidishia wanachama wetu ajira zilizokuwa hazina kipato.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hawa ndugu zetu wataalamu wajaribu sana kuona kwamba ile mbegu inayoletwa hapa inakwenda na wakati na inakubaliana na hali ya hewa ya Zanzibar, sio tukajichukulie hatimaye wananchi wetu tukawapa kazi nzito, halafu kipato tulichokusudia wakipate kikakosekana.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye ukurasa wa 28, sehemu ya Idara ya Mazao Baharini. Mhe. Mwenyekiti, hapa niipongeze serikali kwa kuona kwamba bahari ina mazao mengi na mazao haya ni faida kwa nchi na wananchi wenyewe. Lakini tatizo lililokuwepo ni nini Mhe. Mwenyekiti, ni usimamiaji ndio ambao unasumbua. Kwa kweli usimamiaji wa mazao baharini ni mdogo mno. Mimi huwa najiuliza tatizo ni nini, ajira ndogo. Ukiangalia kwa kweli Zanzibar yote imezungukwa na bahari na kila kijiji kuna wavuvi na hao wavuvi wanahitaji kupata maelekezo kwa watu wenye taaluma.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kuongeza ajira za wataalamu kuwaelimisha hawa wavuvi wetu, ili hizi rasilimali tulizonazo tuweze kuzienzi vizuri na kuzivuna pale ambapo zimefikia wakati wa kuvunwa, ili zisiwe ni zenye kumalizika haraka.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kwa bahari zetu hizi za ndani ndani basi utapata kazi kubwa kumpata yule kaa, utakwenda masafa marefu. Ni kweli kwamba kuna baadhi ya wavuvi wanaharibu mazao, lakini wanahitaji kupewa taaluma na wanapopewa taaluma kwa sababu anajua kwamba anapovua yule anayestahiki kuvuliwa baada ya mwezi tu basi eneo lile lile atakuwa na uwezo wa kuvua samaki wengine. Lakini unapokosa taaluma, basi wewe ni kuchukua tu anayeuzika, anayelika na asiyelika na hatima yake anatupwa ufukweni analiwa na mbwa na wanyama wengine. Kwa hivyo, bahari inaanza kupata umaskini.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana hawa wataalamu wetu wa uvuvi, kujaribu kuwaelekeza wavuvi wetu waliomo katika madago mbali mbali, ili kuinusuri bahari kuingia katika wimbi baya la ukosefu wa rasilimali hizi tulizonazo.

Mhe. Mwenyekiti, sijisifu wala sijidai lakini kwa Zanzibar hii samaki mwenye ladha tamu zaidi basi ni wa Bandari ya Tumbe. Bandari hii

inazalisha samaki watamu sana na wavuvi wako wengi, kwa Pemba nzima basi Tumbe ni bandari ambayo inaingiza wavuvi na wachuuzi na wale watu wengine wanaotafuta kitoeleo kwa Pemba nzima basi utawakuta pale Tumbe. Lakini Mhe. Mwenyekiti, huyu samaki muache avuliwe hata Msuka, basi akifika Tumbe pale basi ladha yake ni ya maajabu kabisa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, usimamizi unakuwa na mavutano mno, maelewano yanakuwa ni madogo na hasa kwa wavuvi wetu hawa wadogo wadogo, kipato chao chao hakiendi na wakati. Kwa hivyo, kama hawa wanaweza kukusanywa pamoja wakapatiwa taaluma na wakapatiwa vyombo ambavyo vinakaribiana na vya hawa wenzetu wanaouza sasa, basi tutapunguza haya malalamiko ya wavuvi wetu pale Tumbe. Lakini hili halipo na halipatikani.

Mhe. Mwenyekiti, tunawaomba sana wataalamu waje waonane na sisi, ili wavuvi wetu wadogo wadogo waweze kupata maslahi kwa sababu wengi wanaitegemea bahari. ili waweze kufaidika na bahari ile.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze tena serikali kwa kuona kwamba Tumbe inastahiki kuwa na soko la samaki, hili ni jambo la maana kweli na serikali ililifanyia kazi, walitafuta mradi na tayari soko pale limejengwa. Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha katika soko lile, kwanza huo mradi wenyewe na hiyo kampuni iliyopewa ovyo. Mhe. Mwenyekiti, hiyo kampuni inaitwa ni Kampuni ya Ngogo.

Mhe. Mwenyekiti, kule kwetu ngogo ni samaki na huyu samaki ana miba mitatu, mmoja upo kichwani hapa, na upande wa kushoto na kulia. Lakini miba hii ina sumu mno Mhe. Mwenyekiti, akikutoga ngogo basi unaweza kupata wazimu, kama hukupata mtu akakufanyia utibabu basi unaweza kupata wazimu ukapoteza akili kwa kiasi fulani. Sasa na ngogo huyu wa kampuni ametutoga watu wa Tumbe, alipewa mradi wa kujenga soko lile.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ndiye aliyeweka jiwe la msingi pale, alitoa hotuba nzuri mno na kuwataka watu wa Tumbe washirikiane na kampuni ile ili lile soko liweze kujengwa pale na hatimaye wapate faida watu wa Tumbe na watu wa maeneo mengine. Mhe. Mwenyekiti, soko limejengwa, lakini kwa taarifa yako soko lile halijaamiwa wala halijafunguliwa, lakini nataka uende ukaone zile mvua zilizonyesha juzi basi solo lote limefanya michirizi, sisi tunaita pweza. Nyumba inayovuja ikitoa michirizi basi sisi tunaita pweza yule, basi soko nzima liko hivyo kwenye maeneo ya nje, jengo halijahamiwa. Lakini pia kimo cha juu ni kifupi mno.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe umebakiza dakika tano.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kimo chake ni kifupi mno haiendi na wakati tulionao, kwa sababu pale unataka kuwakusanya watu na ukiwakusanya watu wanahitaji kupata lile soko liwe na nafasi ya kupita upepo, lakini halina nafasi. Kwa hivyo, kiza kilichomo mule ndani kinasababisha hata ule mnada utakaokuja kufanyika mule iwe watu hawaoni kinachoendelea.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, maeneo ya juu ya dari zake zinavujisha. Makaro yaliyochimbwa kwa ajili ya vyoo, basi yameachana na ardhi. Kwa hivyo, eneo zima la soko halifai, sisi wenyewe watu wa Tumbe tunasema kwa soko lile hatuko tayari nalo, kwa sababu linahatarisha hali ya maisha yetu. Linahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina, kwa sababu zile ni pesa za wananchi zinahitaji kurejeshwa na Wazanzibari wote, lakini jengo halijahamiwa kwa sababu haliendani na wakati wala halifai.

Kwa hivyo, mim ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti kwa kupitia kwako, basi Kamati yako ya PAC ikafanye uchunguzi hapa ili kuzinusuru pesa hizi za wananchi. Pia aliyesababisha jengo lile kufikia vile aweze kuwajibishwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ukiangalia hiki kitabu cha bajeti, kutokana na muda sina tena, kitabu hiki cha Mhe Waziri wa Mifugo na Uvuvi, huko kwenye picha ya mwanzo utamkuta Mhe. Rais, Mkuu wa Mradi wa *TASAF*, Katibu Mkuu, Waziri wa Mifugo na Uvuvi na wengine. Huu ni mfano wa soko lilioko Tumbe, lakini soko hili lipo hapa Mazizini. Hiyo sehemu unayoiona Mhe. Mwenyekiti, ndio sehemu ya mnada na huo weupe uliopo mbele ya Mhe. Waziri hapo ni kikuta cha wavuvi cha kuwekea samaki wao na wale watu wa minada wakaweza kutia minada. Hapo pembeni Mkuu wa Mradi wa *TASAF* anampa taarifa Mhe. Rais, nataka umuangalie Mhe. Rais katika picha hapo, inaelekea maelezo aliyoyapata Mhe. Rais hakufurahika nayo, hana hata tabasamu. Lakini mjumbe mmoja aliyeko kushoto kwako alishikilia kichwa na huku anajikuna kichwa, anasema kwamba ama hapa Rais tunamkanganya.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, huo ndio mfano kama wa soko la Tumbe lilivyo. Kutokana na mfano huu ningewaomba watendaji kile kinachotakiwa kifanywe basi kifanywe kama kilivyo. Mhe. Rais kakosa tabasamu bwana hana furaha, anaona pesa za wananchi nyingi zimepotea na hatimayake soko analolizindua la Mazizini halina muelekeo wa aina yoyote.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana nipate maelezo ya kina kabisa ya soko hili la Tumbe, ya kina yatakayonifurahisha mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe, kinyume na hivyo basi sitounga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Rufai Said Rufai. Sasa anafuatia Mhe Salim Abdalla Hamad na baada ya hapo Mhe. Jaku Hashim Ayoub na ajitayarishe Mhe. Marina Joel Thomas.

Waheshimiwa Wajumbe naomba tujali muda sana, kwa sababu muda unatukimbia kesho tunataka kufanya majumuisho. Kwa hivyo, kila anayekuja atoe *points* kama kutakuwa na *points* mpya, *points* za zamani tena ziachwe sasa hivi. Kama kutakuwa na *ponts* mpya Waheshimiwa naomba zaidi tuzizungumzie hizo, zile ambazo zimezungumzwa tusizirejee rejee, ninaomba sana ili na wengine waweze kupata muda wa kuchangia, nashukuru Mhe. Salim Abdalla Hamad, karibu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitoe shukrani zangu za dhati kwa kupata dakika hizi za majeruhi katika kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa na kwa sababu ya wakati naomba nizungumze kidogo tu pale alipofikia Mhe. Rufai Said Rufai, kuhusu soko la Tumbe, soko ambalo mimi mwenyewe nilikwenda nikaliona. Mhe. Mwenyekiti, soko lile limeshajengwa na azma ya soko ilikuwa lifunguliwe na lianze kazi lakini mpaka leo bado kabisa halijafunguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufuatilia kwangu nimepata taarifa kuwa kuna mtambo mkubwa tu ambao mtambo huu unahusika na kuweka samaki ili wasiharibike katika soko la Tumbe. Lakini mtambo huu tokea kufika hapa Unguja basi haukujulikana ulipo na wala Tumbe haupo. Kwa hivyo, kwa kuongezea pale ambapo Mhe. Mjumbe alipozungumzia, ningeomba kujua mtambo ule uko wapi hivi sasa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa tunachangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Hii wizara ina kazi kubwa sana na ni wizara ambayo inahusika na kuwapatia wananchi chakula bora, ikiwa ni pamoja na nyama, samaki, maziwa, mayai, samli, siagi, mtindi na hata chakula kizuri katika *juice* kinachotokana na mwani na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wizara hii moja kwa moja inahusika na viumbe. Kwa hivyo kuna ulazima kabisa kwa wizara kujua ni kitu gani hasa kinachoendelea katika ufugaji wa viumbe wenyewe. Wizara hii ilikuwa na kitengo chake cha utafiti na imeshafanya kazi kubwa na ilifikia pahala pazuri lakini kwa bahati mbaya katika kitabu kumeelezwa kuwa utafiti huu hautoendelea tena katika wizara hii ya mifugo na uvuvi na badala yake utafiti huu umepelekwa katika Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mimi Mwenyekiti, nataka nijue sababu hasa kwa vile hii wizara ndio inayohusika na ufugaji wa viumbe vya nchi kavu na baharini. Je, ilikuaje wakati ina wataalamu wa kutosha wa kufanya utafiti na wasomi wazuri tu, iwe kazi hii ambayo walikwisha ianza vizuri ihamishiwe katika Wizara ya Kilimo na Maliasili, suala hili naomba nipatiwe jibu ili nijue.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja nianze na mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya mifugo. Suala hili liko katika ukurasa wa 3 na wa 4 wa kitabu na kwa ruhusa yako naomba nisome kama ifuatavyo.

'Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 sekta ya mifugo imeweza kupata mafanikio kadhaa na miongoni mwa mafanikio hayo ni kama yafuatayo.

1. Kuimarika kwa utoaji wa huduma ya uzalishaji na utibabu wa mifugo'.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tukifungua ukurasa wa 41 kwenye jadweli Nam. 4 ambalo linaonesha idadi ya ng'ombe waliopandishwa kiwilaya kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama mtaalamu amewagawa ng'ombe hawa katika visiwa mbali mbali, yaani Unguja na Pemba. Swali la mwanzo kwa nini katika Kisiwa cha Unguja wilaya ni 5 tu zilizofanyiwa shughuli hizo wakati tunajua ni kisiwa chenye wilaya 6 na hapo nataka nipate maelezo. Vile vile tukiangalia katika mwaka huu 2012/2013 kwa kisiwa cha Unguja lengo lilikuwa ni kupandisha kwa njia ya sindano ng'ombe 2,000, lakini waliopandishwa ni ng'ombe 1,079 ni asilimia 53 tu. Kwa hivyo, nataka kujua kwa nini ilikuwa ni 2,000 na ukawa 1,079 kwa nini lengo halikufikiwa.

Halafu kwa upande wa Pemba kulikuwa na lengo la kupandisha ng'ombe 4,000, lakini upandishaji ulikuwa kwa ng'ombe 2,540 mpaka kufikia mwezi wa Machi na hii ni mafanikio ya asilimia 63.50. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuelewa kwa nini lengo halikufikiwa. Mhe. Mwenyekiti, kwa nini Unguja ikawa ng'ombe ni kidogo kuliko kule Pemba ni kwa sababu Pemba kuna wafugaji bora zaidi au vipi pia ninaomba maelezo.

Nikiendelea na mchango sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 42 na hapa kuna kiambatanisho Nam. 5 ambacho kinahusiana na mradi wa upandishaji ng'ombe kwa sindano. Mhe. Mwenyekiti, katika kiambatanisho hichi kwanza mradi huu umeelezwa kuwa utakuwa umeanza mwaka 2010/2011 na unamalizika mwaka 2017/2018 na hicho ni kipindi cha miaka minane. Swali

wakati suala hili ni endelevu kwa nini ikachukuliwa muda wa miaka minane na baada ya miaka minane kuna kitu gani kinachofuatia.

Pia tukiangalia lengo kuu la mradi huu ni kupunguza umaskini kwa kuinua kipato cha wafugaji wadogo wadogo kwa kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wa kienyeji kwa kupandisha madume bora yenye sifa ya uzalishaji wa maziwa na kuzalisha ng'ombe chotara.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu haujaanza leo na tokea miaka ya 1980 kulikuwa na mradi hapa wa kopa ng'ombe ulipe ng'ombe na mambo haya ya upandishaji wa sindano, lakini hatukuona maendeleo ya kupata vizazi ambavyo ni endelevu. Sasa kabla ya kuanza tena huu mradi kwa mujibu ilivyo mwaka 2011 na kuendelea mpaka hapo mwaka 2018. Wizara imejifunza nini kutoka huko tunakotoka kuona kuwa lengo halikupatikana na wamejirekebisha vipi ili waone kwa huko tunakokwenda mafanikio yatapatikana.

Katika upandishaji huu ni ng'ombe wetu wa kienyeji kwa madume bora. Mhe. Mwenyekiti, madume bora ni yale ambayo hayamo katika nchi hii na yanaagizishiwa pale Maruhubi yapo na yanatumiwa kwa ajili ya kueneza mbegu. Mhe. Mwenyekiti, kinachozaliwa ni kitu kipya kutokana na viumbe wawili wenye mazingira tofauti, yaani wale wa asili na wale ambao si wa asili na wale ambao hapa si asili basi wana uasili wa huko kwao na pengine wetu sisi wa asili hakuna. Mwenyezi Mungu anapopeleka viumbe vikawa endelevu ni kuwa viumbe vile tayari vinaweza kuhimizi mazingira kadhaa, vyenginevyo huwa haviwezi kuishi. Kwa hivyo, ikiwa wizara inajishughulisha kutafuta machotara na safari ikawa kubwa wakizaliana hawa machotara basi mwisho itafika asili ile kule ambayo hayo madume bora yanatoka. Lakini je, kutokana na kufeli huku nyuma kama nilivyoeleza na sasa kazi hii tunaendeleza tena. Kwa maana hiyo, sijui tumejipanga vipi miaka ijayo kwa machotara tutakayokuwa nayo kuona kwamba watakuwa na uhakika watakuwa endelevu, yaani watazaana kikawaida na kuishi kwa raha kama wanavyoishi wa asili hapa ili isijeikawa ni hasa hapo baadaye.

Mhe. Mwenyekiti, wakati tunatumia ng'ombe wetu wa kienyeji na hawa mwisho watazeeka na wala hawatazaa tena na baadae watakufa watakuwa na machotara watupu. Je, kama machotara hawakuweza kuishi kama wanavyoishi hawa wa kienyeji itakuwa sisi tumepoteza ng'ombe wetu wengi sana. Je, wizara ina mpango gani wa kuhakikisha hasa kuwa kiasi fulani cha mbegu bora ya asili inabakia na wala haiguswi ili iweze kuendeleza kama tulivyoikutia hapa.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na ukurasa huu wa 43 tutaona kuwa kuna malengo ambayo tutayafanya na malengo haya moja ni kufanyiwa *service* mtambo wa *liquid nitrogen* ambao hivi sasa ndio tunaoutumia kwa shughuli hizi za uwekaji wa mbegu kuzisafirisha na kupandishwa na kupata hizo mbegu tunazozitaka.

Sasa huu mtambo unataka kufanyiwa *service* na hapo zamani tulitoa ushauri wakati tulipokuwepo katika kamati inayoshughulikia wizara hii kutokana na kwamba tuliona kwamba watu waliokuwepo hawakuwa na utaalamu basi tukaomba kuwa mtambo huu wachukuliwe waende wakasome ili likitokezea tatizo lolote basi waweze kuufanyia matengenezo. *(Makofi).*

Je, hao wanaotaka kufanya matengenezo ni Wazanzibari wenyewe wanaofanyakazi kule wizarani au wanakuja wageni kutoka nje kuja kuufanyia matengenezo madogo madogo hiyo *service* na kama ni kutoka nje ni kiasi gani cha fedha kitatumika.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kwenye mradi huu wa kupandisha ng'ombe kama nilivyosema kwamba utachukua muda wa miaka minane na itakapofika mwaka 2018 itakuwa ni basi kwa mujibu wa kitabu kilivyoeleza. Kwa hivyo sisi tunao mtambo wa *liquid nitrogen* ambapo mtambo huu uliagizwa makusudi, ili utusaidie na zamani ilikuwa tunapata tabu sana na ilifika wakati ikawa kazi hayendi kwa sababu ilikuwa hatuna hii *nitrogen.* Sasa ikawa mradi huu ndio basi mtambo huu utafanya kazi gani, kazi ya kutoa *liquid nitrogen* na kuuza au tena hatma yake itakuwa, naomba na hii nipate maelezo.

Katika ukurasa wa 42 kuna shughuli moja muhimu ambayo Mhe. Mwenyekiti, naomba nieleze ni kuhusu malengo ya mwaka 2012/2013 na utekelezaji hali na malengo haya yalikuwa ni malengo ya uzalishaji wa *liquid nitrogen* pamoja na idadi ya ng'ombe ambao walikuwa wapandishwe kwa mwaka huu 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka huu uzalishaji uliokusudiwa ulikuwa uwe lita 3,000 za *liquid nitrogen*, lakini kwa bahati mbaya zilizopatikana ni lita 1,972 na hii ni sawa na asilimia 65 ya makadirio na mapungufu ni asilimia 64.27. Vile vile ng'ombe ambao walikuwa wapandishwe kwa sindano kwa mwaka huu 2012/2013 ni ng'ombe 4,000 na waliopandishwa kwa sindano ni ng'ombe 2,407 ni sawa la asilimia 60.18 ya makadirio. Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba kupatiwa maelekezo.

Pia kuhusu suala la kufanyiwa *service* kwa mtambo huu *liquid nitrogen* ni kwa sababu umeshazeeka na huwezi kutoa tena *liquid nitrogen* kama inavyohitajika au ni sababu gani iliyosababisha hii *liquid nitrogen*

iliyopatikana ikawa ni kidogo na ikasababisha asilimia ndogo ya ng'ombe kupandishwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika 5 zimebakia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kwa hivyo, moja kwa moja tutaendelea na sekta ya uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii kama yanavyooneshwa kwenye ukurasa wa 5 kama ifuatavyo:- Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu kidogo.

Ukurasa wa 5 unaeleza hivi:-

> "Sekta ya uvuvi imezidi kuimarika kutokana na kuongezeka kwa uvuvi wa baharini na pia wananchi wengi wameanza kufuga samaki na mazao mengine ya baharini. Hivi sasa wananchi wengi wameshajihika na wameanza kufuga mazao ya baharini kwenye maeneo yao. Mafanikio makubwa yameweza kupatikana hasa katika Kisiwa cha Pemba".

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio yenyewe ni kama ilivyo kwanza katika mwaka 2011 jumla ya kilo samaki zilizovunwa ni milioni 28,758,997/= na thamani yake ilikuwa ni shilingi bilioni 85,667,819,000.35/=, lakini mwaka wa 2012 kilo za samaki zilizovunwa ni milioni 29,410,544 na fedha zilizopatikana ni shs.103,180,931,590/=. Kwa hivyo, hii ni ziada ya *kilogram* 651,557 na thamani yake ikiwa ni bilioni 17,513,172,565/= na ziada hii ni asilimia 2.3 ya uzalishaji wa kilo za samaki na katika mauzo ni ziada ya kilo 20.4 na haya ni maendeleo mazuri sana na pato la taifa limekua kuanzia asilimia 6.7 mpaka asilimia 7.1.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umebakisha dakika moja.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo kwa sababu ninaunganisha. Sasa tukiangalia Mhe. Mwenyekiti, kuongezeka kwa wingi wa samaki na wanaofugwa na waliovunwa ni kuwa Pemba ilivuna samaki tani 7.733 na Unguja ilivuna samaki tani 2.55 na jumla ikiwa ni tani 9.88 na Pemba ilivuna asilimia 79 na Unguja ni asilimia 21. Kwa upande wa vikundi vinavyofuga samaki 146 Pemba ina 85 na Unguja 61 na huku asilimia 58 na kule 41.

Mhe. Mwenyekiti, nakusudia kusema kutokana na hali ilivyo kwa sababu idadi ya wafugaji hawakupitana sana, lakini huku mazao yamepatikana sana kutoka tani 7.33 ukilinganisha na Unguja tani 2.055. Sasa hapa nataka kujua

ni kwa sababu gani watu wa Unguja hawakushajihishwa vizuri na ufugaji wao hauridhishi au ni kwa sababu Pemba imekuwa na *pressure* zaidi na hapa ninataka nijue kwa sababu ufugaji huu kwa vile unatuletea faida, basi mimi ninataka uende katika haki sawa kwa wote, yaani ongezeko liweko huku na huku.

Mwisho kwa sababu ya wakati Mhe. Mwenyekiti, naomba kuzungumza kuhusu ukulima wa mwani na watu wanalima mwani kwa wingi Unguja na Pemba. Kwa mfano, nilikwenda Tumbe mwani ni mwingi yaani mwani unalala mpaka kwenye nyumba na wala hakukaliki kwa harufu ya mwani. Sasa nataka kujua kwamba watu wale hawaathiriki kiafya kutokana na hali halisi ilivyo na pili wanafanya hivyo kwa sababu ya ukosefu wa bei ambapo bei ni mbaya sana. Kutokana na hali hiyo, ninamuomba Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ashirikiane na Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kama alivyofanya kwenye karafuu akaweza kupandisha bei. Kwa hivyo, na wananchi ambao wanajitahidi sana na ukulima huu wa mwani basi waweze kufaidika ili waondokane na hali ile ya kuweka mwani nyumbani na badala ya kuuza na kupata matarajio ya kuendesha maisha yao. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa anafuatia Mhe. Marina Joel Thomas na baadaye atakuja Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuichangia hotuba hii. Pili napenda kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuandaa bajeti ambayo ni nzuri kabisa. Tatu pongezi kwa serikali kwa jitihada kubwa ambazo wanazifanya kwa wananchi za kuwaletea maendeleo. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nitachangia katika maeneo kama matatu na eneo la kwanza ni Idara ya Sera na Utafiti, pili sekta ya uvuvi na tatu Idara ya Mazao ya Baharini.

Nianze na Idara ya Sera na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, utafiti ni muhimu sana na pia unasaidia kujua hali halisi ya jambo, mafanikio, matatizo pamoja na kusaidia kuweka mikakati ambayo itaweza kupunguza na kuondosha matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi wamehamasika sana katika suala zima la ufugaji kama vile kuku, ng'ombe, mbuzi na kadhalika. Lakini mimi nitazungumzia kuhusu suala zima la soko la kuku na hapa ninalo swali naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba wizara iliwahi kufanya utafiti kujua hali halisi ya soko la ndani. Kwa kweli nasema hivyo kwa sababu tunazo

hoteli nyingi ambazo kila siku zinatumia mifugo hii ya kuku, ng'ombe, jambo ambalo litawasaida wananchi wetu kukuza mifugo yao na ninajua kwenye hoteli hizo mahitaji yapo.

Kwa hivyo, naomba kuishauri wizara Mhe. Mwenyekiti, kwamba iwasaidie wananchi hawa kuwapangia mikakati madhubuti kuona kwamba wanaunganishiwa mpango mzuri na wawekezaji hawa ili bidhaa au mifugo yao ipate kununuliwa. Hali hii itasaidia wananchi wetu kuzidi kujiimarisha wao wenyewe na pia kuimarisha kukuza ajira zao na kuliko kuagiza kuku kutoka nchi za nje jambo ambalo linachangia kuangusha soko letu la ndani. *(Makofi).*

Nikiendele na mchango wangu sasa naomba niende kwenye sekta ya uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa kwamba kuna changamoto mbali mbali na mimi nitazungumzia changamoto mmoja tu ambayo ni uwezo mdogo wa jamii wa kuwekeza katika ufugaji wa mazao ya baharini kutokana na gharama kubwa za uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kabla sijatoa ushauri Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza serikali kwa jitihada inazozifanya kupitia mradi wa *MACEMP*. Mradi huu umefanya kazi nzuri umewapatia nyenzo mbali mbali wavuvi wetu ikiwemo nyavu, boti, mashine na hii imesaidia wananchi wetu kupata ajira pamoja na kunufaika. Vile vile na hapa ninao ushauri Mhe. Mwenyekiti, kwamba wizara izidi kuchukua jitihada za makusudi kwa ajili ya kutafuta wawekezaji wengi zaidi, ili kuwekeza katika sekta hii ya uvuvi na pia hali hii itasaidia vijana wetu kupata ajira na serikali kuingiza pato ambalo litasaidia kuleta maendeleo katika nchi yetu hii. *(Makofi).*

Nikiondoka hapo sasa naomba nizungumzie kuhusu Idara ya Mazao ya Baharini. Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 29 katika utekelezaji wa mwaka 2012/2013 naomba kunukuu kidogo.

Ukurasa wa 29(a) kinaeleza hivi:-

(a) "Jumla ya watu 29 wakiwemo wajasiriamali 23 na wafanyakazi 6 walihudhuria mafunzo juu ya njia bora za ufugaji wa mazao baharini na kilimo cha mwani nchini China.

Aidha mafunzo ya uimarishaji ukulima bora wa zao la mwani na ufugaji wa mazao ya baharini yamefanyika kwa wajasiriamali 154 wa mazao ya baharini

wakiwemo wakulima wa mwani, wafugaji wa samaki, kaa, chaza na majongoo;

(b) … katika utekelezaji huo wameeleza kama kuna jumla ya samaki wadogo wadogo (vifaranga) 10,995 wamesambazwa kwa wafugaji wa samaki Unguja na Pemba;

(c) …vile vile katika ripoti hiyo ya utekelezaji imeendesha mafunzo ya usarifu na matumizi ya mazao ya baharini yametolewa kwa wajasiriamali 100 kutoka katika wilaya zote za Unguja …"

Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba baada ya mafunzo hayo ambayo wameyatoa kwa wajasiriamali mbali mbali. Je, kuna ufuatiliaji kuona kwamba mafunzo hayo yamefanya kazi ipasavyo na baada ya mafunzo hayo kuna mabadiliko yoyote ambayo yametokea katika shughuli zao za wajasiriamali hao.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mwaka 2012/2013 na hotuba pia imeeleza kuongeza kwa wingi wa samaki wanaofugwa ambao jumla ya tani 9,788 za samaki zimevunwa kwa Unguja na Pemba kwa mwaka huu 2012 kutoka kwenye mabwawa ya wananchi. Kwa kweli hii ni hatua nzuri Mhe. Mwenyekiti, na inastahili kupongezwa na katika hili pia ninao ushauri.

Kwa hivyo, wataalamu wafanye ufuatiliaji wa karibu sana ili kuona kwamba wananchi hao wanaofanya kazi hizi za kufuga samaki kwenye hayo mabwawa wanakabiliana na changamoto tofauti. Sasa wataalamu wakifuatilia watajua jinsi gani wananchi hawa wawasaidie kutatua changamoto hizi na pia watasaidia kuboresha shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwenda kwenye *page* ya 20(a)(i) ambapo naomba kunukuu kidogo Mhe. Mwenyekiti.

Ukurasa wa 20(a)(i) kinaeleza hivi:-

"Kwa mwaka 2013/2014 Idara ya Uzalishaji Mifugo inalenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuongeza uzalishaji mifugo na mazao yake kwa kutumia
mikakati ifuatayo:-

(i) Kuimarisha huduma za ugani (elimu kwa wafugaji),

Mhe. Mwenyekiti, suala la elimu kwa wafugaji ni muhimu lakini watakapokutana na wafugaji wawaelimishe wafugaji hawa suala zima la uzururaji wa wanyama katika Mkoa wetu wa Mjini/Magharibi. Kwa kweli suala hili ni sugu kabisa na siku nyengine hata kwenye misafara ya mbali mbali ya viongozi wetu kama vile Mhe. Makamu wa Kwanza na wa Pili na hata Mhe. Rais mwenyewe, na kasoro hizi zinatokea.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka kwenye ziara moja Mhe. Rais alifanya ziara katika Mkoa wetu wa Mjini/Magharibi na ilikuwa Wilaya ya Mjini na lilitokea suala hili. Kutokana na hali hii Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atumie kipengele hichi ambacho anawafundisha wafugaji wake ufugaji bora wa mifugo, pia atumie fursa hiyo kuwaelimisha wale wafugaji suala zima la uzururaji wa wanyama.

Mhe. Mwenyekiti, naona nimemaliza ahsante sana na baada ya hapo naunga mkono hoja. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ninakushukuru. Sasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub bado hajafika aliniomba anakwenda kusali. Kwa hivyo, nakupa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk dakika tano kama ulivyoziomba hazizidi hapo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kidogo nataka nitie baraka katika wizara hii na wala sitokuwa na mengi sana. Kwa kweli suala langu kubwa ambalo limeshazungumzwa isipokuwa mimi nataka nilizungumze kwa upana zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunalo wimbi kubwa na kuingiliwa na kuletewa kuku kutoka nchi za nje ambao kuku hao ni athari kubwa kwa binadamu na tayari athari hizo zinaendelea kuwepo, kwa sababu kuku hao wanalala sana kwenye barafu. Hali hii ya kukaa kwenye barafu kwa muda mrefu, yaani chakula chochote kikikaa kwenye barafu kwa muda mrefu basi kina leta athari kwa binadamu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kwa hili sitomsamehe kabisa kwa sababu kwa namna moja au nyengine wananchi wa Zanzibar wanakosa soko kubwa na wanashindwa kuendeleza kufuga kuku kwa sababu ya uingizaji huo. Kwa mfano, wenzetu Bara wameshapiga hatua na wameshazuia masuala kama hayo na wala hawataki tena kuingiziwa vitu vya aina kama hiyo na kutoa fursa kwa wale wazalendo wenyewe waendelee kufuga vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kifungu cha sera na mipango nitakizuia mpaka anipe jibu tena ni kuzuia kibali moja kwa moja na wala hakuna mas-hara, ndicho hicho kifungu ambacho nimesimama kwa ajili ya kuomba dakika tano kwa hilo tu kwamba tumeshachoka kuletewa maradhi. Kwa mfano, juzi tumeletewa unga mbovu na leo tunaletewa kuku kama hao.

Mhe. Mwenyekiti, naheshimu muda wako na nasema kuwa mimi sitounga mkono kama Mhe. Waziri wakati atakapokuja hapa hatosema kwamba anafuta kibali cha kuleta kuku wanaotoka nje, kwa ajili ya kuwaokoa wananchi wa Zanzibar kupata afya nzuri na kuweza kufuga kuku wenyewe sambamba na hilo kupata ajira kuliko kuletewa kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa tunamkaribisha Mhe. Asaa Othman Hamad na baadaye atafuata Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii ya kuweza kusema machache ndani ya wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, moja ambalo huwa linasikitisha kwamba Baraza lako tukufu linajadili makadirio ya mapato na matumizi ya serikali na hii ndio kazi moja ya chombo hichi. Lakini bahati mbaya mara nyingi serikali huwa haimo humu ndani na masuala ambayo yanaihusu moja kwa moja serikali huwa tunahitaji tupate majibu ya moja kwa moja. Kwa kweli jambo hili kwa kiasi fulani linarudisha nyuma kazi inayofanywa na Baraza hili, hata hivyo tutaendelea kufanya yaliopo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ina umuhimu wa pekee kwa faida na maslahi ya taifa hili kiuchumi. Tatizo linalokabiliwa na wizara kwanza ni bajeti finyu, yaani bajeti haikidhi mahitaji pia haiwezi kuonesha ile dhamira iliyokusudiwa ya wizara hii kwa faida ya wananchi wake, kwa sababu Wizara hii ni ya Mifugo na Uvuvi. Kwa hivyo, tunataka tufuge badala ya kuchunga, tunataka tuvue badala ya kugaragara na mpwa. Mhe. Mwenyekiti, haya hayawezekani kwa fedha hii inayoekwa humu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ng'ombe, mbuzi, kuku na kadhalika kutokana na Zanzibar yetu hii hatuwezi kuendelea kuchunga na lazima tufuge ng'ombe, mbuzi, kuku na jamii yake. Humu si tu kama tutakuwa na lishe bora lakini tutaongeza pato la wafugaji kwa kiwango kikubwa zaidi. Lakini jengine kubwa Mhe. Mwenyekiti, ni namna ya uhifadhi wa mazingira yetu ambalo ni jambo muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, serikali naiomba, hawamo humu ndani wenyewe, yumo Waziri wa Katiba na Sheria na mwenzake wa Uwezeshaji ambaye anahitaji hizo pesa, Waziri wa Ardhi naye ardhi taabani lakini watapeleka hizi salamu.

Mhe. Mwenyekiti, ifike mahali serikali ikubali Wazanzibari kiuchumi wana hali ngumu sana. Kidogo kinachopatikana kiweze kutumika kwa wote na kwa faida ya wote. Hali inavyokwenda sasa hivi ya serikali kubeza kila kile tunachokisema sisi kwenye chombo hiki na kwamwe kukataa kuchukua hatua dhidi ya wale wanaofuja kwa makusudi hicho kidogo kinachopatikana, hali hii inatilisha unyonge. Ni unyonge wa watu wetu, ni unyonge wa taifa hili, badala yake ni kubaki kuomba omba.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto zilizokuwepo kwenye mifugo tunahitaji fedha ili hayo ninayoyasema yaweze kufuatiliwa, wawe na vyombo vya kufuatilia, wawe wanapata mitaji ya ufugaji, taasisi za fedha zitoe mikopo nafuu. Mhe. Mwenyekiti, kule vijijini waweze kutumia nishati mbadala badala ya umeme huu haufiki. Umeme nchi hii si kwamba umechukuliwa kama vile ni lakshari si huduma, wanyonge hawa hawawezi kuulipa umeme. Ndani ya umeme alipe *VAT* ndani ya umeme sijui kuna *service charge* haijulikani inatokea wapi. Lakini utakapompa ng'ombe wawili hawa wa kisasa yaliyobaki haya yote atayapata kwenye nyumba, matumizi ya umeme *bio gas* atatumia, lakini pia atapata na mbolea, lishe hiyo tunayoihitaji.

Madhumuni mengine makubwa Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa na mifugo hii na kilimo hichi kiende sambamba na suala la utalii. Hali ya hivi sasa ndio kelele zinakuja tunaletewa kuku kutoka nje, tunaagiza na maboga kutoka nje, keroti kutoka nje, hivi tujiulize tunafanya nini? Kama serikali haijakuwa tayari katika hili utalii wetu bado utadorora. Utalii kwa wote Zanzibar itakuwa ni hadithi tena ile ya alinacha. Hatutoweza kamwe kuwafanya wafugaji wetu na wakulima kwenda sambamba na utalii tunaouzungumza.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye uvuvi, nimesema tuondokane na mgaragara napwa tuvue. Tutavuaje kama wavuvi wetu hawatoweza kuingia kina cha maji marefu. Wizara Mhe. Mwenyekiti, imejipanga mwaka kesho au mwaka huu wa fedha itapata boti. Boti hii itachukua vijana idadi labda ya thalathini hivi, watakapomaliza mafunzo uvuaji wa huko bahari kuu chengine kinachofuata ni kipi. Wachukuliwe wengine thalathini mzunguuko wa namna hiyo. lakini hakuna tena, hakuna mipango ya wale waliopata mafunzo kwamba sasa waende wakavue. Watakaa juu watakwenda tena Darajani, wakenda Darajani Dokta Mwinyi hakubali, bado tatizo la maisha vijana linakuwa ni gumu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kama ninavyoendelea kusema, kama kuna bomu linafugwa nchi hii ni kukosa ajira kwa vijana. Mwenyekiti, vijana wanateketea, wanateketea ajira hawana, wanajichanganya kwa madawa ya kulevya njaa balaa jengine. Mhe. Mwenyekiti, hili jukumu tutalibeba sisi. Tutalibeba sisi kama hii serikali iliyokuwa haitaki kusikia hii hatukuidhibiti sisi, jukumu hilo ni Baraza hili. Serikali inabeza, haya tunayoyazungumza humu ndani kwa sababu hiyo sasa imekuwa ni tatizo, haiwezekani. Tumeleta hapa maboti wizara hii hii, yakagaiwa ki-mjomba mjomba na hivyo hivyo. Matokeo yake hakuna kilichokuwa. Hali ipo pale pale, maboti hayakuleta tija, baadae wale waliopewa wakaonekana labda watakidhi hiyo haja na wao wakayakodisha huko walikoyakodisha mengine yakapotelea mbali.

Uvuvi wa bahari Kuu si kukusanya leseni, hapa hatujafanya tulichokikusudia. Mhe. Mwenyekiti, leseni zinazotolewa halali na leseni zinazotolewa haramu. Mhe. Mwenyekiti, hii ni wizara yangu ya asili na pia nimepewa kwenye hii Kamati, naipenda sana. Lakini leo nitamuomba Mhe. Waziri anipe maelezo ya kina ili turidhike na Wazanzibari hawa wanyonge wanaoteseka kwa shida, pesa hizi zinazochezewa namna hii na mtu au kikundi cha watu.

Mhe. Mwenyekiti, inakuwakuwaje mtu anathubutu kutoa leseni feki akaipa meli ya kigeni kuvua. Lakini ni kwa sababu kaona kwa wenzake, wanaofanya maovu kama hayo ndani ya serikali hawaulizwi. Kwa nini na yeye asifanye. Hali ya namna hii Mhe. Mwenyekiti, serikali itatufikisha mahali tuwatake wananchi sasa wasimame wenyewe kudai haki yao, kwa sababu Wawakilishi wao serikali haitaki kutusikiliza. Sasa tukijumuika na wao tukakae kwa Makamu wa Pili wa Rais pale mpaka atujibu yote tunayodai ndani ya serikali, itafika siku tutafanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakisha dakika 5.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Dakika tano zilizobaki utwambie ni meli ngapi, ni leseni ngapi feki wizara yako imetoa, zenye thamani ya kiasi gani, tumepata hasara kiasi gani na tungefaidika fedha hizo kama zingetoka kihalali kiasi gani. Na ni hatua zipi serikali imekusudia kumchukulia, mumtaje angalau tumsikie sisi kwanza humu ndani kutoka kwenye Wizara yenyewe lakini kama wizara hii bado ni ile ile *theory* ya serikali kuhifadhiana. Ya nini kufunikana, Kiswahili sahihi labda sijakipata lakini tunachotaka hawa watu watajwe kwanza hadharani angalau itakuwa adhabu nambari moja, vyenginevyo Mhe. Waziri nakuonea tabu sana kwa sababu mimi nataka ipite hii bajeti lakini nitakuwa napitisha haramu ndiyo tatizo liliopo. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niipitishe kwa asilimia 100 lakini imeingia dosari, nitakataa kufanya hivyo mpaka nipate jibu la leseni sasa.

Mhe. Mwenyekiti, majumba yaliyochukuliwa na watu wasiostahiki wa wizara hii, Mhe. Waziri tunataka utupe kinaga-ubaga wizara imefikia wapi katika hili. Lakini jengine ni maeneo yaliyovamiwa Kisakasaka na Tunguu, hatua za wizara zimefikia wapi. Kisakasaka, Tunguu watu wanagawana Mhe. Mwenyekiti, kama vile Juja wa Maajuja keshafika ni hatari kubwa sana hii. Shamba ni kwa ajili ya mifugo, wameingia binadamu na akili zao tena wenye akili na wenye dhamana ya kuongoza nchi wanagawana kama nzige. Mhe. Waziri hebu twambie ni akina nani waliojigawia na wewe mwenyewe unachukua hatua ipi, tusikie angalau hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie sekunde kumi. Fedha nyingi za mkopo *MACEMP* kuna mazuri mengi yaliyofanywa lakini tunamalizia mabaya. Soko hili Mhe. Mwenyekiti, hebu atwambie Mhe. Waziri ameshakabidhiwa na kweli amaridhika kulipokea namna ile ya soko lilivyo na kama bado ana dhamira ya kulipokea katika hali ile au kuna maelezo mengine atakayotupa. Kwa sababu sisi na mimi kama ni mjumbe wa kamati, ishara ya ubadhirifu na ubovu na maovu katika ujenzi ule, sijui kapewa ngogo, sijui samaki, sijui kitu gani tuliliona mapema na tukatahadharisha. Sasa kama wizara ilichukua hatua ni vyema, kama ilibeza hili hatutokubaliana nalo.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii Mhe. Waziri nina nia njema kabisa na wizara yako lakini nataka maelezo kwa yale maeneo niliyoyahoji, sijapata hivyo nakamata mshahara mpaka nipate jibu sahihi na nataka niridhike na maelezo utakayotoa kwa sababu mambo mengine tunayo tunayafahamu, yamo ndani ya mifuko yetu. Baada ya kusema hayo nakutakia mafanikio mema na majibu mazuri. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimshukuru Mhe. Rais kwa uteuzi wake alioufanya katika Wizara pekee inayoongozwa na vijana ikiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wote wa wizara hii. Lakini cha kusikitisha bajeti ya wizara hii ni ndogo, hawa vijana hawatoonekana vizuri utendaji wao. Bajeti ya wizara hii ni ndogo, vijana mimi naamini bado damu inawachemka na ni watendaji wazuri. Waziri mimi namuamini, Naibu Waziri ndio kabisa haisemeki, Katibu Mkuu bado kijana.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kupoteza muda kama nilivyosema nichangie katika ukurasa wa 28 kwa haraka haraka Idara ya Mazao Baharini. Niwapongeze sana wakulima wa zao la mwani kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa ukizingatia wananchi wa jimbo la Muyuni wanafanya kazi katika mazingira magumu, vitendea kazi hawana. Suala hili tumekuwa tukilipigia kelele kila siku Barazani lakini uwajibikaji hauonekani. Mhe. Mwenyekiti, suala hili nalichangia kwa uchungu mkubwa na kwa hisia tofauti kwa sababu limegusa kila sehemu ya mwananchi, suala hili lipo kwenye kifungu cha (c) ukurasa wa

28. Kuhamasisha usarifu na matumizi ya mazao baharini na ukuzaji wa soko ndani na nje.

Mhe. Mwenyekiti, hapa panasikitisha sana kwa bahati mbaya sijui Zanzibar tunarogwa na nani na mchawi sijui nani. Wana sayansi wamekuja na wakafanya utafiti kuhusu mwani unaota kima kikubwa cha maji. Ripoti zimekamilika na kila kitu lakini kwa bahati mbaya sijui tuseme nini, kilichofanyika kipi watu wanazidi kuteseka. Kubainika mwani katika kima kirefu cha maji una uwezo Zanzibar kulimwa na unaota, ukilinganisha na mwani wa kutumia vijiti na kupanda kwenye vijiti. Ukizingatia mwani wa vijiti mazingira yake si mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiwa nipo hapo hapo sehemu ya baharini Zanzibar kuna kitengo hichi nafikiri kinaitwa *International Service Zanzibar* kwa kufadhiliwa na mradi wa Benki ya Dunia. Mwani unaolimwa katika kina kirefu cha maji kina faida mbili kubwa. Kwanza bei yake ni nzuri. Pili unasaidia hifadhi ya mazingira ukilinganisha na kilimo cha kutumia vijiti. Lakini cha kusikitisha hadi hii leo kilimo cha chanja kimeshindikana kwa sababu ya mambo mawili tu. Serikali kushindwa kuweka mipaka ya wakulima wa mwani na wavuvi. Katika hili nitahitaji maelezo suala hili nimepiga kelele sana katika kipindi cha maswali na majibu karibu siku zote.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili hili wana sayansi wamefanya kazi kubwa sana, wameweza kugundua kwamba unga wa mwani una soko kubwa na bei nzuri kuliko kuuza mwani mkavu katika soko la ndani na nje. Mheshimiwa kilo ya mwani inauzwa Sh. 400/- wakati kilo ya unga ya mwani inauzwa Sh. 10,000/-. Watendaji wetu Mawaziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu hili suala mlichukulie kuwa mwani karibu unauzwa shilingi elfu kumi wa unga na faida ya unga huu wa mwani tunapata dawa na hata keki zinatengenezewa. Mhe. Mwenyekiti, kama tumeshindwa kutumia mashirika yetu ya viwanda vidogo vidogo vya Tanzania Bara (*SIDO*) sijui utafanya nini, hatuwezi kufika kwa mambo kama haya, wananchi wetu wanazidi kuteseka. Mimi kuna wananchi wangu wa Jambiani mwani wao karibu wote umeharibika na sijui serikali itawasaidia nini kuhusu hili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba kuchangia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, ukurasa wa 25. Idara hii ni muhimu sana bahati mbaya sikio la kufa halisikii dawa Mhe. Mwenyekiti. Utamaduni tunaokwenda nao na serikali kutoa fedha miradi baadaye inapofadhiliwa na wahisani, Serikali haibebi na anayebebwa hujikaza. Hivi sasa mheshimiwa mradi unapomaliza muda wake kitengo hiki hakitosaidia kuharakisha maendeleo ya Zanzibar. Msije mkasema mimi Mhe. Mwenyekiti, haya maneno yapo ndani ya kitabu hiki, hakiwezi

kusema na mimi ndio ninavyosemea, ushahidi kamili tuangalie kiambatisho Nam 9.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwa sababu hiyo ukiwemo mradi wa kuhifadhi mazingira katika ukanda wa pwani *MACEMP* tumemaliza muda wake mwaka huu chini ya udhamini wa Benki ya Dunia. Mwaka huu serikali ilitakiwa kuchangia shilingi milioni mia ili kuendeleza kazi za mradi huo. Bahati mbaya serikali ilichangia asilimia 30 jambo ambalo ni la kusikitisha na la kutia unyonge mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, serikali ikitaka jambo lake haishindwi, hapa kitabu juzi tulikimaliza cha Wizara ya Habari, Utalii na Michezo, ukurasa wa 13, gharama za mradi huu ni shilingi milioni nne ambazo hadi sasa kufika Juni, 2013 jumla ya shilingi milioni ziliingizwa kwa asilimia 100. Kwa hivyo serikali ikitaka jambo lake Mhe. Mwenyekiti, haishindwi. Hawa vijana wetu tutazidi kuwalaumu tu. Ushahidi huu hapa Mheshimiwa juzi tu tumesoma hiki kitabu.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo nije mradi wa jimboni kwangu, huu ni mwaka watatu siwezi kulaumu Waziri aliyepita Mhe. Ramadhani Abdalla Shaabani kuhusu boti ya wavuvi wa Muyuni. Boti hii imeleta kizungumkuti kwa ufupi. Nimshukuru Mhe. Waziri aliitisha kikao mimi akanijumuisha katika kikao hicho lakini cha kusikitisha hakuna hatua iliyochukuliwa, akaja Mhe. Naibu Waziri naye nimshukuru sana kwa jitihada alizochukua, akaitisha kikao nitakuwa si mwingi wa fadhili na sikumtendea haki kwa jitihada alizochukua kama sikumshukuru. Wananchi wa Muyuni bado wana malalamiko na mimi ndio walioniajiri na ndio nitakaendelea kuwatumikia, vyenginevyo vyovyote nitakuwa sijawatendea haki. Niliambiwa kuwa nitatafutiwa boti nyengine tuwapelekee wananchi wa Muyuni lakini bado mpaka hii leo hakuna kinachoendelea.

Kama haitoshi hapo Mhe. Mwenyekiti, vijiji vya Muyuni/Jambiani, Mfumbwi hivi sasa wanawake hao ni kikundi cha ushirika wanakodi boti wanakwenda kutafuta mwani. Mhe. Waziri ningekuomba sana wananchi hawa wakapata kusaidiwa. Mhe. Mwenyekiti, kuna hizi nyumba za Wizara za Uvuvi. Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze ni nyumba ngapi, maana kuna taarifa kwamba hizi nyumba wanakaa wananchi tu hivi sasa. Kuna mradi umetolewa kuhusu ng'ombe wa maziwa na mbuzi wa maziwa, sijui wananchi wananufaika vipi na mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha chengine sisi eneo kubwa tunalo la bahari, tumezunguukwa na bahari tofauti. Wenzetu wa Mwanza wamezunguukwa na ziwa tu lakini wana viwanda vya samaki. Mhe. Mwenyekiti mpaka hii leo

Zanzibar tunashindwa hata kutengeneza viwanda vya kusindikia samaki, ni jambo la kusikitisha sana na hapa nitahitaji maelezo.

Baada ya mchango huo Mhe. Mwenyekiti, mimi sitounga mkono hoja mpaka Mhe. Waziri atakapokuja kuniridhisha na hoja hizi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii Mwenyezi Mungu akubariki akupe kila la kheri akuondoshee kila la shari. Baada ya dua hiyo sasa nije kwenye hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Mhe. Abdillahi Jihadi Hassan).

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii jukumu lake kubwa ni kusimamia maendeleo ya mifugo na maendeleo ya uvuvi ambapo asilimia kubwa ya wananchi wa Zanzibar hasa wale wenye kipato cha chini shughuli hizi ndio shughuli zao za ufugaji pamoja na uvuvi. Ninachotaka kusema kwamba wizara hii ina jukumu kubwa sana lakini bado haijaonesha mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa nikikipitia kitabu hiki cha hotuba cha Mhe. Waziri sijaona mafanikio katika maeneo haya yote mawili au ile *seriousness* ya serikali juu ya maeneo haya. Maeneo haya kama serikali itayashughulikia ipasavyo basi mapato au wananchi wale hasa wenye kipato cha chini mapato yao yangeongezeka kwa kiasi kikubwa. Lakini haya maendeleo yenyewe ambayo yametajwa humu ya mifugo na uvuvi inabakia jina tu lakini hakuna kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametueleza humu mafanikio lakini ametuelezea na baadhi ya changamoto katika sekta hizi mbili, ambapo katika eneo la sekta ya mifugo ametuelezea kuna mambo hapa lakini anasema kuimarika kwa utoaji wa huduma za uzalishaji na utabibu wa mifugo. Mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri ana madaktari wangapi wa mifugo katika Wizara yake. Hili nilikuwa nataka kujua.

Lakini katika changamoto ambayo moja ameieleza hapa amesema ni maradhi ya mifugo na upungufu wa vifaa vya kudhibiti maradhi hayo. Nayo nilitaka kujua vipungufu vya kudhibiti maradhi hayo ni nini na nini. Eneo jengine ni bajeti ndogo ya sekta ya mifugo. Hili nakubaliana nalo kwamba bado bajeti ya mifugo inaonekana ni ndogo. Ndio lile nililolizungumza mwanzo kwamba *seriousness* inaonekana bado katika serikali juu ya maeneo haya haijaipa kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili la mifugo nilikuwa nataka Mhe. Waziri anipe maelezo atakapokuja kufanya majumuisho anipe maelezo ya kina ili

niridhike. Wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na kidogo Wizara ya Uwezeshaji, walikusanya fedha za wajasiriamali wa Mkoa wa Kusini Unguja na fedha hizo zilizokusanywa zilikuwa na lengo la kutoa elimu kwa wajasiriamali wale, juu ya suala la kuwapatia ng'ombe wa kisasa pamoja na kuku, kwa mama mmoja kutoka Tanzania Bara kwa kushirikiana na wizara hizi. Alikuja na akatoa mafunzo hayo na akakusanya fedha kiasi cha wajasiriamali 300 ambapo kila mmoja wao alitoa karibu shilingi laki tatu. Lakini hadi leo mama yule anaonekana kaingia mitini. Sasa sijui kama wajasiriamali hawa tunawasaidia au tunazidi kuwatia unyonge. Cha kusikitisha zaidi kuna baadhi ya wajasiriamali wale waliuza ng'ombe wao wa kienyeji kwa lengo la kupata ng'ombe hao wa kisasa.

Sasa nataka maelezo juu ya jambo hili ili niweze kukupitishia bajeti yako lakini isitoshe walitoa fedha kwa ajili ya kununua kuku, kuku wameletwa lakini kuku wenyewe badala ya kuletwa, wameletwa vijogoo. Sasa kweli jambo kama hili sisi Wawakilishi wa wananchi hatuwezi tukalifumbia macho, tukalinyamazia kimya, kuona wananchi wanyonge kwa kushirikiana na taasisi hizi za serikali na watu wengine kuona fedha zao zinachukuliwa na hakuna jambo lolote ambalo linaeleweka. Kwa hivyo nahitaji maelezo Mhe. Waziri.

Eneo jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo limezungumzwa sana na wenzangu hapa ni juu ya kuku hawa wanaoletwa kutoka nje. Wengine wanaitwa makuku kutokana na ukubwa au kutokana na ubovu wao. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefanya utafiti au nimefanya *follow up* ukisema utafiti labda ni wa kitaalamu, juu ya mahitaji ya kuku. Kama tunavyojua sisi tupo katika sekta ya utalii. Sekta ya Utalii ina mahitaji mengi, ikiwemo kuku, samaki, mbogamboga na mambo mengine. Lakini takriban ukiachilia mbali mahitaji ya hawa samaki lakini mahitaji ya mboga mboga na mahitaji ya hawa kuku kwa kiasi fulani asilimia kubwa inatoka nje ambako ni Tanzania Bara ama kuku wanaotoka nje hawa ambao wanaoletwa.

Mhe. Mwenyekiti, mahitaji halisi niwambie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mwezi ni karibu tani 585, mahitaji yetu halisi. Uzalishaji wetu ni tani 163 tu. Lakini katika hao kuku ambao wanakuja kutoka nje tunaolalamikia ni tani 54 peke yake. Ukiangalia takwimu utaona kwamba kuna nakisi ya karibu tani 369. Hebu tuangalie hali halisi ya uzalishaji wetu na mahitaji ya soko hasa katika maeneo ya utalii. Utaona ni dhahiri kwamba bado wafugaji wetu hawajaweza kutosheleza soko.

Mhe. Mwenyekiti, watalii kutoka nje hawapendi kula kuku wetu hawa tunaozalisha hapa hasa hawa wa kisasa na kwa sababu wanasema kuku wale tunaozalisha sisi hapa wana harufu ya uvundo kutokana na vyakula vile wanavyokula vya dagaa. Kwa hivyo watalii hawapendi kula kuku hawa wana

harufu kwa lugha nyengine na wanapendelea kuku wale wanaotoka nje ambao sisi tunapiga vita wasiingizwe nchini ambao kuku wale wa nje wao hutumia chakula chao cha soya, kwa hivyo ana harufu nzuri na wenyewe wanawapenda.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, lazima tukubaliane tuendane na hali tumekubali soko la utalii katika nchi yetu, kwa hivyo tukubali na mazingira ya utalii nchini. Kiwango cha kuku kinachoingizwa hapa si kikubwa kiasi hicho na zaidi ukitilia maanani kwamba kuku wetu hawa wageni hawawapendi. Lakini hata hawa kuku wa kienyeji tunaosema hapa hebu tuangalie ni wananchi wangapi wanyonge wenye uwezo wa kununua kuku. Kuku wetu kwa vyovyote vile tujue kwamba ni ghali lakini kuku hawa wanaotoka nje bei yake ni nafuu. Siku hizi Mhe. Mwenyekiti, kila Mzanzibari ana uwezo wa kula kuku, akipata mapaja yake nono mawili tayari kishapata kitoweo, samaki hawanunuliki lakini wananchi wanyonge wana uwezo wa kula kuku. Kuku zamani Mhe. Mwenyekiti, walikuwa wanaliwa siku kuu hadi siku kuu, lakini siku hizi kwenye majumba ya kawaida kila nyumba unayokwenda watu wanakula kuku bukheri wa hamsa ishirini.

Kwa hivyo mimi hoja za Waheshimiwa Wajumbe za kutaka kuku hawa wasiingizwe nchini napingana nazo sikubaliani nazo, bado kuku kutoka nje waletwe ili wananchi wanufaike na kuku hawa kwa sababu ni nafuu kuliko wale kuku tunaozalisha humu na isitoshe kiwango kinachoingizwa hapa bado hakijatosheleza soko la Zanzibar, kuna jinsi ya tani karibu 369 zinahitajika hapa kwa ajili ya mahitaji ya hapa. Kwa hivyo tunapojenga hoja Waheshimiwa Wajumbe kwanza tufanye *follow up* juu ya jambo hili. Uwezo wa kuzalisha kuku hawa wafugaji wetu ni mdogo hawawezi kutosheleza, leo hata tutazuia kuku hawa wanaotoka Brazil na Marekani wanaokuja hapa wenye mahoteli watalazimika kununua kuku aina hii Tanzania Bara kwa sababu lazima watalii wapate kuku aina hii.

Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, lazima tulifanyie utafiti wa kina na tuone mahitaji. Mimi nakubaliana na kuingizwa kuku hawa hapa Zanzibar na kwa sababu bado hawajaua soko kama tunavyozungumza, tatizo kuku wetu hawa wa kienyeji wanaozalishwa hapa wanauzwa ghali, wananchi wanyonge hawawezi kununua kuku wale. Lakini na mtu aliyekuwa hawapendi kuku wale kwani analazimishwa kununua? si kama ana fedha zake ende pale marikiti tu akanunue hao kuku wa kienyeji, anayetaka atakwenda kununua kienyeji aliyekuwa uwezo wake mdogo atakwenda kununua paja nono, kuna tatizo gani maadam uwezo wake mdogo atakula na watoto wake. Alimradi kuku hawa wanaoingizwa hapa vyombo vile vya Tume ile ya udhibiti wa maradhi ile ya Hospitali ya Mnazi Mmoja basi ifanye kazi kuona kwamba wale kuku wanaoingizwa hapa hawaleti madhara kwa wananchi.

Si kweli kwamba kuku wote wanaotoka nje ni wabovu wana madhara. Sisi tunapokwenda nje kutembea Ulaya wote tunakula siku zote tunazokaa huko tunakula kuku hawa hawa, kuna kuku wa kienyeji tunaokula kule. Mtu aliyekuwa hawapendi asile tu si basi, lakini wale wenye uwezo wa kutaka kununua wache wanunue wananchi wanyonge waweze kula kuku na waweze kufaidika kuku. Kwa hivyo mimi sikubaliani na hoja ya Waheshimiwa Wajumbe kwamba Waziri apige marufuku uingizaji wa kuku ule ilhali uzalishaji wa kuku ni kidogo sikubaliani nalo. Mhe. Mwenyekiti, duniani kote bei ya kitoweo cha kuku inatakiwa iwe ya nafuu bei ya chini dunia yote. Hapa unakwenda marikiti kikuku kidogo kile unakwenda unaambiwa elfu kumi, mwananchi mnyonge atawezaje kula kuku Mhe. Mwenyekiti, *definitely* hana uwezo wa kununua kuku, tuwaachie wananchi wetu wafaidie na paja nono ni almradi tu vyombo vile vinavyohitajika basi tuangalie na kama watakuwa katika hali nzuri basi wananchi waruhusiwe wafaidike na kuku hawa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mradi wa *MACEMP* ni mradi ambao umefanya kazi vizuri na umepiga hatua kubwa na umefanya shughuli nyingi, lazima hilo tukubaliane na umepiga hatua kubwa na kwa bahati nzuri kamati yangu iliyokuwa inasimamia wakati huo wakati huo hakujawa na mabadiliko umepiga hatua kubwa wananchi wetu wamefaidika sana na mradi huu. Lakini kinachosikitisha kwamba mradi huu baada kukamilika serikali haijaweza kutenga fungu kwa ajili ya kuuendeleza. Humu tu inasema mradi kwamba huu umefikia mwisho lakini mradi huu unahitaji kuendelezwa, unahitaji kwa sababu ni mradi endelevu yale mazuri ambayo tuliyoyaanzisha wakati ule yanahitaji kuendelezwa, wenzetu hawa wanapotupa misaada ama mikopo kwa ajili ya kujiendeleza lengo lao tuianzishe ile miradi halafu tuiendeleze.

Lakini inasikitisha Mhe. Mwenyekiti, kwamba mradi huu haukutengewa hata shilingi safari hii, sembuse mwaka jana umetengewa milioni mia moja wakapata milioni thalathini, mwaka huu imesahauliwa kabisa. Hivi lengo la serikali katika mradi huu uliogharimu mamilioni mengi lengo lake nini? Maana yake uishe hivi hivi. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja uje utueleze kwa nini hukutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi huu katika yale maeneo mbali mbali ambayo miradi ile ilikuwa imeanzishwa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, la mwisho nisile muda wako mwingi ni suala hili la uvuvi wa bahari kuu. Suala la uvuvi wa bahari kuu linasikitisha, Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ametujaalia bahari wenzetu Bara wana madini, dhahabu, almasi, *Tanzanite.* Sasa hivi tunasikia wameshaanza kuwa na *uranium* na mambo mengine. Sisi Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu katujaalia tumezungukwa na bahari ndio raslimali ya wananchi wetu lakini raslimali hii ya bahari kuu hatuitumii vizuri, bado serikali haijaonesha juhudi ya kutumia bahari kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Zanzibar. Kama

hatutoitumia bahari kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu kila wakati tutakuwa tunapigishana kelele, kila siku tunapigishana kelele kwamba tunataka fedha zetu hizi huyu apewe hiki, kwa sababu tayari hatuna lile eneo ambalo linazalisha mali. Wenzetu wa Srilanka ni kisiwa kama sisi kinaitumia bahari kwa maendeleo ya wananchi wake. Sasa hivi pato la mwananchi wa Srilanka sasa hivi ni dola elfu kumi kwa mwezi ni kiwango kikubwa. Sisi hatutumii uvuvi wa bahari kuu kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu inasikitisha sana.

Ukiangalia kitabu cha Mhe. Waziri kinasema, 'Mradi wa kuimarisha uvuvi wa bahari kuu umepatiwa shilingi milioni tisa ambazo ni sawa na asilimia tatu ya makadirio, kuna fedha zilikuwa zimetengwa karibu milioni mia nne lakini zimepatikana milioni tisa ambazo ni asilimia 3 ya makadirio ya mwendelezo wa uvuvi wa bahari kuu'. Hii inaonesha dhahiri ni jinsi gani tulivyokuwa hatuko *serious* katika maeneo haya. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba muda wako mdogo, tuna mengi ya kuchangia katika Wizara hii ya Mhe. Waziri lakini bado *seriousness* ya serikali katika maeneo haya mawili, maeneo ya mifugo, maeneo ya uvuvi inaonekana bado ni dhaifu na kwa kweli serikali inatakiwa iweke nguvu katika maeneo haya kwa ajili ya kupata maendeleo ya watu wetu.

Naunga mkono hoja kwa asilimia 50.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru sana kunipatia nafasi hii na nichukue nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, kumpongeza sana Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake kwa jinsi ambavyo wametuletea kitabu kifupi sana lakini chenye takwimu ambazo zimejitosheleza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kuunga mkono ile hoja ya Mhe. Salmin kwamba mimi sili kuku wa paja nono siwapendi na siwapendi kwa sababu ya ninavyowaona mwenyewe, lakini naunga mkono kwamba serikali isije ikathubutu kuwazuia kuku wale. Cha msingi ni kwamba serikali ijipange, ijizatiti kulinda usalama wa Wazanzibari juu ya kuku wale lakini kama mtu hawapendi kama mimi basi si sababu ya kupiga marufuku. Maana wengine hawapendi mbuzi, wengine hawapendi kondoo, wengine hawapendi ng'ombe lakini ni mtu mmoja mmoja. Lakini hoja ya kuwapiga marufuku kuku wale kwa sababu kwamba mtu hawapendi nadhani si hoja ya msingi, serikali ijipange kudhibiti matumizi mazuri wa kuku wale na usalama wa wananchi wetu ili kuwalinda na maradhi ambayo yanasababishwa na bidhaa ile kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo naunga mkono hoja ya Mhe. Salmin kwamba kuku paja nono kwamba wasipigwe marufuku lakini serikali iwalinde wananchi wake kwa usalama kwa maana kwamba idhibiti matumizi ya kuku wale wanapoingia wawe wamekaguliwa na kwamba afya ya Wazanzibari wetu iwe katika hali ya usalama.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ambayo nataka nichangie katika kitabu cha Mhe. Waziri ukurasa wa 4 amezungumza changamoto za sekta ya uvuvi na moja katika changamoto hiyo amesema kwamba kuna upungufu wa wataalam mbali mbali wa sekta ya mifugo na dawa yake Mhe. Waziri amezungumza kwenye ukurasa wa 5 kwamba wamekusudia kuongeza uwezo wa taalum kwa wafanyakazi na kuajiri wataalamu zaidi ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za mifugo. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo zuri lakini nimepata wasi wasi kwamba bado Wizara hii haina umakini katika kuajiri wataalamu. Kwa hivyo ningeomba Mhe. Waziri awe makini sana katika kuajiri wataalamu na nimepata ufanisi huo kwa sababu nimegundua kama alivyosema Mhe. Salmin kuwa kuna tetesi kwamba Wizara yake imeajiri wataalamu vijana watano kutoka Chuo cha Kizimbani bado wakiwa ni wanafunzi. Hili ni kosa kisheria. Sasa sitaki nitaje majina ya wale walioajiriwa lakini nitampatia Mhe. Waziri, tumeyazungumza haya kwamba mtu ambaye bado anasoma hapaswi kuajiri ni kosa. Kwa hivyo serikali inakuwa nzito, serikali inakuwa na masikio ya chini haisikii na inaendelea kufanya ajira kinyemela bila ya utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, vijana hao walioajiriwa wamemaliza *Certificate in General Agriculture* wameajiriwa Idara ya Mifugo kama ni wataalamu wa mifugo. Ana *certificate in general agriculture* ndio anaajiriwa kuwa mtaalamu wa mifugo tutafika wapi? Kwa hivyo sitaki nitaje majina lakini nakwambia kwamba hatuwezi kwenda hivi maadam mtu mwanafunzi lazima asubiri amalize ili aajiriwe. Zanzibar kuna vijana wengi waliosoma Kizimbani ambao hawana kazi kwa nini tuwaajiri wanafunzi? Mhe. Mwenyekiti, hili nitamletea majina Mhe. Waziri na sitokubaliana nalo, naomba sana tujenge tabaka la wakubwa na wadogo, wanaosoma waendelee kusoma wakimaliza waajiriwe. Hili Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana Mhe. Waziri alifanyie kazi.

Jengine ambalo nataka niliseme ni ukurasa wa 7 changamoto za sekta ya uvuvi. Mhe. Waziri amesema kwamba kwanza una changamoto ya kuongezeka kwa shindikizo la uvuvi, yaani *fishing pressure* katika maeneo ya hifadhi kutokana na ongezeko kwa idadi ya wavuvi. Lakini la pili kwamba kuna ukiukwaji mkubwa wa sheria ya uvuvi unaofanywa na baadhi ya wavuvi. Mhe. Mwenyekiti, sawa haya yapo lakini bado nasema kwamba serikali haijakuwa makini tumesema mara kadhaa humu ndani kwamba sheria ya uvuvi tuliyoipitisha ina mapungufu yake, wazanzibari ambao asilimia kubwa ni wavuvi wanalalamika na sheria hii, kwa nini serikali iwe kaidi

isikae na Tume kupitisha sheria wakaipitia sheria hii wakairekebisha vipengele ambavyo vinawakwaza wananchi wetu tukapata ufanisi kwenye uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, masuala ya *fishing presure* nadhani sio tu kwa wazalendo kama kuna *fishing pressure* kubwa ni kwa meli za kigeni ambao zinavua bahari kuu, lakini serikali haitaki kusikia hilo. Wanamuonea mvuvi wa Kwahani, Micheweni, Kiwani kwamba ndio mharibifu wa mazingira lakini wanashindwa kusema hoja kwamba kuna wavuvi wa nje meli za kigeni wanatuharibia mazingira yetu wanashindwa kusema hivyo serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna *fishing pressure* kubwa ni ya meli za kigeni ambayo zina athari kwa mazingira na kuathiri uchumi wa nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atoe tamko kwa hili kwa nini wanakuwa wazito kudhiti uharamia wa wizi wa samaki wetu katika bahari kuu. Tumekuwa tukiwaambia mara nyingi lakini hebu tuambiwe ni mtaji wa nani kwa nini serikali tunawaelimisha na kuwaambia kwamba kuna wizi mkubwa wa samaki wetu baharini lakini wanashindwa kuchukua hatua, badala yake anaonewa mvuvi wa dagaa, mvuvi wa pweza na chaza ndio wanachukuliwa hatua. Anafungwa, anakamatwa mitego inaharibiwa lakini hawa mapapa ambao wanatuharibia uchumi wa nchi hakuna hatua inayochukuliwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kifungu hiki mimi naona udhaifu mkubwa wa serikali ni wa serikali katika kusimamia raslimali bahari na raslimali fedha. Mhe. Mwenyekiti, mwaka juzi ilikamatwa meli moja tu na maarufu meli ya Magufuli ina samaki zaidi ya tani mia tatu na hakuna hatua iliyochukuliwa. Zanzibar imekuwa inafanya kazi gani lakini Mzanzibari mwenye kuvua vidagaa imekuwa *issue*. Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana mimi kwamba Wazanzibari wanaharibu mazingira lakini basi waone kwamba raslimali samaki, raslimali bahari inawasaidia vipi Wazanzibari wetu badala ya kuwaonea wananchi wadogo wadogo. Kama kuna udhaifu mkubwa wa serikali hii ni kule kudhibiti raslimali bahari na kudhibiti raslimali fedha tumeambiwa hapa asubuhi na mimi nilikuwa ninayo hapa ile hoja kwamba bahari kuu tu na mimi nimpongeze mkurugenzi kwa kugundua wizi wa wachache wanaojinufaisha, bahari kuu tu zaidi ya bilioni mbili zimeibiwa, serikali inajua, serikali ipo hakuna hatua. Lakini atachukuliwa hatua mvuvi mwenye nyavu ya mita kumi tutakwenda wapi Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo kama kweli serikali iko makini basi itwambie huyu aliyeiba zaidi ya bilioni mbili za bahari kuu ni nani na kwa nini hajachukuliwa hatua labda kuna hatua zipi? Mimi sikubaliani na utaratibu wa kupeleka Polisi. Serikali hii imekuwa na utaratibu wa kupeleka Polisi kwa sababu ukipeleka Polisi ndio

tayari imekuwa ni damu, chukueni hatua mtu ametuibia mfilisini mali yake turejeshe mali serikalini. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atupe jibu nani aliyechukua fedha hizi kwa msingi gani ili tuone kwamba kweli muko makini katika kusimamia raslimali za nchi. Hatuwezi kuachia wajanja wachache kufisidi nchi huku Wazanzibari wakila hasara maisha yakiwa magumu katika taifa lao.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ni Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Mhe. Waziri aliyepita Mhe. Said Ali Mbarouk alifanya ziara katika jimbo langu eneo la Mwambe katika kisiwa cha Shamiani na aligundua kwamba kule kuna bwawa la kimaumbile limekaa kimaumbile lina maji zaidi ya mita nne, kina cha maji na mule mna samaki akaamua kama bwawa lile litakuwa ni kituo cha kufanyia utafiti wa viumbe vya baharini.

Mhe. Mwenyekiti ninamuomba Mhe. Waziri basi anambie nini hatua ya serikali katika bwawa lile ili wananchi wa Jimbo la Kiwani na Wazanzibari wote wapate kujua utafiti hasa wa samaki na viumbe vya baharini katika eneo lile la bwawa la Shamiani kule Mwambe. Mhe. Mwenyekiti niseme kwamba serikali isifanye masihara Wazanzibari wamekuwa na shida sana ya maisha kwa sababu ya udhaifu wa serikali. Watu wanagawana fedha kama njugu, watu wanagawana mali kama halua wakati serikali ipo tena ina viongozi makini tunavyoamjbiwa, wizi wanauona lakini hakuna hatua. Mimi napata mashaka Mhe. Mwenyekiti, na ninaamini kwamba inawezekana pengine kuna wakubwa wana maslahi yao. Haiwezekani kwamba mdogo anaiba hakuna hatua iwe hakuna jambo ndani yake. Mhe. Mwenyekiti, napata mashaka kwamba haiwezekani kama wadogo wanaiba wanajulikana hakuna hatua itakuwa kuna watu wana maslahi yao ndani ya wizi huu. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atwambie kwa nini hakuna hatua za msingi katika wizi unaofanywa.

Mimi sikubaliani sana kwamba hoja ni fedha ndogo, fedha ndogo kweli katika Wizara ya Uvuvi lakini jinsi gani fedha ndogo wanaitumia katika maslahi ya umma. Kwa hivyo fedha ndogo ni kweli lakini hiyo ndogo vipi inalindwa katika matumizi ya fedha za umma na ufanisi wa miradi mbali mbali. Inawezekana hiyo ndogo na mimi ninaamini kwamba asilimia 40 ya fedha za Serikali za Zanzibar zinaliwa. Kama utafanya utafiti hapa *more than 40 percent* ya fedha za umma zinaishia mifukoni mwa watu. Kwa hivyo si sababu tu ndogo ya fedha lakini nini nidhamu ya matumizi ya fedha za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii mimi nina imani sana ina Katibu Mkuu mzuri sana, Waziri mzuri sana, Naibu Waziri anafuatilia hadi vijijini. Katika Naibu Waziri ambaye anafanya kazi nzito anakwenda *deep* ni Naibu Waziri wa

Wizara hii, lakini bila ya hatua hakuna ufanisi, twambieni ufanisi kwa wale ambao wamehujumu mali za umma kupitia Wizara yako, vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, sitounga mkono hotuba hii. Hatuwezi kumlinda mtu aliyeiba zaidi ya bilioni mbili ukamhukumu mnyonge aliyevua samaki vidagaa vinne.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba niseme tu kwamba Wizara imebeba kundi kubwa la Wazanzibari waliojiajiri. Kwa hivyo ni wizara ambayo ingehitaji umakini mkubwa, ingehitaji ufanisi mkubwa na umoja wa wavuvi wote wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, wavuvi wa Zanzibari na kamwe tusijenge imani kwamba wavuvi ni wakorofi. Katika watu watiifu wanaofuata sheria ni wavuvi kwa sababu bahari ndio mtaji wao Mhe. Mwenyekiti, lakini inawezekana kama serikali inatumia ubavu wakati mwengine kuwasaidia wavuvi.

Mhe. Mwenyekiti, *MACEMP* ni mradi mzuri sana lakini leo ufanye utafiti ni kiasi gani mali ambayo *MACEMP* wametoa maboti bado yako salama, maboti mengi yameuzwa na watu wamegawana kiholela. Kwa hivyo nia nzuri ya serikali na Mkurugenzi wa Idara hii alikuwa na nia nzuri tu kabisa, lakini kiasi gani serikali imelinda maboti yale. Kwa nini yalipotea kwa sababu watu waligawana bila ya utaratibu hakupewa mvuvi, kapewa mtu mwenye maslahi yake. Mhe. Mwenyekiti, na hili ni tatizo kwamba maboti yale wangepewa wavuvi, wavuvi wangeyatumia kwa uvuvi lakini kapewa Hija, kapewa Hassan, kapewa Juss si wavuvi ni watu maslahi yao Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe kwamba serikali itwambie maboti yale ni mangapi na mangapi yapo salama mikononi mwa wavuvi. Mhe. Mwenyekiti, kamati nyingi za uvuvi Unguja na Pemba walipewa watu si wavuvi na hii ndio athari yenyewe. Nitoe wito kwa serikali tuache tabia ya kusaidiana, mvuvi apewe mvuvi, mchangaji apewe ng'ombe na mwalimu apewe vitabu na wanafunzi

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba hii ni Wizara muhimu sana na mimi nikuombe sana kwamba ili tukupitishie mambo yako kwa urahisi tusaidie basi wale wanaohujumu fedha za umma ili tuamini kwamba fedha za umma zinalindwa katika misingi hiyo.

Mimi nipendekeze kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mkurugenzi wa Bahari Kuu ametusaidia kuonesha kwamba kuna wizi katika Idara yake, naomba Baraza la Wawakilishi Waziri akubali hoja yangu kwamba sasa Mkurugenzi na wataalamu wake tuongeze na timu ya Wawakilishi fulani tuchunguze wizi huu ni wizi mkubwa sana, tofauti mnavyoufikiria kwamba ni bilioni moja tu. Kuna wizi mkubwa sana sana. Kwa hivyo Mkurugenzi yule mwenye nia nzuri Wawakilishi wapo wachaguliwe tukafanye utafiti wa kina

tujue ni kiasi gani fedha za umma zimepotea ili tuwabainishe wananchi, kuwa serikali hii tukiwaachia hawatamgundua mwizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaombe Wawakilishi wenzangu kuwa serikali inavyojua hawatomgundia mwizi watakupiga maneno tu blaa blaa, maana yake mwisho watu wananufaika. Kwa hivyo niombe Baraza la Wawakilishi Wajumbe wenzangu tukubali basi kujenga hoja kwamba tuunde Kamati Teule chini ya Mkurugenzi wetu yule tufanye utafiti ili Wizara hii tuwagundue wale wanaohujumu fedha za umma kwa msingi wa kujinufaisha. Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni hiyo Mhe. Waziri akiikubali nitaunga mkono hoja, asipoikubali sitounga mkono hoja hii. Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana kwa utulivu wenu na kwa michango yenu mbali mbali ningesema kwamba bado kulikuwa na watu ambao wamejiandikisha kuchangia, lakini kwa bahati mbaya muda haututoshi kwa sababu matarajio yetu kesho kumaliza Wizara hii. Kwa hivyo kwa kesho nitawapa nafasi watu wawili wachangie ambaye ni Mhe. Suleiman Hemed na baadae atachangia Waziri wa Biashara Mhe. Nassor Mazrui na baadae tutampisha Mhe. Waziri na yeye vile vile aje afanye majumuisho.

Baada ya hayo ninawashukuru sana ninaahirisha kikao hadi kesho Ijumaa, Ahsanteni ninawashukuru.

(Saa 8.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 26/7/2013 saa 3.00 asubuhi)